

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 2 Julai, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mne Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) Pamoja na (Utawala Bora) kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UHUSIANO NA URATIBU):

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,
Uhusiano na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) Pamoja na (Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

MHE. KULIKOYELA K. KAHIGI - MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA) PAMOJA NA (UTAWALA BORA):

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani ya Ofisi ya Rais (Menejimentii ya Utumishi wa Umma) Pamoja na (Utawala Bora) Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Katibu ili atuongoza ratiba yetu ya leo, nasimama kwa mujibu wa Kanuni kuwapatia taarifa ifuatayo:-

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika wetu, Mama Anne Makinda, hatakuwa hapa Bungeni kwa siku kadhaa, amepata msiba, amefiwa na Bibi Zena Stephan Semamba. Huyu Bibi Zena Stephan Semamba alikuwa ndiye mtunzaji wa Marehemu Mama yake mzazi katika kipindi kile ambacho Marehemu Mama yake mzazi alipokuwa akiugua lakini katika kipindi chake cha uzee huyu Marehemu Zena Stephan Semamba ndiye alikuwa mtunzaji mkuu wa yule Marehemu Mama yake na Mheshimiwa Spika.

Kwa hiyo, huyo mtunzaji naye Mwenyezi Mungu amemwita. Hivyo basi Mheshimiwa Spika, anawajibika kwa kweli kwenda kuhakikisha anamfanyia mazishi huyu Mama yetu Zena Stephan Semamba. Kwa hiyo, hatutakuwa naye hapa kwa siku zile ambazo atakuwa anashiriki kikamilifu kwenye msiba huo. Kwa hiyo, nimesimama kuwapa taarifa hiyo. Basi sisi tutaendelea na shughuli hizi mpaka hapo Mheshimiwa Spika atakaporudi ataungana nasi kuendelea na kazi zilizopo Bungeni.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 108

Gharama za Maonyesho ya Miaka 50 ya Uhuru

MHE. SALIM HEMED KHAMIS (K.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED) aliuliza:-

Je, hadi sasa Serikali imetumia kiasi gani cha fedha kwa kila Wizara kwa ajili ya maonyesho ya miaka 50 ya Uhuru?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Siha ninaomba kutoa pole sana kwa Mheshimiwa Spika, kwa msiba huu ambao umetutangazia sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara yalifanyika nchi nzima kwa kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 1 Juni, 2011 hadi tarehe 12 Desemba, 2011.

Serikali iliadhimisha Kumbukumbu hii muhimu ya taifa letu kwa faida ya Watanzania na hasa kukijengea uzalendo kizazi cha sasa ambacho hakikuwepo wakati tulipopata uhuru. Aidha, kupitia maadhimisho hayo ya kihistoria, nchi yetu imejitangaza nje ya nchi na kujiletea sifa kubwa na pia kuvutia wawekezaji na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanikisha maadhimisho hayo, Serikali ilipanga kutumia shilingi bilioni 30. Hata hivyo katika kubana matumizi Serikali imetumia shilingi bilioni 27.5 (27,540,218,803) ambazo ni matumizi ya Wizara, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi mbalimbali.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sherehe kubwa za kuadhimisha miaka 50 ya uhuru ambazo zilifanyika nchi nzima Mikoa na Wilayani na ambazo zimegharimu mabilioni ya fedha.

(a) Je, nini tathimini ya Serikali kuhusiana na jambo hilo?

(b) Kwa kuwa kupanga ni kuchagua na kwa kuwa hivi sasa nchi yetu inakabiliwa na mambo muhimu ya kimsingi kwa mfano upungufu mkubwa wa madawati mashulenii, vitabu vyatatu na wanafunzi, nyumba za walimu, madaktari na wafanyakazi wengine wa Serikali, maabara na kadhalika.

Je, isingekuwa jambo la msingi kwamba Serikali ingefanya sherehe moja tu kubwa ya kitaifa ili kuokoa fedha ile ambayo ingetumika kujenga shule, kununua madawati, vitabu na kadhalika? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Salum Hemed Khamis, kama ifuatavyo:-

Kwanza kuhusu tathimini sisi wote ni mashahidi Wabunge wote na Tanzania, vizazi hivi vipyta vyote vimeona jinsi ambavyo tumeweza kuiweka nchi yetu katika historia yake. Nchi ambayo haina historia imekufa. Kwa hiyo, tulichofanya hapa wako watoto ambao wamezaliwa hawajui kipindi hiki cha uhuru kilikwenda kwendaje.

Kwa hiyo, leo wanajua historia yetu. Wanajua tulianza na vyama vilivyoanza, vilivyopigania uhuru Tanzania Bara na Tanzania Visiwani wanajua. Wanajua mifumo mbalimbali, mabadiliko tuliyopata, siasa ya ujamaa na kujitegemea, misukosuko tuliyopita nayo katikati, kuhama hama katika mfumo wa Chama Kimoja kwenda kwenye vyama vingine na ninyi wote mliona Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tulishiriki katika jambo haraka haraka ni kwamba kila mtu aliridhika kwamba walau tumeweza kuwafanya Watanzania na wale wengine walioko nje ya nchi kwamba nchi yetu imetimiza miaka yake 50 jambo ambalo kwa maoni yangu ni jambo la kujivunia sana

kwamba tumeweza kuonyesha historia yetu. Tumeweza kujua kwamba tumetoka wapi. Je, ni kiasi gani tumeweza kuelimisha watoto wetu, hospitali zilizojengwa, tumeweza kuonyesha barabara, tumeweza kuonyesha viwanda na mambo mengine ya kiuchumi mbalimbali ambayo yametokea katika nchi yetu.

Kwa hiyo, kwenye hili hatuhitaji kumwita mtu kutoka nje atufanyie tathimini, mafanikio ni makubwa tulifanya nchi nzima na sisi wote tuliona jambo lile. (*Makof*)

Sasa linakuja jambo hapa kwamba hizi hela zinazozungumzwa hapa kwa nini msingezi peleka kwenye madawati, vitabu na kadhalika. Hili tukio la miaka 50 ya taifa si jambo dogo hata kidogo.

Kwa maana ya kwamba haya yote ni mafanikio ambayo nimesema hapa yasingelikuwepo sasa kwa maana ya kwamba watu wasingejua, wanafunzi unawaona wamekaa pale juu wao hawajui kipindi hicho cha nyuma kilikuwaje, wamefahamu leo. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ambaye ameuliza swali hapa leo watoto hao wanajua Hamad Rashid Mohamed aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Leo watoto wa Tanzania wanajua kwamba amewahi kuwa Naibu Waziri wa Fedha, leo wanaweza kujua kwamba Makamu wa Rais wa Kwanza Zanzibar pale, leo wanajua alitoka wapi mpaka amefika hapo alipofika. Yako mambo mengi tu ambayo unaweza

ukayazungumza hapa ambayo tunatakiwa sisi Watanzania tufike mahali tujidai, tufike mahali tuseme kwamba tunajivunia taifa letu kwamba limeweza kufika katika hatua hii lilipo.

Kwa hiyo, mimi nasema kusema kwamba tungepeleka katika elimu tunafanya hivyo, lakini jambo hili pia nalo ni muhimu sambamba na yale mambo ambayo nayazungumza hapa. Nashukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, wakati akisimama kwenye swali la nyongeza alisimama mtu mmoja tu mwuliza swali na nilishasema nimemwona mtu mmoja.

Na. 109

Uhamisho wa Walimu wa Taaluma na Elimu Maalum

MHE. MARTHA J. UMBULLA (K.n.y. MHE. AL-SHAYMAA JOHN KWEGYIR) aliuliza:-

Serikali ilitoa agizo la kutowahamisha watumishi wote wakiwemo walimu wanaojiendeleza kitaaluma na wahitimu wa fani mbalimbali ikiwemo elimu maalum:-

(a) Je, ni kwa nini walimu wa taaluma na elimu maalum hususan ya watu wenye ulemavu wamekuwa wakihamishwa bila kuzingatia agizo hilo?

(b) Je, uhamisho huo unazingatia vigezo gani hadi kushindikana kuwatambua walimu wa elimu maalum?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegiyir, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b).

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inawatambua na kuwathamini sana wanafunzi wenyе mahitaji maalum na wakati wote imekuwa inatoa kipaumbele cha kuhakikisha walimu wenyе fani husika wanapatikana ili kuweza kuwapa fursa sawa ya kupata huduma ya elimu.

Uhamisho wa watumishi katika mamlaka za Serikali za Mitaa hufanyika kwa kuzingatia mahitaji kiikama na maombi ya watumishi husika. Kutokana na uchache wa walimu wenyе taaluma ya elimu maalum, Serikali imekuwa inahakikisha na kuelekeza kuwa wanapohamishwa au kupangwa wapelekwe katika maeneo yenye mahitaji.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wanapoomba kuhama wana maelezo yanayotofautiana kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kumfuata mwenzi wake, ugonjwa, kubali mazingira ya kufanya kazi baada ya kukaa kituo

kimaja kwa muda mrefu, kujijandaa, kustaafu na mtumishi kuwa na wazazi wanaomtegemea. Jambo la msingi ni waombaji kutimiza masharti ikiwemo ridhaa ya mwajiri anakohamia kumpokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo walimu ambao huijendeleza na kupata sifa mpya, Serikali imekuwa inatoa maelekezo kwao kurejea kwa waajiri wao ili wapangiwe majukumu kulingana na sifa wanazopata.

Katika kundi hili wapo wahitimu ambao wakati fulani hulazimika kuhamishiwa katika kituo chenye mahitaji kwa sababu kabla ya kujijendeleza walikuwa katika shule zisizo na wanafunzi wenyе mahitaji maalum. Utekelezaji wa zoezi hili hutegemea uwepo wa fedha za uhamisho na kukamilika kwa taratibu za kiutumishi kwa wale wanaohitajika kutoka shule zilizo katika mamlaka za Serikali za Mitaa kwenda Mwajiri au Wizara nyingine.

Mfano ni uhamisho wa walimu kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenda Vyuo vya Ualimu au shule zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu naomba nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada za kufuatilia hali ya utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenyе mahitaji maalum. Nimsihi tu Mheshimiwa Mbunge kuwa kama lipo jambo la kipekee Serikali itaendelea kutoa ushirikiano wa dhati kwake katika kupata ufumbuzi. (*Makofi*)

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa Majibu yake mazuri. Nina swali moja dogo la nyongeza.

Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba pamoja na kwamba uhamisho huwa ni suala la hiari na maelewano na la kisheria, lakini Waziri atakubaliana na mimi kwamba ni vizuri walimu wa elimu maalum kama hawa wanapopata uhamisho iangaliwe vizuri kwamba pale wanapohamishiwa wanakwenda kuwashudumia watu wenye ulemavu maalum kama ambavyo walikuwa wameajiriwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Martha Umbulla kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa sharti tu mwalimu anapohama kutoka kule anakotoka kwa mfano kutoka pale kwako Songea Peramiho lazima umpe kitu kinachoitwa *disturbance allowance* na wale kule anakokwenda lazima waseme tuko tayari kumpokea na atachukua nafasi ya ama aliyekuwa marehemu fulani au ambaye alihamishwa na kule wanamlipa kitu kinachoitwa *subsistence allowance*.

Sasa mazingira ya nyumba, mahali pa kuishi na vitu vingine yote yatategemeana na kule anakokwenda, hatuna tatizo katika hilo.

Utaratibu wa kawaida ambao unahamisha watumishi ndio utaratibu tu naotumia hata hawa ambao wana vipaji maalum kwa maana ya kwamba jinsi yaku-deal na walemaru wasioona, wasiosikia hapa kwetu kuna Bwigiri, kuna Kigwe wakija hapa tunaangalia mazingira hayo yote yanayozungumzwa lakini hatuna tatizo na hilo analosema Mheshimiwa Mbunge, tunakubaliana naye. (*Makofi*)

MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nianze kwa ku-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, sasa swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule nyingi ambazo tumepita kuna uhaba mkubwa sana wa walimu wa taaluma hususani kuhudumia watu wenye ulemavu. Serikali ina mpango gani wa kuongeza idadi ya walimu hawa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sikusikia jina lake.

MWENYEKITI: Dkt. Anthony Gervase Mbassa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Dkt. Mbassa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza na watu wa kitengo hiki mara tu baada ya kupata hili swali. Tumshukuru sana Mheshimiwa Kwegyir ambaye anafuatilia sana masuala ya walemvu. Kila wakati tumekuwa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba walimu hawa wanaongezeka na idadi yao inaongezeka. Sina takwimu hapa kwamba ni kiasi gani tumefanya katika hilo eneo na niombe tu kumthibitishia kwamba kila wakati idadi hii imekuwa inaongezeka, wengine wako katika shule wanafundisha, lakini anaamua kwenda Chuo Kikuu ili kwenda kujifunza mafunzo maalum kwa ajili ya walemvu. Mimi mwenyewe nimejifunza habari hii, mwalimu wangu pale Chuo Kikuu Dkt. Gichoi ndiyo alikuwa anafundisha, nafikiri siku hizi wanamwita Dkt. Mboya. Ametufundisha eneo hili kwa hiyo, nalifahamu jambo analolizungumza hapa. Lakini idadi yao imekuwa inaongezeka kutohana na mahitaji haya ya nchi kwa ujumla. Baadaye nitamtafutia takwimu ili kuweza kuona jinsi ambavyo imekuwa inapanuka.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi sana kupata nafasi hii. Kwa kuwa tatizo kubwa kama swali lilitolizwa sasa hivi ni uhaba wa walimu wenyewe na kwa kuwa kuna chuo cha walimu wenyewe mahitaji maalum kule Lushoto ambacho kinaitwa SEKUKO na tatizo kubwa ni kupata vifaa vya kufundishia. Je, Serikali inatamka nini kwa Chuo hiki ili kipate msaada tupate walimu wengi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa

Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Shekifu, Mbunge wa Lushoto kama ifuatavyo:-

Kama sikosei na atanisahisha, nadhani chuo anachokizungumza hapa ni chuo ambacho ni cha binafsi na ambacho tunaweza tukakaa, tukazungumza nao, lakini hatuwezi sasa kama Serikali hapa tukakitamkia kwamba kifanye hivi, unajua kuna mambo ya *public private partnership* ni nini, lakini niseme kwamba ni wazo zuri, tunaweza tukawasiliana nao tukaona kwamba wanafanya nini, lakini kwa *perspective* ya Serikali hatuwezi kusema kitu kwa sababu bado hiki ni chuo cha binafsi.

Na. 110

Vibali Vya Ujenzi wa Nyumba

MHE. ALI KHAMIS SEIF aliuliza:-

Je, baada ya mwananchi kukamilisha taratibu za kuomba vibali vya ujenzi wa nyumba unahitaji muda gani ili Serikali kutoa vibali vya ujenzi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007 kifungu cha 35(i), Serikali za Mitaa (*Planning Authority*) zinatakiwa kutoa kibali cha ujenzi ndani ya siku sitini 60 tangu mwombaji awasilishe maombi yake. Aidha ndani ya muda huo mamlaka zinatakiwa kumjumlisha mwombaji kuwa amekubaliwa au amekataliwa ombi lake na kutaja sababu zilizosababisha ombi lake kukataliwa. Kwa mujibu wa kifungu cha 35(iv) cha Sheria hiyo kinabainisha kuwa endapo mamlaka zitashindwa kumjulisha mwombaji kuwa amekubaliwa au amekataliwa ombi lake ndani ya siku 60 tangu awasilishe ombi lake, mwombaji atatakiwa kuwasiliana na mamlaka husika ili kupata kibali hicho kwa maandishi.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuwa mhusika kama hajapata jibu au kibali cha ujenzi anatakiwa aende katika mamlaka husika na alete barua au apelike barua kwa maandishi.

(a) Je, kama mwananchi ameshaandika barua hiyo, na bado jibu hajalipata. Mwananchi huyu aende katika chombo gani ili aweze kukipata kibali hicho katika kupeleka malalamiko yake?

(b) Kuna utaratibu wa vikao vinavyotoa vibali vyatuhusu ujenzi kukutana kila baada ya miezi mitatu kitendo ambacho kinaleta urasimu mkubwa katika kupata

vibali hivi. Je, Serikali itakubaliana nami kuwa sasa wakati kuwa vikao hivi vikutane kila baada ya mwezi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ali Khamis Seif, kama ifuatavyo:-

Mimi namwelewa rafiki yangu anachozungumza pale anaongea jambo la msingi. Tujifanye kwamba vibali vilitoka jana pale na leo umepeleka ombi lako pale, unataka kupata building permit. Maana yake utakwenda tena siku 90 ndipo upate kile kibali na Sheria inasema siku 60 hapa ndicho anachokisema pale yani mimi wala siwezi kubishana nae pale.

Sasa huyu mwananchi huyu atalalamika kama anavyosema pale kwa sababu hataangalia. Sasa kikao kile cha Kamati anachokizungumza hapa ni tofauti na kikao cha Kamati ya Fedha ambacho kinakaa kila mwezi mara moja amabcho tunaweza tukazungumza hapa ni kwamba sasa sisi wote tulione hilo tatizo ambalo linajitokeza hapa, tuweze kuangalia kama Sheri aile imekaa sawa sawa ili iweze kukidhi hiyo. Hiyo *contradiction* tunaiona pale. Kama unazungumza habari ya siku 60 lakini Kamati inakaa baada ya miezi mitatu, kuna *problem* pale.

Kwa hiyo, tunalionwa wazo lako Mheshimiwa na nikuombe tu kwamba hili tutajaribu kuliangalia ili tuweze kuona saa kwamba je turudi kwenye Kamati ile

ya Fedha na Uchumi na Utawala pale ndiyo wafanye kazi hii badala ya hiyo Kamati inayofanya kazi na kadhalika.

Sasa hili la kwamba hajapata sasa, tukisema hapa tuchukulie tu kwamba kwa vile hujapata ni *automatic* anachukua pale, pale Temeke pale palianguka gorofa pale likadondoka chini kama muhogo kapu pale likakatika pale, tukiruhusu hapa tukasema, tunachosema hapa tunazitaka mamlaka zetu na kama Mheshimiwa Mbunge analo tukio ambalo anaona kwamba kuna watu wengine wanavuta vuta tu pale kama wanataka kushawishi jambo fulani, ninakuomba utusaidie kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tujue nani hao wanaofanya hivyo kwa sababu utaratibu unatutaka mwananchi apate haki hiyo na akienda katika Halmashauri apewe barua yake pale anayotakiwa.

Kama Wabunge mnao watu ambao unaona kwamba anadilidali imepita miezi sita hatoi, anazungusha zungusha pale, kwa sababu kuna mazingira ambayo naona unayajenga pale, utusaidie, halafu sisi tutashughulika nao.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kunipa nafasi niulize swalí moja la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa kumekuwa na wimbi kubwa la watu wanaojenga katika maeneo ya wazi katika Halmashauri mbalimbali nchini ikiwepo maeneo ya shule, mipira kwa ajili ya michezo ya wanafunzi, hifadhi za maji na *recreation centres* katika Miji. Je, Halmashauri sasa haioni sasa kwamba ni wakati

muafaka wa kuanzisha *land rangers* watakaozuia ujenzi huo batili ili kuhakikisha kwamba maeneo hayo hayajengwi?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO

YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Pauline Gekula kwa swali lake zuri sana. Nipende tu kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendelao ya Makazi ya mwaka 2011/2012, tulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeanza mchakato wa kurejea kada hiyo ya askari arthi (*Land Rangers*) na kwa kuanzia, tulianza kwa majaribu kwa kuajiri *land rangers* 15 ambaao tuliwatawanya katika Manispaa ya Jiji la Dar es Salaam na kazi wanayofanya *land rangers* wale imeonekana kwamba ni nzuri.

Kwa hiyo, wito ambaao tumetoa kwa Halmashauri zote ni kwamba wafanye taratibu za kuomba vibali ili waweze kuwa na *land rangers*. Wamesaidia sana kuweza kutambua uharibifu unaofanyika na hivyo kujulisha mamlaka zinazohusika na kuzuia mapema.

Na. 111

Watumishi Kukimbia Mazingira Magumu ya Kazi

MHE. MENDRAD L. KIGOLA (K.n.y. MHE. KAIKA S. TELELE) aliuliza:-

Wilaya nyingi nchini zina mazingira magumu ya kufanyia kazi, hali inayofanya watumishi wengine wa

Serikali kukimbia wanapopangiwa vituo vyatya kazi katika maeneo hayo hususan walimu:-

Je, Serikali iko tayari kuwaruhusu wazawa wa Wilaya husika kwenda kufanya kazi kwenye Wilaya zao bila kujali ugumu wa mazingira, bila sharti la kutakiwa kutakiwa kutafuta mtumishi wa kubadilishana nao?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Sining'o Telele, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa baadhi ya Wilaya zina mazingira magumu ya kufanya kazi hali inayofanya watumishi wengi wa Serikali wakiwemo walimu, kutoripoti vituoni wanapopangiwa kazi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo dhamira ya dhati ya kushughulikia tatizo la upungufu wa watumishi katika maeneo yenye mazingira magumu ili kuwafanya watumishi waweze kubaki na kufanya kazi katika maeneo hayo. Katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(a) Kulegeza masharti ya kuajiri watumishi wa kada kama za Afya, Elimu, Kilimo na Mifugo ili wahitimu wa fani hizo wasilazimike kuomba ajira na kufanya usaili na badala yake wapangiwe vituo vyatya kazi moja kwa

moja mara tu wanapomaliza kufuzu masomo yao.
(Makofi)

(b) Kutunga Sera ya Malipo ya Mishahara na motisha katika utumishi wa Umma ya mwaka 2010 ambayo imezingatia pia suala la mazingira magumu. Kwa sasa Serikali imekamilisha mkakati wa utekelezaji wa Sera hii.

Katika mkakati huo, Serikali imeainisha vigezo hivyo, maeneo yenye mazingira magumu na kwa msingi wa vigezo hivyo, maeneo yenye mazingira magumu yatabainishwa ili watumishi waliopo katika maeneo hayo wapewe motisha *incentives* na kuboreshwa mazingira yao ya kazi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo utaratibu wa kufanya kazi kwa kuzingatia uzawa bila kubadilishana watumishi wa Wilaya nyingine utaruhusiwa, upo uwezekano mkubwa wa kuleta ubaguzi na kujenga matabaka katika nchi hii. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi kwamba mfumo wa sasa umejenga utaifa zaidi.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri na kwa kuwa kuna tatizo kubwa sana la watumishi hasa upande wa afya na kuna watu ambao wameshasoma kozi ya mwaka mmoja na wako majumbani na wako tayari kufanya kazi mahali popote.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwaahidi hawa ambao wako majumbani kwamba watapata hizi ajira za moja kwa moja?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kigola la nyongeza kama ifuatavyo:-

Wale wanaochukua kozi ya unesi ya mwaka mmoja, wanaweza wakaajiriwa kama *nursing attendant*, lakini mara nyingi tunapendelea zaidi kwamba wajiendeleze ili wafikie *level midwife*. Wale ma-nurse *attendant* tunaweza tukawaajiri lakini kulingana na nafasi. Lakini mara nyingi tunapenda wajiendeleze wawe *nurse midwife* ili waweze wakafanya kazi zao vizuri.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ningependa kuiuliza Serikali je ina utaratibu gani kwa watumishi ambao waume zao wako Mikoa mingine na wanapewa masharti katika swali lake la msingi kwamba kutafuta watu wa kubadilishana nao wakati tayari ni wana ndoa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, kama ifuatavyo:-

Kuhusu wale ambao ni wanandoa. Wanandoa inategemeana na nafasi katika sehemu husika. Kama

hakuna nafasi, hakuna njia kwa sababu kama tukisema wanandoa wote wa Dar es Salaam waume zao au wake zao wawafuate ina maana kwamba Dar es Salaam inaweza ikafurika watumishi wengi. Kwa hiyo, hilo suala lazima apate mtu wa kubadilishiana inategemeana na mazingira husika.

Sehemu nyingine anaweza akampata wa kubadilisha naye, sehemu nyingine kuna nafasi, kama kuna nafasi, hiyo haina tatizo la kubadilishana. Waheshimiwa Wabunge tukisema tufuate hasa kwamba kila anaeolewa aende sehemu Fulani, utakuta katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Vijiji ni hawatapatikana watu kwa sababu mara nyingi wamama wakifika katika Halmashauri za Wilaya anafunga ndoa ili aletwe Mjini. Sasa tutakosa watu wa kufanya kazi katika baadhi ya sehemu tukiruhusu hiyo. (*Makof*)

Na. 112

NHC Kujenga Nyumba 50 Longido

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y. MHE. MICHAEL L. LAIZER) aliuliza:-

Mwaka 2007 Serikali iliahidi kuwa Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) litajenga nyumba 50 katika Wilaya mpya ya Longido:-

Je, ujenzi huu utaanza lini?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa mwaka 2007 Serikali illahidi kutekeleza mradi wa kujenga nyumba 50 katika Wilaya ya Longido. Ahadi hiyo ilikuwa ni sehemu ya mkakati wa Serikali kujenga majengo ya ofisi na nyumba za makazi katika Mikoa na Wilaya mpya zilizoanzishwa katika kipindi hicho. Hata hivyo, utekelezaji wa mradi huo katika Wilaya ya Longido haukuanza mara moja kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kupatikana kwa ardhi na viwanja kuandaliwa mradi wa ujenzi wa nyumba 50 katika Wilaya ya Longido unatarajiwa kuanza mwaka 2012/2013.

Hii ni sehemu ya utekelezaji wa mpango mkakati wa Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) wa kujenga nyumba 15,000 kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (2010/2011-2014/2015), kama inavyoelekeza llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya ujenzi wa nyumba kupitia Shirika la Nyumba la Taifa inatarajiwa kuongezeka baada ya Shirika kutiliana sahihi mkataba wa kibiashara na mabenki manane nchini. (*Makof*)

Mabenki hayo ni *Azania Bancorp*, *NMB-Bank*, *NBC Bank*, *Kenya Commercial Bank*, *Exim Bank*, *Commercial Bank of Africa*, *Bank of Africa* na *Stanbic Bank*. Mabenki hayo yatawakopesha wananchi kwa ujenzi na ununuzi wa nyumba za Shirika mikopo ya muda mrefu kuanzia miaka 15 hadi 20 kwa riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wizara yangu kupitia Shirika la Nyumba la Taifa inafanya mazungumzo na uongozi wa Wilaya ya Longido juu ya namna ya kugharamia miundombinu ya barabara, maji na umeme ili nyumba zitakazijengwa ziwe za gharama nafuu. Tunaamini kuwa kama Halmashauri ya Wilaya ya Longido wataendelea na ushirikiano wa karibu na Shirika, ujenzi wa nyumba hizo utakamilika ifikapo mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha Shirika la Nyumba la Taifa kutekeza mpango wake wa kuwezesha wananchi kupata nyumba bora za kuishi kwa gharama nafuu natoa wito kwa Halmashauri za Mji na Wilaya kutenga viwanja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kuishi, maofisi na biashara na kuvikabidhi kwa Shirika la nyumba la Taifa, kwa kuwa nyumba ni rasilimali muhimu katika maendeleo ya Taifa.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, nina maswali madogo mawili.

- (a) Kwa kuwa Wilaya ya Longido ni mpya na Halmashauri ni mpya na mapato ni finyu.

Je, Serikali iko tayari kufanya gharama za miundombinu ya umeme na maji kuwa sehemu ya mkopo huo wa muda mrefu?

- (b) Kwa kuwa Shirika la Nyumba la Taifa limenza mpango mzuri wa kujenga nyumba za kuwauzia wananchi katika Mikoa ya Dar es Salaama na Dodoma.

Je, ni lini mpango huo utaenda kwenye Mikoa mingine kama Mbeya, Iringa, Rukwa na Ruvuma?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO

YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa, Mwambalaswa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, suala la miundombinu kwa Wilaya ya Longido, Serikali, inachoweza kufanya ni kuhimiza Mashirika ya Shirika la Umeme nchini, *TANESCO* pamoja na Mamlaka za Maji, ziingize mpango huo katika sehemu za miradi yake ya maendeleo, ili iweze kuweka kuomba fedha kutoka *REA* na kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ratiba ya ujenzi wa nyumba za Shirika la Nyumba maeneo mengine ya nchi, kwanza kwa Mkoa wa Ruvuma, juma lililopita,

Wataalam na Viongozi wa Shirika la Nyumba, walikuwa Mkoani Ruvuma.

Walianzia Lindi, wakaenda Mtwara na kutoka Mtwara, wakaenda Lindi; kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya nyumba, pamoja na kufanya tathmini ya gharama za ukarabati wa nyumba za zamani zilizoko katika Mikoa hiyo kwa sababu, nyingi zimechakaa na tulitoa maelekezo ya kwamba, nyumba zote nchini zikarabatiwe ili ziweze kuwa katika mazingira mazuri ya kuishi binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia kwamba, kabla ya mwisho wa Mkutano huu, tutatoa ratiba ya ujenzi wa nyumba katika Wilaya zote nchini. Kwa hiyo, tutawagawia Waheshimiwa Wabunge, ratiba hiyo na tutaomba ushirikiano wenu ili Shirika liweze kutekeleza mpango huo.

MHE. HAROUB M. SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Mheshimiwa Rais, alitoa kauli kwamba, nyumba za *National Housing* zilizoko katika Jiji la Dar-es-Salaam watauziwa wakazi wake. Na kwa kuwa, kauli ya Mheshimiwa Rais, ni amri.

Je, watendaji wa Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa nini hawatekelezi kauli ya Rais? Je, si kumdhhalilisha Mheshimiwa Rais, huku?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,

napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shamis, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana kwamba, Mheshimiwa Rais, aliwahi kutoa maelekezo hayo. Sisi hatukatai kwamba, maelekezo ya Mheshimiwa Rais sio amri. Tunachosema ni bila ya shaka utakumbuka kwamba, mwaka jana 2011 Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, alizungumza hapa na kusema kwamba, kwa kuzingatia maoni ya wananchi walio wengi, kikiwemo Chama cha Wapangaji Tanzania, wasingeshauri nyumba za Shirika la Nyumba zilizopo ziuzwe, bali utaratibu uliowekwa na Serikali, wa kujenga na kuuza nyumba, ndio utekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la kuuziwa nyumba ni la siku nyingi. Mimi mwenyewe, zamani nilikuwa Katibu wa Wapangaji katika Mkoa wa Dar-es-Salaam. Kipindi nikiwa Katibu, tuliomba kuuziwa nyumba tulizokuwa tukiishi, lakini tulielezwa kwamba nyumba ambazo zimetaifishwa na Serikali, hazitauzwa. Kwa sababu, ni sababu ipi iliyotufanya tukataifisha, halafu leo tuje tubinafsische. Lakini pili, kuna nyumba ambazo tumejenga kwa kupitia msaada wa Serikali rafiki, nyumba hizo pia hatutauza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuzingatia hali hiyo. Kwa mfano ukiangalia nyumba zote za *llala pale*, *llala Flats*, zote zimejengwa kwa msaada wa nchi rafiki. Tukasema hatuuzi. Tukasema basi kwa sababu, tunazo kauli mbalimbali za viongozi zilizowatia matumaini na kuwapa matumaini wananchi hawa, tujenge nyumba

na kuwauzia. Huo ndio utaratibu ambao unaendelea hivi sasa wa kujenga nyumba na kuwauzia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano pale Dar-es-Salaam, tuna nyumba zaidi ya 200 zinajengwa pale Kibada za gharama nafuu ambazo zitauzwa. Nyumba ya vyumba viwili (2) itauzwa kwa 27,000,000/=, nyumba ya vyumba vitatu (3) itauzwa kwa 38,000,000/=. Ni bei rahisi ukilinganisha na hali halisi ya soko hapa nchini kwa sasa hivi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na swali namba 113 na 114, naomba niseme neno kidogo. Maswali haya mawili yanaulizwa na Wakuu wa Wilaya 2 ambao wameteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais, kuwa ni wawakilishi wa Mheshimiwa Rais, katika maeneo hayo husika. Sasa baada ya uteuzi wao kuwa Wakuu wa Wilaya, *in principle*, moja kwa moja wao ni sehemu ya Serikali. (*Makofi*)

Sasa kwa kutumia Kanuni 2(2), niseme kwamba, Kanuni hii inampa Spika, nafasi ya kufanya maamuzi, katika jambo ama shughuli yoyote ambayo haikuwekewa masharti. Sasa bado Kanuni zetu, haziwataji moja kwa moja Wakuu wa Wilaya, kama ni watu wasiopaswa kuuliza maswali. Lakini nadhani kwa Uendeshaji Bora wa Shughuli za Bunge, mtu anapokuwa tayari ni sehemu ya Serikali, sidhani kama tena na yeze anaihoji Serikali hiyo hiyo ambayo na yeze ni sehemu ya Serikali hiyo. (*Makofi*)

Sasa kwa maana hiyo ya Kanuni Namba 2, basi naomba nitumie Mamlaka ya Kiti changu, kuyaondoa Maswali hayo Namba 113 na Namba 114. Huko mbele, kama kutakuwa na majadiliano mengine ya Kisheria, basi tunaweza tukafikia maamuzi mengine.

Lakini kwa Mamlaka niliyopewa kwa Kanuni hii na kwa kuzingatia kwamba, uteuzi wao unawafanya kuwa ni sehemu ya Serikali, ninaomba Waheshimiwa Wabunge, mkubaliane na maamuzi ya Kiti, kuondolewa kwa Maswali hayo mawili na tutaendelea na Maswali mengine yanayofuata. Kwa hiyo, tunaendelea na maswali yanayofuata. (*Makofi*)

(Swali Naamba 113 na Namba 114, yaliondolewa katika orodha ya maswali ambayo yangeulizwa)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa tukiondoa Maswali hayo mawili, swali linalofuata linaenda Wizara ya katiba na Sheria. Swali hilo linaulizwa na Mheshimiwa Rita Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Iringa.

Na. 115

Sheria Zinazowanyanyasa Wanawake Kurekebishwa

MHE. RITA E. KABATI aliuliza:-

(a) Je, ni lini Sheria za Mirathi zitarekebishwa, kwani bado zinamnyanyasa mwanamke?

(b) Je, Serikali, inasemaje kuhusu Sheria ya umiliki wa Ardhi kwa wanawake?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Rita Enespher Kabati, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya Mirathi nchini kwetu, yanasmamiwa na Sheria Kuu nne (4). Sheria hizi ni Sheria ya Mirathi ya Kimila, zinazopatikana katika Kanuni za Urithi, kuitia Tangazo la Serikali Namba 436, la mwaka 1963; Sheria ya Mirathi ya Kiislamu, Sheria ya Kiserikali, ambayo ni Sheria ya India ya Mirathi ya Mwaka 1865, ambayo Bunge letu liliidhinisha itumike pamoja na Sheria ya Mirathi ya watu wenyewe asili ya Kiasia, wasio Wakristo. Aidha, pamoja na uwepo wa Sheria hizi, mtu ye yeyote anayo haki ya kurithisha mali yake kwa kutumia utaratibu wa kuandika Wosia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa niingie katika kipengele (a) na (b) cha swali la Mheshimiwa Rita Kabati.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali iko katika mchakato wa kuandaa Waraka wa Serikali (*White Paper*) kwa ajili, ya kukusanya maoni ya wananchi kwa nia ya kuziboresha Sheria hizo. Waraka huu wa Baraza la Mawaziri, tayari umeshaadaliwa na

unasubiri kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri, kwa ajili ya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira wakati taratibu hizi zinaendelea.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inatambua haki ya kila mtu kumiliki mali, ikiwa ni pamoja na ardhi, kama rasilimali mojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza azma hii, Bunge lako Tukufu, lilitunga Sheria ya Ardhi Namba 4 na 5 ya Mwaka 1999 na Sheria hizi zimeeleza bayana kwamba, wanawake wanayo haki ya kumiliki, kuhodhi, kutumia au kushughulikia ardhi sawasawa na wanavyofanya wanaume. Aidha Sheria ya Ardhi ya Vijiji, inaeleza kwamba, uamuzi wowote utakaotolewa kwa kufuata Sheria ya Mila, utakuwa ni batili endapo uamuzi huo utawanyima wanawake haki yao ya Kisheria ya kumiliki au kutumia ardhi.

Kwa mujibu wa Sheria hizi, mchango wa mwanandoa mwanamke (yaani nguvu zake) katika upatikanaji, uendelezaji na utunzaji wa ardhi, unatambulika na kumpa fursa ya kumiliki ardhi hiyo sawa na mwanaume, hata kama jina lake halijaandikwa katika Hati ya Kumiliki ardhi na ningependa hapo kidogo watu watie msisitizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999, imempa uwezo Msajili wa Hati, pale ambapo mwanandoa anaomba umiliki wa ardhi kwa ajili, ya matumizi ya familia, kuwasajili wanandoa wote wawili kama wamiliki wa pamoja wa ardhi hiyo. Hivyo, kwa ujumla utaona kwamba, Sheria hizi, Sheria Namba 4 na Sheria Namba 5 ya Mwaka 1999, imezingatia haki sawa baina ya wanawake na wanaume katika umiliki wa ardhi, tofauti na ilivyokuwa katika miaka ya nyuma, ambapo mwanamke alikuwa hana haki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kuwaelimisha wananchi wetu kuhusu haki za wanawake kumiliki ardhi kama zilivyo kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi.

MHE. RITA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri ambayo kwa kweli, Sheria hizi zimekuwa zikitunyanyasa sana sisi wanawake. Nina maswali madogo ya nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika jibu lake la msingi amekiri kwamba, mwanamke pia ana haki ya kumiliki ardhi. Je, Serikali, inasema nini kwa wanandoa ambao wamekuwa wakichukua mikopo katika benki na kuweka rehani za mali hizo za familia na baadaye kusababisha mali hiyo kuuzwa kwa mnada na kusababisha mwanandoa huyo kupata

matatizo? Pengine mwanandoa mwingine hajashirikishwa katika kuchukua madeni hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kumekuwepo na ongezeko kubwa sana la watoto wa mitaani (ombaomba) katika miji yetu mikubwa kama Dar-es-Salaam, Mwanza, hata Iringa sasa hivi pia. Je, Sheria inasemaje kuhusu watoto wanaozaliwa nje ya ndoa kumiliki mali ya familia?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rita Kabati. Swali la kwanza, ameuliza kuhusiana na ardhi au nyumba kuwekwa rehani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mkopaji anapoweka nyumba au ardhi ya familia kama rehani, anawajibu wa kumshirikisha mwanandoa mwenzake, ili aweze kuridhia nyumba hiyo au ardhi hiyo ambayo anaitumia kuweka rehani. Lakini pia, napenda kusitiza kwamba, kwa wanaokopesha, mabenki na taasisi nyingine au mtu binafsi, pindi unapomkopesha mtu ambaye ni mwanandoa, basi wewe kama mkopeshaji unao wajibu wa kujiridhisha kwamba, mwanandoa ameridhia.

Lakini sio hiyo tu, kujiridhisha kwamba, mtu huyo anayekopa ana ndoa au la. Na mwanandoa atakapokuwa ameridhia, basi wewe mkopeshaji unao wajibu wa kujiridhisha kama mwanandoa yule ni halali au si halali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika swali la pili, umeulizia kuhusiana na watoto wa nje ya ndoa, endapo wana haki ya kurithi mali. Kwanza kabisa kwa Sheria za nchi yetu, watoto wa nje ya ndoa, hawana haki ya kurithi isipokuwa wanaweza kurithi pale tu ambapo watakuwa wamehalalishwa kwa kufuata desturi au taratibu zinazojulikana na kutambulika katika jamii hiyo. (*Makofi*)

MHE. CECILIA DANIEL PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, katika Sheria ya Ndoa Namba 5 ya Mwaka 1971, ina kipengele kinachomkandamiza mtoto wa kike, kwa kutoa ridhaa ya mtoto wa kike kuolewa.

Je, ni lini Serikali, italeta hapa Bungeni, ili Sheria hiyo, iweze kufanyiwa marekebisho?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Katika swali lake ametaka kujua Sheria ya Ndoa Namba 5 ya Mwaka 1971, ambayo inatoa ridhaa kwa mtoto wa miaka 14 kuolewa, ni lini itarekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtakumbuka wakati wa Bunge la Bajeti Mwaka jana, wakati aliyekuwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Celina Kombani, wakati akihitimisha

Hotuba yake ya Bajeti aliahidi kwamba, Sheria ya Ndoa na Sheria za Mirathi, zitaingizwa katika mchakato wa kutafuta maoni (*White Paper*).

Tayari nimeshaeleza tangu awali katika jibu langu la msingi kwamba, hivi sasa tayari Serikali, imesha andaa Waraka ambao Waraka huo, tunakusudia saa yoyote kuupeleka katika Baraza la Mawaziri. Endapo utaridhiwa, basi mchakato na taratibu zingine zitaendelea. (*Makofii*)

Na. 116

Uandishi wa Miswada na Hukumu za Kesi kwa Kiingereza

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI aliuliza:-

(c) Je, ni lini Serikali, itaanza kuandika Miswada kwa lugha ya Kiswahili, kama ilivyo Sheria Mama (Katiba)?

(d) Je, ni lini kumbukumbu za Mahakama, zikiwa ni pamoja na Hukumu za Kesi mbalimbali zitaanza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Miswada kuwa katika lugha za Kiswahili. Kama ambavyo wote tunafahamu, Miswada yote ambayo imekuwa ikiletwa katika Bunge hili, kwa madhumuni ya kujadiliwa na kupitishwa, huandikwa kwa lugha ya Kiingereza kwa sababu, ya Mfumo wa Kisheria, ambao nchi yetu imeurithi kutoka katika Mfumo wa Kiingereza.

Mfumo huu wa Kisheria na utaratibu wa kurithi Sheria, kama ilivyofanya Tanzania, unafuatwa na nchi nyingine ambazo zamani zilikuwa chini ya utawala wa kikoloni wa Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mijadala yote kuhusu Miswada inayoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu, huendeshwa kwa lugha ya Kiswahili, ambayo inaeleweka na Watanzania walio wengi na Miswada hiyo, huambatana na tafsiri ya lugha ya kiswahili kuhusu madhumuni na sababu ya Miswada yenewe, ili wananchi wapate fursa ya kuelewa kile ambacho kimo katika Muswada.

Hata hivyo, Serikali inatambua umuhimu wa kutafsiri Sheria hizi kwa lugha la Kiswahili na ndio maana Wizara yangu, imeanzisha Kitengo cha Tafsiri, chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha Kitengo hiki cha Tafsiri, kimekuwa kikabiliwa na upungufu wa watumishi, hususan Wataalamu wa Tafsiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaanza mawasiliano na Chuo Kikuu, kupitia taasisi za taaluma

za kiswahili (*TATAKI*), ili kuona ni kwa kiasi gani basi Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali, inaweza kutumia huduma za taasisi hiyo ya taaluma za kiswahili katika kufanya tafsiri za Miswada mbalimbali kwa ajili, ya kuwasilishwa Bungeni.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake kipengele (b), kuhusiana na hukumu za Mahakama zetu nchini kuwa katika lugha ya Kiingereza; ni kweli, Hukumu za Mahakama zetu nchini, isipokuwa Mahakama za Mwanzo, zinapaswa kuandikwa katika lugha ya Kiingereza, kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinazoongoza mienendo na uandishi wa Hukumu katika Mahakama zetu.

Sheria na Kanuni hizo, ni pamoja na Kifungu cha 13(2) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11, Kanuni ya 2 ya Kanuni ya Lugha ya Mahakama, Tangazo la Serikali Namba 31, la Mwaka 1986 na Kanuni ya 5 ya Kanuni za Mahakama ya Rufani za Mwaka 2009 pamoja na Tangazo la Serikali Namba 368 la Mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa linalosababisha uandishi wa Hukumu kuwa katika kiingereza swahili, ni kutokana na masuala ya Kisheria kuwa katika Masuala ya Kiufundi.

Kama mnavyotambua Istilahi mbalimbali za Kisheria, bado hatunazo nyingi na maamuzi mbalimbali ya kesi, yamekuwa yakiangalia masuala mengine kama maamuzi mbalimbali ya nyuma. Kwa hiyo,

imekuwa ni vigumu kwa hivi sasa kuanza kutumia lugha Kiswahili katika uandishi wa hukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo Serikali, kwa kuona umuhimu wa kutumika kwa lugha ya Kiswahili katika tasnia ya Sheria, inaendelea kutafsiri Sheria zake katika lugha ya Kiswahili na inaangalia uwezekano wa kuona kwa namna gani tunaweza tukatumia lugha ya Kiswahili, katika uandishi wa kumbukumbu zetu, lakini pia katika kumbukumbu za Mahakama.

Lakini pia, tutambue kwamba, hata hivi sasa katika Mitaala yetu ya Shule za Msingi na Sekondari, tumekuwa tukipata changamoto ni kwa namna gani basi, tunaweza tukatumia lugha ya Kiswahili.

Lakini Serikali, inafanya kila jitihada kuangalia ni kwa namna gani huko baadaye tunaweza tukatumia lugha ya Kiswahili katika uandishi wa hukumu pamoja na kumbukumbu mbalimbali za mahakama. (*Makofî*)

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninayo maswali mawili madogo ya kuuliza. Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba tatizo ni mfumo wa kikoloni mbona Zanzibar ambao ni wenzetu katika Muungano katika Katiba yao ya mwaka 1984 kama ilivyorekebishwa mwaka 2010 wametaja waziwazi kwamba Kiswahili ndicho kitumike katika sheria. Kwanini huku Tanzania Bara bado tunasua sua?

Naibu Waziri amesema kuwa wako katika mchakato wa kutafsiri sheria zote kwa Kiswahili, hadi sasa wametafsiri sheria ngapi? Wanamkakati gani wa kutafsiri sheria zilizobaki?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kuhusiana na kwamba wenzetu wa upande wa Zanzibar wameingiza katika Katiba yao kwa mujibu wa mabadiliko waliyoyafanya mwaka 2010 kwamba hukumu zote zitakuwa zikitumia lugha ya Kiswahili. Hatuwezi tukajilinganisha lakini isipokuwa kwamba sisi ndiyo mfumo ambao tulikuwa tukiutumia lakini ni jambo jema unapoona wenzako wanafanya mambo mazuri basi na sisi kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tutaangalia pindi tutakapoingia kwenye mchakato wa Katiba na sisi huenda tukaliingiza humo basi ili Serikali iweze kuridhia na hukumu zetu ziwe katika lugha ya Kiswahili.

Lakini kuhusiana na swali la pili Mheshimiwa Kahigi ametaka kujua ni sheria ngapi mpaka hivi sasa ambayo zimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Sitaweza kutaja idadi lakini naweza kuahinisha baadhi ya sheria ambazo zimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili.

Kwanza ni sheria ya mtoto ya mwaka 2009, sheria ya watu wenye ulemavu, sheria ya watu waishio na virusi vya UKIMWI, sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai, sheria ya ubia baina ya Umma na watu binafsi, sheria itokanayo na fedha haramu pamoja na sheria zingine na tupo katika mchakato wa kuendelea na

tafsiri ya sheria zingine kwa kadri Bajeti itakavyoruhusu.
(Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge naona muda umeshapita na bado tuna swalı moja. Naomba mnikubalie tu twende kwenye swalı hili la mwisho tuendane na muda nisiache swalı la Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda. Naomba Mheshimiwa Christowaja nikupe muda uulize swalı lako.

Na. 117

Kuanzisha Miradi ya Maendeleo Vijijini ili Kuleta Ajira Kwa Vijana.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA aiuliza:-

Liko tatizo sugu la vijana kuhamza makazi yao vijijini na kukimbilia mijini kutafuta ajira na vibarua vyatua kuwapatia riziki na kuishia kufanya shughuli za umachinga na vibarua vyatua kufyatua matofali na ujenzi.

Pamoja na juhudzi za serikali za kukuza ajira kama vile kutoa mitaji na kujenga maeneo ya biashara, Serikali pia ingeweza kuanzisha miradi mbalimbali kama vile ujenzi wa zahanati, madarasa, maghala na barabara ambayo ingeweza kutoa ajira kwa vijana waliohitimu vyuo vyatua ufundi.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha miradi hiyo ya maendeleo vijijini yenye uwezo wa kutoa ajira nyingi kwa vijana kama njia mojawapo ya kupunguza tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, kama ifuatavyo.

Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuwepo kwa shughuli nyingi za kiuchumi vijijiini ikiwepo miradi aliyoitaja kutapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana sambamba na vijana kukimbilia mijini. Juhudi za Serikali kuendelea kutenga fedha nyingi kwenye Bajeti yake kwa ajili ya miradi ya maendeleo vijijiini kama kwenye miradi ya kilimo, mifugo, uvuvi, huduma za jamii, miundombinu na utunzaji wa mazingira huko vijijiini zitasaidia sana kupunguza tatizo hili la ajira la vijana kukimbilia mijini.

Jitihada za Serikali zimekuwa pia ni kushirikiana na wadau katika kutekeleza miradi mbalimbali vijijiini ikiwemo miradi inayofadhiliwa na mfuko wa maendeleo ya jamii yaani TASAF, miradi ya kilimo ngazi za wilaya *DADPs* na kadhalika miradi hii ina fursa kubwa kutoa ajira kwa vijana huko vijijiini. Aidha, Wizara ya Kazi na Ajira, imeanzisha utaratibu wa kuziwezesha Wizara na Taasisi za Umma kutambua fursa za ajira katika mipango na programu za maendeleo. Hatua hii itawezesha Serikali kutambua idadi na fursa za ajira zitokanazo na utekelezaji wa mipango yake ya maendeleo kila mwaka ikiwemo miradi iliyoko vijijiini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kushirikiana na Serikali na wananchi wa maeneo yao kuibua miradi mbalimbali itakayowezesha kutoa fursa za ajira kwa vijana waishio vijijini.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Naibu Waziri nina majibu mawili ya nyongeza. Kwa kuwa miradi mingi inayofadhilliwa na mfuko wa TASAF pamoja na mradi wa kilimo katika ngazi ya wilaya imekuwa haitekelezeki kutokana na kuchelewa kufika kwa fedha au mara nyingine fedha hizo kuliwa na watendaji wasio waaminifu kule vijijini, na hivyo kufanya miradi mingi kusimama.

Je, Serikali haioni kwamba matumizi mabaya ya fedha za miradi na ubadhifuru yanayofanywa na viongozi au watendaji wa vijijini ndiyo sababu kubwa inayowafanya vijana wa vijijini kukosa ajira na hivyo kukimbilia mijini?

Kwa kuwa ajira zinazofanywa na vijana mijini za kudhalilisha kwa mfano kuokota machupa ya maji barabarani au kwenye mabaa au wakati mwingine vijana kuwa wapiga debe kwenye vituo vyta mabasi na wakati mwingine watoto wa kike kuuza miili yao.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutoa semina vijijini kwa vijana hususan za ujasiriamali ili kuwafanya vijana hawa waweze kujiajiri wenyewe na kuacha mijini ambako wanakwenda kuathirika ahsante.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna ubadhirifu kwenye baadhi ya miradi inayotekelozwa huko vijiji ingawaje suala hili si kwamba ni kubwa kiasi cha kuathiri sana vijana kupata kazi. Lakini niseme vilevile kwamba kwa kweli katika miradi ambayo imetekelozwa vizuri bila ubadhirifu mkubwa ni miradi ya *TASAF* imekuwa ikisimamiwa vizuri sana. (*Makofi*)

Siwezi kuamini kwamba miradi hii kwa kweli imesimamiwa vibaya kiasi kwamba imesababisha vijana kukosa kazi. Hata hii miradi ya *DADPs* inawezekana kweli hela zikawa zimechelewa kwa maeneo fulani lakini kwa ujumla mimi naamini kabisa kwamba huku vijiji kama tukiboresha kilimo chetu na tukitumia kilimo cha Kisasa, kwa mfano kutumia vifaa vya kisasa kama matrekta na vijana wakakaa kwenye vikundi wakakubali kwamba kilimo vile vile ni ajira siyo lazima waende mjini wakawe machinga nadhani vijana wataweza kupata ajira huko vijiji.

Kuhusu hili suala la pili kwamba vijana wanaokotota makopo mjini nimesema kwamba kwanza kwenye ujasiriamali, kuna mambo mengi ambayo unaweza kufanya. Haya makopo wanayosema yanaokotwa kama ni machupa kama inafanyika kwa utaratibu mzuri wa kuri-cycle vitu hivi na ikafanywa kwenye vikundi inaweza kuwa njia nzuri tu ya kujipatia ajira. Lakini siyo labda ile makopo ambayo wanaokota lakini haiwezi kuwawezesha kwa kujialiri vizuri.

Lakini kwa ujumla mimi niseme tu kwamba ajira itapatikana vijijini lakini vilevile mijini kwa utaratibu ambao utakuwa mzuri vijana kukaa kwenye vikundi. Hili la semina Waheshimiwa Wabunge ndiyo maana nimesema sisi kama Wabunge vilevile tushirikiane kwenye Halmashauri zetu kutoa hizi semina ili vijana wetu huko vijijini waelewe kwamba wanaweza wakajiajiri hata vijijini bila kwenda mjini kwa sababu wakienda mjini wanakuta kwamba wanaathirika zaidi kuliko hata wangekaa vijijini wakafanya shughuli zao hasa za kilimo, uvuvi na vitu kama vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema tufanye kazi hii ya kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata ajira popote pale tulipo isiwe ni kazi ya Serikali peke yake sisi Wabunge tushiriki vilevile. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge muda umetutupa sana na kama mlivyoangalia kwenye *Order Paper* uwasilishaji leo wa hotuba hapa mezani utatuchukua muda mrefu kidogo kwa sababu wawasilishaji wako wengi kwa hiyo naomba mkubaliane na mimi dakika hizi tulizozitumia zimeshafidia dakika za uwasilishaji wa Hati Mezani.

Kabla hatujaendelea Waheshimiwa Wabunge ninayo matangazo hapa, tangazo la kwanza naomba niwatambue wageni ambao wako ndani ya ukumbi wa Bunge leo na nianze na kumtambua mgeni wa Mheshimiwa Spika. Huyu ni Kamanda Aiyenda, ni Kamanda wa Vijana kutoka Mkoa wa Mara, naomba Bwana Aiyenda, Kamanda wa Vijana kutoka mkoa

wa Mara, mgeni wa Spika usimame, karibu sana.
(Makofi)

Baada ya kutambua mgeni huyo wa Mheshimiwa Spika (naomba tu ukae mgeni wetu). Sasa naomba niwatambue wageni kutoka Ofisi ya Rais wanaongozwa na Ndugu George Yambesi, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, yuko Ndugu Habbi Mkwizu, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, yuko Peter Ilomo, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu, yuko Ndugu Suzan Mlawi, Naibu Katibu Mkuu Ikulu, yupo Dkt. Philipo Mpango, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, wako Manaibu Katibu watendaji watano kutoka Tume ya Mipango. Naomba wote wasimame kwa umoja wao. Wako makamishna, Wenyeviti, Makatibu na Wakuu wa taasisi zote zilizoko chini ya Ofisi ya Rais, naomba hawa wote nao wasimame kwa umoja wao. *(Makofi)*

Naomba nimtambue sasa Dkt. Edward Hosea, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (*PCCB*), ahsante sana. Naomba niwatambue wakuu wa Idara na Vitengo vyote kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Tume ya Mipango. Sasa wale wote waliobaki nao wasimame kwa umoja wao kwa kutambua uwepo wao.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa naomba nimtambue mgeni wa Waziri kivuli Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Prof. Mtoto wa Kalikoyela Kahigi, Mbunge ambaye ni Celina Kahigi na huyu ni mke wake

mpenzi na Prof. Kahigi. Mrs. Celina Kahigi naomba usimame. (*Makofi*)

Tunakushukuru sana tumefurahi kukufahamu na tunakushukuru kwa kazi yako nzuri ya kumtunza Profesa karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge baada ya kumtambua mke wa Profesa Kahigi na nadhani kwa kweli hata Mawaziri Vivuli wengine mngekuwa na utaratibu wa kuwaleta waume zenu na wake zenu, inapendeza sana. Vile vile hata Mawaziri, hata Mawaziri pia. (*Makofi/Kicheko*)

(*Hapa Wabunge walionyesha dalili ya kufurahi sana*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa niwatambue wageni wa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, ambao ni wasanii wa Muziki wa Kizazi Kipyä na tunaposema wasanii siyo kwa maana ile nyingine hawa ni wasanii wa muziki wa Kizazi Kipyä. Anslem Ngaiza Sog Dog, Bwana Sog Dog, naomba usimame kama upo ndani ya ukumbi, ooh! Hawa watu sijui watakuwa wapi, Ndugu Innocent Sahani Binobi na yeye pia hayumo ndani ya Ukumbi huu. Ndugu Joseph Lushashu, Bwana Misosi, haya majina haya kwa kweli Mheshimiwa Mbilinyi haya majina kiboko kweli weli. Kwa bahati mbaya naona hawajaingia bado katika ukumbi huu Bunge, lakini mahali popote walipo tunaomba kutambua uwepo wao na tunawakaribisha sana kwenye shughuli za Bunge. (*Makofi*)

Wageni waliofika Bunge kwa ajili ya mafunzo ni hawa wafuatao: Wanafunzi 40 na walimu wao kutoka shule ya Sekondari ya Mawezi, naomba wanafunzi wa Mawezi wasimame na walimu wao. Ahsantenni sana. Wanafunzi 60 na walimu wao kutoka shule ya msingi Bomani, Singida, karibuni sana tunawatakia kila la heri huko Singida. Wanafunzi 81 na walimu wao kutoka shule ya Sekondari Sangu ya Mbeya tunaomba wasimame wanafunzi wetu kutoka Sangu. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Tunao watumishi wanne wa Afya kutoka Wilaya ya Korogwe, wakiongozwa na Mganga Mkuu wa Wilaya ya Korogwe Dkt. Rashid Said, tunaomba Dkt. Rashid anyoshe mkono juu ahsante sana Dkt. Kwa kutuongozea msafara huo.

Tunao wanachuo 15 toka Chuo Kikuu cha *ST. John's* hapa Dodoma ambao wanatokea mkoa wa Singida ambao ni wageni wa Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mbunge wa Iramba Magharibi. Naomba na wao wasimame naona hawajaingia ukumbini. (*Makofi*)

Sasa naomba nitoe matangazo ya kazi, nimeombwa na Mheshimiwa Mwijage, Mwenyekiti wa Kamati ndogo ya Nishati na Madini, anaomba wajumbe hao wa Kamati Ndogo ya Nishati na Madini wakutane saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa B, Mwenyekiti Kamati ndogo Mheshimiwa Mwijage anaomba sana wajumbe wale wa Kamati ndogo mkutane katika ukumbi huo wa Msekwa B, saa saba mchana bila kukosa.

Sasa hapa ninayo matangazo ya club zetu za michezo Mheshimiwa Husein Mzee, Kocha Msaidizi, wa timu ya *Basketball* ya Bunge anaomba niwatangazie wale wote waliojiandikisha kujunga na timu yetu ya Bunge ya *Basketball* kwamba mazoezi yameshaanza katika uwanjwa wa *CBE*. Kwa hiyo, wote mnaombwa kufika kesho tarehe 3 Julai, 2012 saa kumi na mbili asubuhi ili kuendelea na mazoezi na nasikia timu hiyo imeanza kupamba moto sana. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, wachezaji wa *Basketball* muanze kuhudhuria mazoezi. (*Makof*)

Sasa nimeagizwa na Mheshimiwa Idd Azzan, Mwenyekiti wa *Bunge Sport Club*, na yeye anasema kuelekea maandalizi ya mapambano kati ya Wabunge wanachama hai wa Simba na Wabunge wanachama hai wa Yanga, pambano ambalo linatarajia kufanyika tarehe 7 sasa siku hiyo sijui itakuwaje. Wabunge kwa Wabunge.

Mheshimiwa Idd Azzan ananiomba niwaambie sasa ile Kamati tendaji ya *Bunge Sport Club* ikutane leo saa tano, hapana Mheshimiwa Idd Azzan vikao vyote ni saa saba sitaruhusu mkutano saa tano tuendelee na kazi za Bunge kwanza.

Kamati tendaji ikutane saa saba badala ya hii saa tano inayosemwa chumba namba 310, wajumbe hao ni Mheshimiwa Amos Makala, Naibu Waziri wa Wizara hiyo inayohusika na michezo, Habari, Vijana na Utamaduni na Mambo mengine. Wajumbe wengine

Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga na Mwanahamisi Kassim.

Sasa hao ndiyo hao Kamati tendaji inatakiwa ikutane huko kwa ajili ya shughuli hiyo. Sasa wameombwa pia Kamati ya Ufundu Mheshimiwa Prof. Majimarefu na Mheshimiwa Waziri Mkuu nao washiriki kikao hicho. (*Kicheko*)

Sasa kutakuwa na wakati mgumu sana kwa hivyo Kamati za ufundu sijui zitaroga timu gani na zote zinatoka Bungeni. Waheshimiwa Wabunge mimi naomba niwashukuru tumemaliza agenda hiyo kwanza naomba nimwite Katibu sasa atupeleke kwenye agenda ya pili. Katibu endelea na *Order Paper*. (*Makofi*)

KAULI ZA MAWAZIRI

KUENDELEA KUTUMIKA MIZANI YA RULA KATIKA ZAO LA PAMBA

MWENYEKITI: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge agenda inayofuata ni kupokea kauli za Mawaziri na kauli ya leo iliyoko mezani ni kauli inayotoka kwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Kwa niaba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y.
WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, nasimama kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara kutoa kauli hii.

Kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Bunge toleo la mwaka 2007 Kanuni Namba 49 naomba kutoa Kauli ya Serikali Kuhusu Suala la Kuendelea Kutumika kwa Mizani ya Rula yaani *Steel Yard* katika ununuzi wa zao la pamba sambamba na kuanza kutumika kwa mizani ya *digitali*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia tangazo lake namba 47 la mwaka 2012 yaani *Subsidiary Registration Supplement Number Five Volume 93* la tarehe 17 Februari, 2012 ilipiga marufuku matumizi ya mizani ya rula katika ununuzi wa zao la pamba. Hatua hii ilichukuliwa baada ya Serikali kuridhika na uhakiki uliofanywa kupitia wakala wa vipimo ambao ulibaini kuwa mizani ya aina hii ni rahisi kuchezewa na hivyo kuwapunja wakulima wanapolima pamba yao. Aidha, hatua hii ilikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya kusitisha matumizi ya mizani iliyotolewa katika kikao cha Bunge la Bajeti la mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza ahadi hiyo ya Serikali ya kusitisha matumizi ya mizani ya rula katika ununuzi wa zao la pamba, Serikali kupitia wakala wa vipimo imefanya uhakiki wa sampuli za mizani ya *digital* ambayo inafaa kwa ununuzi wa zao la pamba.

Baada ya uhakiki huo, wanunuzi wa Pamba kupitia Tanzania *Cotton Association (TCA)* na Tanzania *Cotton Growers Association (TACOGA)* waliruhusiwa kuagiza mizani za kutosha kutoka nje ya nchi kwa

niaba ya wanachama wake. Aidha Bodi ya Pamba nchini (*TCB*) iliweka sharti ya kwamba, mnunuzi wa pamba hataweza kupatiwa leseni ya kununulia pamba hadi aonyeshe na kuthibitisha kwamba ameagiza mizani hiyo kupitia *TCA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakadiriwa kuwa jumla ya mizani 8,000 zinahitajika kuwezesha upimaji wa zao wakati wa ununuzi, lakini hadi sasa *TCA* imeagiza mizani zisizozidi 5,500. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa upungufu wa mizani hizi utaathiri zoezi la ununuzi, na baadhi ya wanunuzi wanaweza kushindwa kuingia sokoni, hasa vyama Vikuu vya Ushirika ambavyo havina uwezo wa kuagiza mizani mbadala kwa bei kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli vyama Vikuu vya Ushirika vimeagiza sehemu ya mahitaji yake kupitia *TCA*, lakini kwa kuzingatia idadi ndogo ya mizani ilioagizwa na *TCA* dhidi ya mahitaji halisi, yakiwamo ya vyama vya Ushirika, vyama hivyo havitaweza kutoa huduma inayokidhi mahitaji kwa wanachama wake. Mpaka sasa hivi vyama vimeweza kulipia mizani 265 tu ukilinganisha na mahitaji ya mizani 1053, (*SHIRECU* – Shinyanga 698; *NCU* – Mwanza 220; *KACU* – Kahama 60; *BCU* – Biharamulo 60 na *ICU* Igembensabo, Nzega 15).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hii na kwa kuzingatia idadi ndogo ya mizani ilioagizwa kutoweza kutosheleza mahitaji; na kwa kuzingatia pia muda mfupi uliobakia wa ununuzi kuanza, ni wazi kuwa vyama vikuu vya Ushirika nilivyovitaja havina

uwezo mbadala wa kuwezesha kuagiza mizani ya ziada kwa sasa na hivyo vitaathirika katika biashara hii ya ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Juni, 2012, ni kiasi cha mizani 2,460 tu zimewasili nchini ukilinganisha na mahitaji halisi. Kutokana na msimu wa ununuzi kupangwa kufunguliwa ifikapo tarehe 2 Julai, 2012, Wizara ya Viwanda na Biashara na Kilimo, Chakula na Ushirika walikutana na Kamati Tendaji za *Tanzania Cotton Association* (*TCA*) pamoja na *Tanzania Cotton Growers Association* (*TACOGA*) mnamo tarehe 26 Juni, 2012 katika Ukumbi wa Wizara ya Kilimo Dodoma ili kutafuta ufumbuzi wa matumizi ya mizani katika ununuzi wa zao la Pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kupitia makubaliano na wadau katika kikao cha tarehe 26 Juni, 2012, Serikali imekubali kuruhusu matumizi ya mizani ya rula kutumika pamoja na mizani ya *digital* katika msimu wa 2012/2013. Makubaliano ya matumizi ya mizani hiyo ya rula yanaambatana na masharti kuwa Wakala wa Vipimo wataimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya mizani iliyokaguliwa na kuthibitishwa katika ngazi zote za ununuzi wa zao. Aidha, *TACOGA* na *TCA* wanatakiwa kuandaa na kutekeleza ratiba ya kuiondoa mizani ya rula kulingana na mizani ya *digital* iliyoingizwa nchini na ile inayotegemewa kuingia nchini katika kipindi kifupi kijacho. Hivyo mizani ya rula itakuwa inaendelea kuondolewa sokoni taratibu katika msimu huu wa 2012/2013. Kwa upande mwingine matumizi ya

mizani ya *digital* yatatoa fursa ya kutathmini ubora wa mizani hiyo kwa maana ndio kwanza itaaanza kutumika kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha matumizi ya mizani ya rula pamoja na ile ya *digital*, nimewaagiza Wakala wa Vipimo waanze mara moja ukaguzi wa mizani ya rula ili itumuke msimu huu sambamba na mizani ya digitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya msimu huu wa ununuzi wa pamba 2012/2013 kumalizika, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika zitaendelea kuzisimamia Mamlaka na Taasisi zote zinazohusika na upatikanaji, uhakiki na usambazaji wa mizani ya digitali ili kuhakikisha kuwa katika msimu ujao wa ununuzi wa pamba 2013/2014, matumizi ya mizani ya digitali yatafanyika kwa ukamilifu wake, tukizingatia matokeo ya tathmini niliyoitaja hapo juu. Hatua hii itasaidia kufikia lengo la matumizi ya mizani ya digitali na hivyo kudhibiti udanganyifu katika ununuzi wa Pamba na mazao mengine katika msimu ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya mizani ya rula yataruhusiwa kwa msimu huu wa 2012/2013 tu kwa kuwa sasa taratibu zote za kuzipata mizani za digitali zimekamilika na kilichobaki ni makubaliano na watengenezaji kutengeneza na kuingiza nchini kiasi cha mizani kinachohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatumia fursa hii kukumbusha na kusitiza kuwa, mnunuzi ye yeyote

atakayebainika kuwa amechezea mizani za kununulia mazao kwa lengo la kufanya udanganyifu katika ununuzi wa pamba na mazao mengine, atachukuliwa hatua kali za kisheria, ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
(*Makofi*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadiro ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 - Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) Pamoja na Ofisi ya Rais (Uhusiano na Uratibu)

MWENYEKITI: Sasa tuanze kupokea taarifa ya Makadirio hayo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Celina O. Kombani.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Ofisi ya Rais Uhusiano na Uratibu. Sasa tuanze kupokea taarifa ya Makadirio hayo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Celina O. Kombani. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33), Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67), Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), na Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 9), Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Kazi kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Pindi Hazara Chana (Mb) na Makamu wake Mheshimiwa John Paul Lwanji (Mb) kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri iliyotoa wakati wa kupitia Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/2013, hatua ambayo imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha Bungeni Hotuba hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani yake kwangu na kunipa dhamana ya kuiongoza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Ninaahidi kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kutekeleza

majukumu niliyopewa kwa kushirikiana na watumishi wenzangu na wadau wengine wote ndani na nje ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba pia, kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa umahiri wake katika kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu. Chini ya uongozi wake Serikali imetekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi alizotoa kwa wananchi wakati wa Uchaguzi Mkuu na kama zilivyoainishwa katika llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2010. Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yameweza kuhusu kuendelea kukua kwa uchumi wa nchi yetu na kuwawutia wawekezaji kuendelea kuwekeza nchini na Washirika wa Maendeleo kuona umuhimu wa kuendelea kuiunga mkono Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha mchakato wa mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba ambayo itaratibu na kukusanya maoni ya wananchi yatakayosaidia kuandikwa kwa Katiba mpya. Hatua hii inaonesha nia ya dhati katika kusimamia na kuimarisha utawala bora na demokrasia. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumjalia afya njema, busara na hekima katika uongozi wake ili nchi yetu iendelee kuwa ya amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Billal kwa uongozi wake bora. Nampongeza pia Waziri

Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb) kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali na utekelezaji wake. Aidha, Hotuba aliyoitao kwenye Bunge lako tukufu wakati akiwasilisha Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2012/2013 ni kielelezo cha ukomavu wake katika uongozi na imeonyesha mwelekeo na dira ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2012/2013. Nampongeza pia Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa (Mb) kwa Hotuba yake ambayo imeainisha misingi na mwelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Pia, nampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mhe. Stephen Masato Wasira (Mb) kwa Hotuba yake kuhusu hali ya Uchumi ya mwaka 2011/2012 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kuongoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima. Nampongeza pia Naibu Spika Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb) kwa kuendesha vyema shughuli za Bunge. Nawapongeza pia, Wenyeviti wa Bunge Mhe. Jenista Joackim Mhagama (Mb) na Mhe. Sylvester Massele Mabumba (Mb) kwa kuendesha vyema vikao vya Bunge. Aidha, nampongeza Mhe. Mussa Zungu Azzan (Mb) wa llala kwa kuchaguliwa bila kupingwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wabunge. Aidha, niwapongeze

Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kutuwakilisha kwenye Bunge la Afrika Mashariki. Ni matumaini yangu watatuwakilisha vyema kwa aslahi na manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mhe. Stephen Masato Wasira (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu; Mhe. Kapt. (Mst) George Huruma Mkuchika (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Mhe. Profesa Mark James Mwandosya (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Maalum kwa ushirikiano wao mkubwa katika kuandaa na kukamilisha hotuba hii. Aidha, nawashukuru Balozi Ombeni Yohana Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana George Daniel Yambesi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bwana Peter Alanambula Ilomo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu; Bwana HAB Mkwizu, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bibi Susan Paul Mlawi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu; Makamishna na Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais;

Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais na Taasisi zake ambao wamefanya kazi kubwa katika kuwezesha hotuba hii kukamilika.

Napenda pia kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wote katika Wizara, Mikoa na Idara mbalimbali za Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma kwa ushirikiano na michango yao iliyowezesha kuandaa hotuba hii. Nawashukuru pia wananchi wa Jimbo langu la Ulanga Mashariki kwa ushirikiano wao

wanaoendelea kunipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu katika nafasi niliyonayo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio tuliyopata. Hivyo, napenda kuchukua nafasi hii kuzishukuru nchi na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yafuatayo: Australia, China, Indonesia, Finland, Ethiopia, Mexico, Brazil, India, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Malaysia, Misri, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Uhlanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi, Marekani, Ireland, Jumuiya ya Madola, Jumuiya ya Ulaya, Israel, Benki ya Dunia, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japani (*Japanese Social Development Fund*), CIDA (Canada), DANIDA, DFID, JICA, NORAD, SIDA (Sweden), UNDP, UNIDO, UNFPA, USAID, GTZ na KOICA.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu itazungumzia maeneo matatu (3) ambayo ni: Mapitio ya Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2011/2012; Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2012/2013 na Maombi ya Fedha kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2011/2012 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA) na llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Kazi zilizotekelizwa na kila Taasisi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza (a) Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zake. Majukumu yake, katika mwaka 2011/2012, Ofisi ya Rais, Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilitengewa jumla ya Sh. 8,524,917,000 (Fungu 20) na Sh. 200,519,723,000 (Fungu 30) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 66,769,353,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Juni 30, 2012 kiasi cha Sh.8,159,632,041 (Fungu 20) na Sh.197,541,403,260 (Fungu 30) za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, jumla ya sh. 48,661,800,213 zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika mwaka 2011/2012, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

- (i) Huduma kwa Rais na familia yake zilitolewa;
- (ii) Huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo mbalimbali kama vile Uchumi, Siasa, Jamii, Sheria na Uhusiano wa Kimataifa zilitolewa;
- (iii) Rais aliwezeshwa kufanya mikutano na Viongozi wa Vyama vya Siasa na Wadau mbalimbali ambao walitoa maoni na ushauri uliosaidia kujenga muafaka wa Kitaifa kuhusu vipengele muhimu vya muswada wa Sheria Mpya ya Mabadiliko ya Katiba;
- (iv) Watumishi 47 waliwezeshwa kuhudhuria mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu kwa lengo la kujenga uwezo wa watumishi;

(v) Vikao 47 vya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri vilifanyika ambapo Nyaraka 103 zilichambuliwa, vikao 26 vya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (*IMTC*) vilifanyika na Nyaraka 76 kuchambuliwa. Vikao 18 vya Baraza la Mawaziri vilifanyika na Nyaraka 45 zilijadiliwa na kufanyiwa maamuzi;

Aidha, Mikutano ya Kazi ya Makatibu Wakuu ilifanyika na ajenda¹⁷ zilijadiliwa. Mikutano 6 ya Kamati ya Katiba, Sheria na Bunge ya Baraza la Mawaziri ilifanyika na Miswada 11 ilichambuliwa. Vile vile Mikutano 2 ya Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama ya Baraza la Mawaziri ilifanyika na Hati 2 zilijadiliwa;

(vi) Mafunzo ya utawala bora, uadilifu, uwajibikaji na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Pili yalitolewa kwa wajumbe 500 wa Kamati za Uadilifu kutoka Mamlaka ya Mapato (200) na Uhamiaji (300);

(vii) Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Awamu ya Pili (Desemba, 2006 – Desemba, 2011) wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa imefanyika na matokeo ya tathmini hiyo yatatolewa mwezi Agosti, 2012;

(viii) Mpango Kazi wa Uendeshaji Shughuli za Serikali kwa Uwazi (*Open Government Partnership (OGP)*) umeandaliwa. Mpango huu uliwasilishwa Makao Makuu Brasilia, Brazil mwezi Aprili, 2012;

(ix) Rufaa 60 za watumishi wa umma ilichambuliwa na kuwasilishwa kwa Rais Kwa uamuzi. Aidha,

malalamiko 170 ya watumishi wa umma na wananchi Wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo na Rais au Katibu Mkuu Kiongozi;

(x) Vikao vitatu (3) vya uratibu wa Programu za Mabadiliko katika Utumishi wa Umma vilivyoshirikisha Makatibu Wakuu, Waratibu wa Programu za Mabadiliko na Wabia wa Maendeleo vilifanyika. Vikao hivyo vilijadili maendeleo na changamoto zilizopo katika utekelezaji wake;

(xi) Mkakati wa kupambana na UKIMWI mahali pa kazi uliandaliwa;

(xii) Uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa kazi za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ulifanyika;

(xiii) Mikutano na viongozi wa dini mbalimbali iliyolenga kupata suluhisho la mgogoro wa uchaguzi wa Meya katika Manispaa ya Arusha ilifanyika na kurejesha amani;

(xiv) Mikutano saba (7) yenye la lengo la kujenga mahusiano mazuri baina ya Serikali na Taasisi za dini ilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha;

(xv) Majengo ya Ikulu, Ikulu ndogo ya Tabora na nyumba za wafanyakazi zilizopo Ikulu, zimefanyiwa ukarabati. Aidha, ukarabati wa Ikulu Ndogo ya Tanga unaendelea; na

(xvi) Maandalizi ya ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano (Multipurpose Hall) yamekamilika na kazi vyatya ujenzi itaanza mwezi Julai, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (*TAKUKURU*) kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007 Sura Namba 329, jukumu kubwa la *TAKUKURU* ni kuelimisha umma juu ya rushwa na athari zake katika jamii na mbinu za kupambana na rushwa nchini, kuchunguza tuhuma mbalimbali na kuwafikisha mbele ya vyombo vyatya sheria wale wanaojihusisha na vitendo vyatya rushwa. Aidha, *TAKUKURU* ina jukumu la kuishauri Serikali namna bora ya kuziba mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

Tuhuma 4,498 zilipokelewa hadi kufikia Mei, 2012. Kati ya tuhuma hizo, tuhuma 3,569 zilichunguzwa ambapo tuhuma 790 uchunguzi ulikamilika. Kati ya tuhuma ambazo uchunguzi umekamilika, majalada 10170 yalifikisha kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya kuomba kibali cha kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani. Kuanzia Julai, 2011 kesi 192 zilifunguliwa mahakamani zikiwemo kesi nne (4) zilizotokana na taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kesi tatu (3) zilizohusu Maliasili, na kesi 19 zilizohusiana na uchunguzi maalum wa Vocha za Pembejeo za Kilimo;

Majalada matano (5) yaliyohusu tuhuma za rushwa kubwa (*Grand Corruption*) yalifikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka Kati ya hayo majalada manne (4) yamepata kibali na watuhumiwa wamefikishwa mahakamani;

Kesi 612 ziliendeshwa mahakamani, kati ya hizo kesi 478 zinaendelea mahakamani na 134 zilitolewa uamuzi ambapo kesi 46 watuhumiwa walipatikana na hatia na kuadhibiwa, kesi 32 zilliondolewa mahakamani kutokana na sababu mbalimbali na kesi 56 watuhumiwa wake waliachiwa huru;

Kupitia vyanzo mbalimbali nya taarifa kiasi cha Sh.4,404,781,998 kiliokolewa kutokana na hatua mbalimbali pamoja na chunguzi zikiwemo Sh. 2,435,572,208 zilizorejeshwa Hazina na Wakurugenzi wa Halmashauri 3111 kati ya 87 zenyetuhuma. Uchunguzi unaendelea kubaini kama kulikuwepo na ukiukwaji wa taratibu katika matumizi ya fedha hizo ili kuchukua hatua zinazostahili dhidi ya wahusika;

Tafiti tatu (3) katika maeneo ya kuimarisha mifumo katika usimamizi wa ruzuku za pembejeo kwa utaratibu wa vocha, huduma zinazotolewa na hospitali za mikoa nchini na utoaji wa vibali nya kazi na ukaazi kwa wageni zimefanyika. Mapendekezo ya tafiti hizo yamewasilishwa katika sekta husika kwa utekelezaji;

Warsha sita (6) za wadau za kujadili matokeo ya utafiti na kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa zimefanyika katika sekta za afya, utoaji wa vibali nya kazi na ukaazi kwa wageni, kilimo (vocha za

pembejeo) na elimu. Aidha, matukio 137 ya udhibiti wa haraka (*quick-wins*) wa vitendo vya rushwa yamefanyika katika sekta za Ardhi, Afya, Maliasili na Utalii, Elimu, Mahakama, Polisi, Nishati na Madini, Ujenzi, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Kilimo;

Taarifa ya utafiti wa kina juu ya hali ya Utawala Bora na Rushwa (*National Governance and Corruption Survey*) ilitolewa rasmi kwa matumizi ya umma na kuwekwa kwenye tovuti ya Serikali. Mapendekezo ya 12 utafiti huo yameandaliwa mkakati wa kuzuia rushwa na kuboresha utawala bora katika Wizara na Idara za Serikali. Aidha, utekelezaji wa mkakati huo umeanza;

Elimu kuhusu rushwa na athari zake ilitolewa kuitia semina 2,114, mijadala ya wazi 126, midahalo 75, kazi mradi 462, ufunguzi wa klabu za wapinga rushwa 76, uimarishaji wa klabu 1,372, vipindi vya redio 143, vipindi vya televisheni 12, mikutano ya hadhara 612, maonesho 92, makala 114, matangazo 553 ya redio na mawili (2) ya televisheni, mikutano na waandishi wa habari 19, taarifa kwa vyombo vya habari 29, matamasha sita (6), shughuli za kijamii 17, matangazo ya kubandika 500, machapisho 87,805, kalenda za ukutani 135,000 na za mezani 5,000, shajara 2,500 na fulana 2,030;

Mafunzo ya kupambana, kudhibiti na kuzuia rushwa na miundombinu ya maadili yalitolewa kwa washiriki 241 toka Asasi za Dini, Vyombo vya Habari, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi na watumishi wa umma 501 toka Idara za Polisi, Mahakama, Uhamiaji, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ofisi ya

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Kurekebisha Sheria, Bunge na wajumbe wa bodi za zabuni katika Halmashauri ili kuwajengea uwezo wa 13 kupambana na rushwa. Aidha, kongamano la kitaifa la wadau wa kupambana na rushwa lilifanyika na kushirikisha wadau 238 toka maeneo mbalimbali;

Utafiti kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kupambana na Rushwa Duniani umefanyika. Matokeo ya utafiti huu yataisaidia Tanzania kufanya maboresho ili kutekeleza kikamilifu mkataba wa kimataifa wa kupambana na rushwa nchini kwa kuzingatia vigezo vyta kimataifa. Matokeo ya utafiti huo yapo katika hatua ya uchambuzi;

Ujenzi wa ofisi katika Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Misenyi umekamilika. Ujenzi wa ofisi katika Mikoa ya Ruvuma, Tabora na Wilaya za Newala na Kasulu umeanza na unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA) Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ulianza mwaka 2004 na ulipangwa kutekelezwa katika awamu nne (4) ambazo ni Tathmini ya Sekta Iсиyo Rasmi, Maandalizi ya Maboresho, Utekelezaji wa Maboresho na Ukuzaji wa Mtaji na Utawala Bora. 14 Jukumu kubwa la Mpango ni kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa biashara nchini. Katika mwaka 2011/2012, kazi zifuatazo zilitkelezwa:-

Kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara Muswada wa Kurekebisha Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 uliandaliwa na Sheria kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kikao chake cha mwezi Aprili, 2012. Muswada huu umefanya mabadiliko kadhaa yanayohusu uendeshaji biashara ikiwa na lengo la kuboresha mfumo wa uendeshaji biashara nchini;

Maofisa 60 katika ngazi za Wilaya, 39 ngazi ya kata na 110 ngazi ya vijiji kutoka Halmashauri za Wilaya za Kigoma, Mpanda, Singida, Mtwara na Ludewa, walijengewa uwezo. Aidha, urasimishaji wa ardhi vijijini katika vijiji viwili (2) kwa kila Halmashauri hizo umefanyika ambapo mashamba 11,014 yalipimwa na Hati za Kimila 7,632 zimetayarishwa. Urasimishaji wa ardhi vijijini unaendelea katika Halmashauri za Wilaya ya Kilombero, Kilosa na Bunda;

Upimaji wa mashamba ya chai 417 na utoaji wa hati kwa wamiliki wake umefanyika 15 kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Njombe, Bodi ya Chai na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai. Aidha, wamiliki wa mashamba yallyopimwa wamejengewa uwezo ili kuwawezesha kutumia hati zao kupata fursa za kiuchumi zilizoko katika soko ikiwemo mikopo kutoka katika vyombo vyatofauti. Vile vile, kazi ya urasimishaji wa mashamba ya chai unaendelea katika Halmashauri za Wilaya za Mufindi na Njombe;

Zoezi la kujenga uwezo na urasimishaji ardhi vijijini katika Wilaya za Kaskazini 'A', Unguja na Mkoani, Pemba linaendelea;

Ujenzi wa masijala nane (8) za ardhi vijijini katika viji vinane (8) kwenye Halmashauri tatu (3) umekamilika. Vijiji hivi ni Sanjaranda, Gurungu na Kitopeni katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni; Munguwi na Pwaga katika Halmashauri ya Mpwapwa; pamoja na Nakalonji, Nahimba na Mbondo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea;

Shughuli za urasimishaji wa rasilimali ardhi mijini katika mamlaka za Miji ya Arusha, Morogoro na Njombe ziliratibiwa. Upimaji unaendelea katika Mji wa Tunduma Mkoani Mbeya na Mtaa wa Baruti Kata ya Kimara Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam ambapo jumla ya viwanja 1,078 vimepimwa eneo la 16 Mji wa Tunduma na viwanja 1,050 vimepimwa katika Mtaa wa Baruti Dar es Salaam;

Urasimishaji wa biashara katika Manispaa ya Mji wa Zanzibar, Unguja na Chake Chake, Pemba umekamilika ambapo jumla yawafanyabiashara 947 wamepatiwa mafunzo juu ya namna ya kufanya biashara kwa kuzingatia matakwa ya Sheria. Aidha, urasimishaji biashara katika Wilaya za Magharibi, Unguja na Wete Pemba unaendelea;

Uratibu wa uanzishwaji wa Mfuko wa Urasimishaji Ardhi wa Wilaya (District Formalization Revolving Fund) unaendelea ambapo Mshauri Mwelekezi ameanza kazi ya kuandaa mfumo wa uanzishwaji wa Mfuko wa

urasimishaji. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwaka 2012/2013;

Taratibu za kurahisisha mifumo ya kodi na uandikaji wa vitabu vya mahesabu kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati umekamilika; na

Mkakati wa Mawasiliano wenyewe lengo la kutoa elimu ya urasimishaji na fursa zinazopatikana katika kushiriki shughuli za uchumi rasmi unaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ulianza utekelezaji wa Awamu ya Pili mwaka 2005 na inatarajiwa kukamilika Juni, 2013. Kutokana na kukamilika kwa awamu hii, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imetayarisha Awamu ya Tatu ya TASAF ambayo utekelezaji wake unaanza mwezi Julai, 2012 na itatekelezwa katika kipindi cha miaka 10. Kama ilivyokuwa kwa Awamu ya Kwanza na ya Pili, jukumu kubwa la TASAF ni kushirikisha vikundi vya jamii, kuainisha, kuchambua mahitaji na kukusanya rasilimali na maendeleo endelevu katika ngazi ya Vijiji, Shehia na Wilaya. Kazi zilizotekerezwa katika mwaka 2011/2012 ni kama ifuatavyo:-

(i) Miradi mipyä 980 yenyé thamani ya Sh.19,250,464,490 iliibuliwa na wananchi na kupatiwa fedha toka TASAF kwa ajili ya utekelezaji wake. Aidha, Sh. 9,825,600,990 zilitolewa kwa ajili ya kukamilisha miradi 813 ambayo ilikuwa hajakamilika kabla ya Juni, 2011 ili itoe huduma zilizokusudiwa kikamilifu;

(ii) Mafunzo ya kujenga uwezo yametolewa kwa vikundi 1,778 vyenye wanachama 22,712 kutoka katika Halmashauri 44 ili kuimarisha shughuli za kuweka na kuwekeza katika Mpango wa Kuweka Akiba na Kuwekeza 18 (*Community Savings Investment and Promotion (COMSIP)*);

(iii) Mafunzo ya kujenga uwezo katika fani za Utunzaji wa kumbukumbu za mapato na matumizi pamoja na utayarishaji wa mipango ya biashara na ujasiriamali yametolewa kwa wadau 241,167 ambao ni:- Wataalamu 6,135 wa sekta zinazohusika katika ngazi ya Halmashauri, wajumbe 103,649 wa Halmashauri za Vijiji/Mitaa/Shehia na wajumbe 131,383 wa Kamati za Miradi;

(iv) Utekelezaji wa Mpango wa majaribio wa Uhawilishaji Fedha kwa Kaya Maskini uliendelea katika Halmashauri tatu za Kibaha, Bagamoyo na Chamwino. Kaya zilizonufaika na Mpango huu zimefikia 4,985. Walengwa waliopo kwenye Mpango huu ni 13,081 kutoka katika Halmashauri hizo tatu (3) na kiasi kilichotolewa kwa walengwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 ni Sh.412,070,100;

(v) Vipindi vinne (4) vya redio na vinne (4) vya televisheni viliendelea kutolewa kila mwezi. Maeneo yaliyoonekana kutoeleweka vizuri yalifafanuliwa na wataalamu na wananchi kupewa fursa ya kuuliza maswali ya moja kwa moja. Pia, TASAF ilishiriki katika maonesho na matukio ya kitaifa kama; Siku ya Utumishi wa Umma, NaneNane, Siku ya 19 UKIMWI, SabaSaba

n.k. Maonesho hayo yalitumika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu fursa mbalimbali zilizopo kupitia *TASAF*;

(vi) Mifumo ya utoaji wa taarifa za miradi uliendelea kuboreshwa. Taarifa zote kuhusu miradi zimehifadhiwa katika mfumo wa kompyuta na hivyo kurahisisha utoaji wa taarifa kwa wadau mbalimbali;

(vii) Tathmini mbalimbali zimefanyika ili kupima manufaa yanayotokana na Miradi ya Jamii na namna nzuri ya kuboresha huduma zinazotolewa. Tathmini hizi zimeonyesha kupatikana kwa manufaa makubwa kwa walengwa wa makundi mbalimbali; na

(viii) Katika kukuza uwazi na uwajibikaji kwa wadau, taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka kwa Halmashauri za Unguja na Pemba ziliendelea kutolewa kwenye Magazeti.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*PTF*)majukumu ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea ni pamoja na kutoa huduma za mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na kutoa huduma za ushauri na mafunzo ya kibiashara ili kuongeza ufanisi katika biashara. Baadhi ya kazi zilizotekelawa katika mwaka 2011/2012 ni kama ifuatavyo:-

(i) Mfumo mpya wa kutunza kumbukumbu uitwao *CRDB Finance Solution* ulinunuliwa na umeanza kutumika. Lengo la Mfumo huu ni kutunza kumbukumbu za kila mteja wa Mfuko na kurahisisha rejea na upatikanaji wa taarifa mbalimbali za wateja;

(ii) Ushauri kuhusu mikopo na urejeshwaji wake ulitolewa kwa walengwa wa Mfuko; na

(iii) Mafunzo kwa Wajasiriamali 226 wa Matawi ya Kilombero, Chalinze na Turiani yalitolewa. Aidha, mafunzo ya uendeshaji kwa watendaji 28 wa Mfuko yalifanyika.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uongozi Taasisi ya Uongozi ilianzishwa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 274 la mwaka 2010 kwa lengo la kuwa Kituo cha Utaalam wa Hali ya Juu (*centre of excellency*) cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Lengo kuu ni kuimarisha uwezo wa Viongozi kwa nia ya kuleta maendeleo endelevu. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza (emerging leaders), wakiwemo wanasiwa, watumishi wa Serikali na Mahakama, ndani na nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, kazi zifuatazo zimetekelizwa:-

(i) Mifumo ya utawala na fedha kwa ajili ya matumizi ya ofisi imewekwa;

(ii) Mpango Mkakati wa Taasisi wa mwaka 2011/2012-2015/2016 uliandaliwa. Mpango huu unatoa mwongozo katika utekelezaji wa Dira ya Taasisi katika kipindi cha miaka mitano (5) ijayo;

(iii) Programu tatu (3) za mafunzo zilibuniwa na kutayarishwa, programu hizo ni Mkakati wa Uongozi kwa ajili ya maendeleo endelevu, Menejimenti inayozingatia matokeo na kutafakari matokeo ya uongozi na kuchukua hatua;

(iv) Vipindi sita (6) vya mahojiano na Wakuu wa Nchi Wastaifu na wataalamu mbalimbali kuhusu uongozi na maendeleo endelevu yalifanyika na kurushwa kwenye televisheni vilifanyika;

(v) Majadiliano ya kujenga uelewa wa viongozi katika masuala ya usimamiaji wa maliasili na uchaguzi barani Afrika yalifanyika;

(vi) Tafiti mbili (2) zinaendelea kufanyika zikiwa ni, Tathmini ya ubia kati ya taasisi za umma, taasisi binafsi na asasi za kiraia na mapitio ya hali ya utawala bora katika taasisi za umma;

(vii) Jukwaa la uchumi unaokua bila kuathiri mazingira (uchumi wa kijani) lilizinduliwa mjini Iringa likiwa na lengo la kuongeza uelewa kwa wataalam watunga sera, watoa maamuzi na watu wenye ushawishi katika jamii kuhusu masuala yanayohusu uchumi wa kijani;

(viii) Mpango Kabambe wa Matumizi ya Ardhi kwa ajili ya Ujenzi wa Makazi ya Kudumu ya Taasisi umeandaliwa na kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi;

(ix) Programu za kuimarisha uwezo wa viongozi zimeanza kutolewa ikiwa ni pamoja na kuwezesha

Semina Elekezi kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, na Makatibu Tawala wa Mikoa. Aidha, Mafunzo ya mawasiliano wakati wa dharura yaliyotolewa kwa Maafisa Mawasiliano kutoka Wizara 25;

(x) Tovuti ya Taasisi ya Uongozi (www.uongozi.or.tz) imekamilika na itaanza kutumika Julai 2012; na

(xi) Kituo cha taarifa cha Taasisi ya Uongozi kimeanzishwa Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake. katika mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali iliidhinisha jumla ya Sh.33,361,247,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2011/2012 kwa Fungu 32. Kati ya fedha hizi Sh.16,022,977,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.17,338,270,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maedeleo. Hadi kufikia Juni, 2012 kiasi cha Sh.16,022,977,000 za Matumizi ya Kawaida zimepokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, jumla ya Sh.15,743,026,000 zimepokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, pamoja na Taasisi zake imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa na

watumishi wa umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi wanapotoa huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelawa katika mwaka wa fedha 2011/2012 ni kama ifuatavyo:-

(i) Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Vibali vya ajira mpya 48,333 kati ya 64,024 vimetolewa. Hadi kufikia Juni, 2012 watumishi wapya 38,289 wameajiriwa (Wizara na Idara za Serikali Zinazojitegemea 4,006, Sekretarieti za Mikoa 368, Halmashauri za Serikali za Mitaa 30,583, Wakala na Taasisi za Umma 3,332). Kutofikiwa kwa Ikama iliyoidhinishwa 2011/2012 kulitokana na baadhi ya watumishi hasa wataalam wa Kada za Afya, Kilimo na Mifugo kuacha kwenda katika vituo walivyopangia, ukosefu wa wataalamu kwenye soko la ajira, na uamuzi wa Serikali kupunguza ajira katika mwaka wa fedha 2011/2012;

(ii) Watumishi 59,827 wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Wakala za Serikali na Taasisi za Umma walipandishwa vyeo na waajiri mbalimbali;

(iii) Tathmini ya Utekelezaji wa Miundo ya Kiutumishi imefanyika kwa lengo la kuona kama miundo hii inawezesha watumishi kuendelea kukua kitaalamu. Matokeo ya tathmini hii yameainisha kuwa miundo hii inahitaji kuhuishwa ili iendane na mabadiliko mbalimbali yanayoendelea katika Utumishi wa Umma kama ilivyoainishwa katika marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Sura Namba 298;

(iv) Madai ya malimbikizo ya mishahara ya Watumishi wa Umma 54,010 yenyе thamani ya Sh. 72,351,994,390.92 yamelipwa;

(v) Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Udhibiti wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara ya Watumishi wa Umma umeendelea kuimarishwa kwa kuhuisha Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (*Human Capital Management Information System – HCMIS*). Mfumo huu umesambazwa katika Taasisi 340 za Serikali ili kuimarisha uwajibikaji na uadilifu katika matumizi ya rasilimaliwatu na rasilimalifedha;

(vi) Mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara ya Watumishi wa Umma yametolewa kwa Maafisa Rasilimaliwatu na Utumishi 688 kutoka Taasisi 348 za Serikali. Mafunzo haya yataendelea kutolewa kwa taasisi 15 zilizobaki;

(vii) Taarifa za Watumishi wa Umma 346,205 kati ya 433,819 sawa na asilimia 80 ya watumishi zimehakikiwa na 26 kuingizwa katika Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara. Taarifa zilizobaki zinaendelea kuhakikiwa; na

(viii) Viongozi Wastaafu wa Kitaifa 13 wameendelea kuhudumiwa kwa mujibu wa Sheria. Aidha, upembuzi yakinifu na uchambuzi wa athari za mazingira kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kuwaenzi Waasisi wa Taifa (Mwl. Julius K. Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume) umefanyika.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma Sura namba 105, Serikali ilitekeleza yafuatayo:-

- (i) Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma lilifanya mikutano minne (4) na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu maslahi ya Watumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2012/2013;
- (ii) Mabaraza ya Majadiliano ya Pamoja ya Kisekta yaliyomaliza muda wake yameundwa upya na yanatarajiwa kuzinduliwa na kuanza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2012/2013;
- (iii) Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma limekutana mara moja kwa mujibu wa Sheria pamoja na mambo mengine limechambua na kupendekeza vigezo vitakavyosaidia kuainisha maeneo yenye mazingira magumu katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kutoa motisha kwa watumishi wa maeneo hayo; na
- (iv) Mabaraza ya Wafanyakazi mahali pa kazi yamekutana kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali kuhusu ufanisi wa kazi, haki na wajibu wa watumishi na kupitisha mipango na bajeti za maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizoteklezwa ni pamoja na:-

(i) Usimamizi wa uanzishwaji wa Wakala wa Serikali Mtandao na kukibadilisha Kituo cha Mafunzo kwa Njia ya Mtandao kuwa Wakala ulifanyika;

(ii) Kusimamia jukumu la kujenga uwezo wa kiutendaji kwa watumishi wa umma kwa kushirikiana na nchi za nje pamoja na mashirika mbalimbali ya kimataifa ambapo watumishi wa umma 426 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika nyanja mbalimbali;

(iii) Tathmini juu ya hali halisi ya Uhimilifu wa Mfumo wa Utunzaji na Kumbukumbu imefanyika katika Wizara 11 na Mikoa 18 kwa lengo la kubaini mafanikio na changamoto zilizopo ili tuweze kuanda mikakati ya kutatua changamoto zilizobainishwa;

(iv) Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha kutunza kumbukumbu Tuli kilichopo Dodoma umekamilika;

(v) Utunzaji wa kumbukumbu katika masijala za Wizara 11 na kumbukumbu za watumishi katika Ofisi 18 za Wakuu wa Mikoa umeboreshwa;

(vi) Mikutano kazi kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za utunzaji na udhibiti wa taarifa za Serikali katika Wizara 13, Idara Zinazojitegemea mbili (2), na Wakala wa Serikali mbili (2) imefanyika;

(vii) Upembuzi yakinifu kwa ajili ya kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma zisizo za msingi (non core functions) Serikalini kwenye Wizara za: Uchukuzi; Ujenzi; Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Fedha

na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma ulifanyika;

(viii) Ufuatiliaji wa Mifumo ya Utendaji Kazi katika Wizara na Idara Zinazojitegemea tano (5) ambazo ni Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Habari, Vijana na Michezo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ujenzi na Sekretarieti ya Ajira umefanyika;

(ix) Mwongozo wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji kazi umeandaliwa;

(x) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara 26 na Idara Zinazojitegemea sita (6) umefanyika;

(xi) Upembuzi yakinifu wa kuunganisha Taasisi za Serikali zilizopo Dar es Salaam kwenye Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali umefanyika;

(xii) Timu ya Kitaifa ya Wataalamu 24 wa Sera kutoka katika wizara mbalimbali imeundwa na kujengewa uwezo wa kuchambua, kutunga, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa sera;

(xiii) Mafunzo ya Maadili ya Utumishi wa Umma kwa watumishi 663 kutoka katika Wizara na Idara Zinazojitegemea nane (8) ambazo ni Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Ujenzi; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Ofisi ya Rais - Sekretarieti ya Ajira; Wizara ya Kazi na Ajira na Mamlaka ya Chakula na

Dawa yametolewa. Pia, mafunzo ya maadili yalitolewa kwa watumishi 1,490 wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 12 katika Mikoa ya Dodoma na Manyara;

(xiv) Utafiti wa majaribio kuhusu hali ya Maadili katika Utumishi wa Umma katika Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi iliyohusisha watumishi 343 na wateja 301 umefanyika. Taarifa ya utafiti huu imetumika kutengeneza mkakati wa kukuza maadili ya utumishi wa umma kwa kutumia mbinu za kimasoko ambao utaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2012/2013;

(xv) Ufuatillaji wa utaratibu wa kushughulikia malalamiko ya wananchi katika Taasisi 10 kwa lengo la kuhimiza utekelezaji umefanyika. Taasisi hizo ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Ujenzi; Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Wizara ya Kazi na Ajira; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Ofisi ya Waziri Mkuu na *BRELA*.

Pia utaratibu wa kushughulikia malalamiko ya wananchi umeanzishwa kwenye Taasisi tano (5) ambazo ni Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; Wizara ya Kilimo na Chakula; Wizara ya Maji na Wizara ya Viwanda na Biashara;

(xvi) Wizara nane (8) – (Afya na Ustawi wa Jamii; Elimu na Mafunzo ya Ufund; Viwanda na Biashara; Kilimo, Chakula na Ushirika; Ardhi, Nyumba na

Maendeleo ya Makazi; Maji; Ujenzi na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma) zimewezeshwa kuandaa na kuhuisha mipango ya rasilimaliwanu ili ziweze kufikia malengo kwa kutumia vizuri rasilimali walizonazo;

(xvii) Mwongozo wa kutayarisha Mpango wa Kurithishana Madaraka katika Utumishi wa Umma kwa Wizara zote; Idara Zinazojitegemea; Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa umeandaliwa na kusambazwa kwa ajili ya utekelezaji;

(xviii) Wizara nane (8) na Taasisi ya Umma moja zimewezeshwa kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo na kuandaa Mipango ya Mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa ajili ya watumishi wake. Wizara na Taasisi hizo ni: Afya na Ustawi wa Jamii; Elimu na Mafunzo ya Ufundji; Kilimo, Chakula na Ushirika; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Ujenzi; Maji na Umwagiliaji; Viwanda, Biashara na Masoko; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; na Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi;

(xix) Watumishi wa Umma 30 (wanawake 28 na wanaume wenyewe ulemavu wawili [2]) walipatiwa ufadhili wa masomo ya shahada ya uzamili katika vyuo vya elimu ya juu hapa nchini;

(xx) Tathmini ya Programu ya Shahada ya Uzamili kwa watumishi wanawake na wenyewe ulemavu waliofadhliliwa na Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kubaini mafanikio ya malengo yaliyokusudiwa imefanyika;

(xxi) Ukaguzi wa masuala ya Anuai za Jamii katika Wizara tano (5) ambazo ni: Elimu na Mafunzo ya Ufundis; Afya na Ustawi wa Jamii; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mambo ya Ndani ya Nchi na Kilimo, Chakula na Ushirika umefanyika;

(xxii) Viongozi na Watumishi Waandamizi 104 wamehudhuria mafunzo ya uongozi ili waweze kukabiliana na changamoto na mabadiliko katika utaratibu wa utendaji kazi Serikalini na kuhimiza utendaji unaojali matokeo;

(xxiii) Makatibu Wakuu wawili (2), Naibu Makatibu Wakuu 11, Makatibu wa Tume/Bodi watatu (3) walipatiwa mafunzo elekezi baada ya uteuzi ili waweze kuelewa na kutekeleza majukumu ya Serikali na wajibu wao kama viongozi wa Serikali;

(xxiv) Viongozi Waandamizi 12 wa Serikali wamehudhuria makongamano na mikutano ya kimataifa yenye lengo la kubadilishana mawazo, ujuzi na uzoefu katika maeneo ya utawala na uongozi ili kutafutia ufumbuzi changamoto zinazojitokeza katika eneo la utawala na uongozi;

(xxv) Tathmini ya Utendaji Kazi wa Wakala 26 za Serikali imefanyika;

(xxvi) Kitengo cha Uratibu wa Programu za Mabadiliko katika Utumishi wa Umma kimewezeshwa kutekeleza majukumu yake ya uratibu wa Programu nane (8) za Mabadiliko katika Sekta za: Utumishi wa Umma; Sheria; Serikali za Mitaa; Usimamizi katika Fedha

za Umma; Mazingira ya Biashara na Uwekezaji; Mkakati wa Kupambana na Rushwa; Kuendeleza Sekta ya Fedha na Mkakati wa Kukuza Kilimo; na

(xxvii) Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imewezeshwa kiutaalam na kifedha kutekeleza shughuli za Programu ya Mabadiliko katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma (PTSC) katika mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo cha Utumishi wa Umma kilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Tawi jipya la Chuo cha Utumishi wa Umma Mkoani Singida lilianzishwa;

(ii) Ukarabati wa madarasa mawili (2) katika Tawi la Tabora na vyumba viwili (2) vya maktaba na kompyuta Tawi la Mtwara ulifanyika;

(iii) Watumishi 179 wa Chuo walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi;

(iv) Kozi 89 za muda mfupi na mrefu katika fani mbalimbali kwa watumishi wa umma na sekta binafsi 9,299 ziliandaliwa na kutolewa; na

(v) Shauri za kitaalamu sita (6) ambazo ni kuhuisha miundo ya utumishi, huduma kwa mteja, tathmini ya kazi, mpango mkakati, uchambuzi wa mahitaji ya mafunzo na kuandaa mpango wa mafunzo zilifanyika.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mafunzo kwa Njia ya Mtandao katika mwaka wa fedha 2011/2012, Kituo cha Mafunzo kwa Njia ya Mtandao kilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Mafunzo ya Mfumo wa Mawasiliano ya Kielektroniki ofisini kwa watumishi 250 wa Serikali yalitolewa;

(ii) Ushirikiano na Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi katika kutoa mafunzo umeimarishwa. Taasisi hizi ni pamoja na "*Ethiopia Civil Service College*", "*Kenya Institute of Administration*", *African Capacity Building Foundation (ACBF)*, *Association of African Distance Learning Centres (AADLC)*, na Chuo cha Benki ya Dunia; na

(iii) Mafunzo katika nyanja mbalimbali kwa washiriki 1,661 yametolewa. Kati ya hao washiriki 320 ni washiriki binafsi na mashirika yasiyo ya Kiserikali na 1,339 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura ya 398, ili kuhakikisha kwamba mienendo na tabia za Viongozi wa Umma walijotajwa katika Kifungu cha 4(1) cha Sheria hiyo inazingatia misingi ya maadili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali iliidhinisha jumla ya Sh.2,597,991,172 kwa Fungu 33 ikiwa ni Matumizi ya Kawaida na Sh. 910,000,000 zikiwa ni za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Juni, 2012 kiasi cha Sh.2,594,853,802 zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kazi zilizotekelawa ni kama ifuatavyo:-

(i) Viongozi wa Umma 8,972 wa kada mbalimbali walitumiwa Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba, 2011. Hadi kufikia Juni 2012 jumla ya Viongozi wa Umma 8,290 sawa na asilimia 93 walirejesha Fomu za Tamko. Hatua zilizochukuliwa dhidi ya viongozi ambao hawajarejesha matamko yao ni pamoja na kuandikiwa barua za kuwataka kutoa maelezo;

(ii) Uhakiki wa Rasilimali na Madeni ya Viongozi wa Umma 133 umefanyika. Miiongoni mwa Viongozi wa Umma waliohakikiwa Rasilimali na Madeni yao ni pamoja na Wabunge, Watendaji Wakuu wa Serikali na Mashirika ya Umma, Makamishna waTume,Wakurugenzi katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Madiwani, Majaji na Mahakimu katika ngazi mbalimbali;

(iii) Malalamiko 215 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yamepokelewa, kuchambuliwa na kufanyiwa uchunguzi wa awali ili kubaini ukweli kuhusu malalamiko hayo. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 125 yanahusu ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili na malalamiko 90 hayahu ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa Sheria

hiyo. Malalamiko yasiyohusu ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili yamewasilishwa kwenye Vyombo husika kwa hatua zaidi;

(iv) Viongozi 432 kutoka Taasisi 13 za Umma na Viongozi wapya 223 walioteuliwa katika kipindi cha mwaka 2011/12 wakiwemo Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya walielimishwa kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, kwa kuitia maonesho ya NaneNane na Wiki ya Utumishi wa Umma, wananchi 2,000 walipata fursa ya kutembelea mabanda na kuelimishwa kuhusu majukumu ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(v) Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura Namba 398 yapo katika hatua ya kukusanya maoni kutoka kwa Wadau, ili yapelekwe Serikalini kwa maamuzi;

(vi) Taasisi saba (7) zikiwemo Asasi za Kiraia, Asasi za Kidini, Vyama vya Kitaaluma na Taasisi za Serikali zimejengewa uwezo katika kukuza uadilifu, uwazi na uwajibikaji kwa kupewa ruzuku na vifaa;

(vii) Watumishi sita (6) wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi 60 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi; na

(viii) Kiwanja kwa ajili ya kujenga Ofisi ya Kanda ya Mashariki ambayo itahudumia mikoa ya Tanga, Pwani na Morogoro kimepatikana Chalinze wilayani Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali iliidhinisha jumla ya Sh. 2,939,650,000 kwa Fungu 67 ikiwa ni Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Juni, 2012 kiasi cha Sh. 1,807,385,544 zimepokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Usaili kwa nafasi wazi za kazi 762 katika utumishi wa umma umefanyika kwa mchanganuo ufuatao: Wizara na Idara Zinazojitegemea nafasi 38; Sekretarieti za Mikoa nafasi saba (7); Mamlaka za Serikali za Mitaa nafasi 148; Wakala wa Serikali nafasi 208 na Taasisi za Umma nafasi 361;

(ii) Usaili kwa nafasi 3,397 unaendelea kwa mchanganuo ufuatao: Wizara na Idara zinazojitegemea nafasi 502; Sekretarieti za Mikoa nafasi 80; Mamlaka ya Serikali za Mitaa nafasi 2,558; Wakala wa Serikali nafasi 26 na Taasisi za Umma nafasi 201. Usaili huu ni nje ya kada za Elimu, Afya, Kilimo na Mifugo ambao unaendeshwa na Wizara mama;

(iii) Waajiriwa wapya 496 waliofanyiwa usaili waliokuwepo kwenye kanzidata (database) walipangwi vituo vya kazi kwa waajiri 52;

(iv) Waajiri katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar walitembelewa kwa lengo la kuwapa uelewa wa majukumu ya Sekretarieti;

(v) Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016) ulihuishwa;

(vi) Kanzidata ya waombaji kazi wenye ujuzi unaotakiwa na waajiri 529 iliboreshwana Orodha ya Wahitimu 21,691 wa kuanzia mwaka 2008 – 2011 kutoka Vyuo Vikuu 11 ilipokelewa;

(vii) Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira (www.ajira.go.tz) ilianzishwa na kuzinduliwa kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano na wadau mbalimbali; na

(viii) Watumishi wapya 25 wa Sekretarieti ya Ajira walijiriwa, watano (5) waliteuliwa na wanane (8) walithibitishwa kazini.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Tume iliidhinishiwa kutumia kiasi cha Sh. 8,779,887,000 ambapo hadi kufikia Juni 2012 kiasi cha Sh. 7,570,699,015 kilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika katika mwaka 2011/2012 ni kama ifuatavyo:-

(i) Vikao vya kisheria vinne (4) vilivyotoa uamuzi wa Rufaa 103 na malalamiko 11 vilifanyika;

(ii) Uguzi maalum kwa Taasisi za Umma 28 ulifanyika ili kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika usimamizi wa Rasilimaliwatu;

(iii) Mafunzo ya ukaguzi wa Utendaji Kazi Binafsi kwa watumishi wa umma 50 yalifanyika;

(iv) Makala sita (6), vipindi 12 vya redio na ziara za kuelimisha wadau kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia uendeshaji na usimamizi wa rasilimaliwatu katika Mikoa minane (8) ziliandaliwa;

(v) Mafunzo ya Maadili kuhusu Maadili na jinsi ya kujikinga na maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI yalitolewa kwa watumishi 70 wa Tume;

(vi) Walimu 8,506 walisajiliwa; 11,436 walithibitishwa kazini; 24,013 walipandishwa vyeo; 8,594 walibadilishwa kazi; 117 walishughulikiwa masuala ya nidhamu; 135 walipatiwa vibali vya maombi ya kustaafu kazi na 695 waliandaliwa kumbukumbu za mafao ya hitimisho la kazi;

(vii) Utafiti kuhusu sababu za utoro kwa walimu wapya wanaopangiwa vituo vya kazi ulifanyika; na

(viii) Mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 86 wa Tume ya Utumishi wa Umma yalifanyika.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Bajeti kwa mwaka 2012/2013. Msingi wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2012/2013 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Miaka Mitano ya Maendeleo (2011/2012-2015/2016), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) na llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010/2015. Kazi zitakazoteklezwa na kila Taasisi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zake ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2012/2013, Fungu 20 Ofisi ya Rais, Ikulu inatarajia kutumia kiasi cha Sh. 9,146,327,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inatarajia kutumia kiasi cha Sh. 217,100,430,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiasi cha Sh. 50,382,037,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu itaendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na:-

(i) Kuendelea kutoa huduma kwa Rais na familia yake;

(ii) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kimataifa na kazi nyingine zinazohusu kumshauri Rais;

(iii) Kuendesha mafunzo kwa Kamati za Uadilifu za Wizara, Taasisi za Umma na Asasi za Kiraia 50 pamoja na Kamati za Uadilifu katika Utumishi wa Umma zinazosimamia utawala bora nchini ili Taasisi hizo ziweze kuwa msaada katika masuala ya kupambana na rushwa;

(iv) Kukamilisha tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Awamu ya Pili wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kwa kuwahusisha wadau wote na kutayarisha Mpango wa Awamu ya Tatu;

(v) Kuendelea kuelimisha watumishi juu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na UKIMWI mahali pa kazi;

(vi) Kufanya uchambuzi na kutoa maoni na ushauri kuhusu Nyaraka za Baraza la Mawaziri na masuala mbalimbali;

(vii) Kuandaa na kufanya mkutano wa Tathmini ya Utekelezaji wa Maamuzi ya Baraza la Mawaziri, utakaoshirikisha Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri Wizarani;

(viii) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa na malalamiko ya watumishi wa umma na wananchi. Vile vile, Taarifa za Tume ya Utumishi wa Umma na za Mamlaka mbalimbali zitapokelewa na kuchambuliwa;

(ix) Kupanga na kuendesha vikao 12 vya Uratibu wa Maboresho kwa Makatibu Wakuu na Waratibu wa

Programu za Mabadiliko kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa Mabadiliko katika sekta ya umma nchini;

(x) Kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na Kutunza kumbukumbu za masuala ya Mabadiliko katika Sekta ya Umma;

(xi) Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (*Open Government Partnership (OGP)*);

(xii) Kuendelea kuratibu masuala ya siasa na mahusiano ya jamii;

(xiii) Kuimarisha mifumo ya Utungaji na Utekelezaji wa Sera, Ufuatiliaji na Tathmini na Uratibu wa Mabadiliko; na

(xiv) Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Katika mwaka 2012/2013, TAKUKURU imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kuchunguza tuhuma 2,774 zilizopo na tuhuma mpya zitakazojitokeza;

(ii) Kuendelea na uchunguzi maalum wa Vocha za Pembejeo za Kilimo, Maliasili na tuhuma zilizobainishwa na taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu

wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2010/2011 kuhusu ubadhirifu katika Wizara na Mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa;

(iii) Kukamilisha uchunguzi wa tuhuma saba (7) za rushwa kubwa (*Grand Corruption*);

(iv) Kuendelea kuendesha kesi 478 zilizopo mahakamani na zitakazoendelea kufunguliwa kutokana na kukamilika kwa chunguzi mbalimbali;

(v) Kuendelea kutoa elimu kuhusu rushwa na athari zake kwa wananchi, watumishi wa Serikali na makampuni binafsi na kuendeleza ushirikiano na asasi za kiraia katika mapambano dhidi ya rushwa;

(vi) Kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania kuratibu utekelezaji wa Mpango Mkakati wa kutambua hali ya rushwa na maoni ya wadau kuhusu kuingizwa somo la maadili, mapambano dhidi ya rushwa na utawala bora katika mitaala ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu;

(vii) Kuendelea kutoa mafunzo ya mapambano dhidi ya Rushwa na Miundombinu ya Maadili kwa Kamati za Uadilifu zilizoanzishwa katika Wizara, Idara na Halmashauri za Wilaya ili kuzijengea uwezo wa kushughulikia masuala yote ya maadili sehemu zao za kazi kwa kuhakikisha kuwa wale wote wanaokiuka maadili ya kazi wanachukuliwa hatua za kinidhamu;

(viii) Kuendelea kuimarisha mifumo ya utendaji dhidi ya mianya ya rushwa kwa kufanya utafiti na

udhibiti wa mianya hiyo katika sekta za Madini na Maliasili;

(ix) Kushirikisha wadau kwa kufanya warsha, kujadili matokeo ya tafiti, kuweka mikakati ya kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya kudhibiti mianya ya rushwa;

(x) Kuratibu Mpango wa Taifa kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Taarifa ya Utafiti wa Hali ya Rushwa na Utawala Bora Nchini; na

(xi) Kukamilisha ujenzi wa ofisi za TAKUKURU katika Mikoa ya Tabora, Ruvuma na Wilaya za Kasulu na Newala na kuanza ujenzi wa ofisi za Mikoa ya Mbeya na Mara.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Katika mwaka 2012/2013, MKURABITA imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea na uratibu wa marekebisho ya Sheria ya Ardhi mjini Sura Namba 113 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Sura Namba 114 kwa kushirikiana na Wizara za kisekta Tanzania Bara;

(ii) Kuanza urasimishaji wa ardhi vijiji sambamba na kujenga uwezo kwa Halmashauri za Wilaya sita Tanzania Bara katika vijiji viwili kila Wilaya. Halmashauri hizi ni Misungwi, Uyui, Chamwino, Tandahimba, Ngara na Kiteto. Aidha, masjala ya ardhi ya vijiji zitajengwa

katika vijiji 12 ambavyo shughuli za kujenga uwezo zitafanyika;

(iii) Kufanya urasimishaji wa ardhi mijini na kujenga uwezo katika Halmashauri za Miji minne Tanzania Bara. Halmashauri hizi ni Moshi, Iringa, Babati na Mbeya. Urasimishaji ardhi mijini utafanyika katika mji mmoja wa Zanzibar;

(iv) Kujenga uwezo na kufanya urasimishaji wa ardhi vijijini katika Wilaya mbili za Zanzibar na kuanza urasimishaji wa biashara katika miji mitatu (3) ya Zanzibar;

(v) Kuanza urasimishaji wa mashamba ya wakulima wa chai katika vijiji 104 katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe. Wakulima ambao mashamba yao yatarasimishwa watajengewa uwezo wa namna ya kutumia hati zao kukuza mitaji kwa maendeleo zaidi;

(vi) Kuanza urasimishaji wa mashamba ya wakulima wa miwa katika Halmashauri za Wilaya ya Kilombero, Kilosa, Misenyi na Mvomero;

(vii) Kuendelea kuratibu zoezi la kutengeneza na kutoa Hati Miliki za kimila kwa wamiliki wa mashamba na kuwajengea uwezo wa namna ya kuzitumia hati hizo katika wilaya 13 ambazo upimaji ulishakamilika. Wilaya hizo ni Masasi, Mkuranga, Meru, Mwanga, Moshi, Geita, Kasulu, Muleba, Kahama, Sikonge, Mbarali, Sumbawanga na Mbinga;

(viii) Kuendelea na uratibu wa shughuli za kutengeneza na kutoa Hati Miliki katika maeneo ya Tunduma – Mbeya na Kimara Baruti, Dar es Salaam;

(ix) Kuanza urasimishaji wa biashara katika Miji mitatu ambayo ni Mbeya, Tanga na Morogoro. Tathmini ya matokeo ya urasimishaji biashara utafanyika katika Manispaa ya Arusha na Jiji la Mwanza;

(x) Kuratibu mchakato wa uanzishwaji wa Chombo cha Kitaifa cha Urasimishaji wa Rasilimali Ardhi na Biashara chenye nguvu ya kisheria ambacho kitasimamia ukuaji wa sekta rasmi katika uchumi wa nchi;

(xi) Kukamilisha uanzishwaji wa Mfuko wa Urasimishaji wa Wilaya na kufanyiwa majaribio katika wilaya mbili; na

(xii) Kukamilisha taratibu za kurahisisha mifumo ya kodi na uandikaji wa vitabu vya mahesabu kwa wafanyabiashara wadogo na wa kat; na

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*). Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2012/2013 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuzindua utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya TASAF kwa kuhamasisha Wadau mbalimbali katika ngazi zote na kuendelea kukusanya takwimu za awali (Baseline Data collection) kwa ajili ya kupima mafanikio ya utekelezaji baadaye;

(ii) Kuziwezesha Halmashauri za Tanzania Bara na Zanzibar kuibua miradi itakayoboresha huduma za jamii na kuongeza kipato. Jumla ya miradi 900 itaibuliwa na wananchi;

(iii) Kuendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi 1,778 vilivyoanzishwa vyenye wanachama 22,712 kutoka katika Halmashauri 44 lengo likiwa katika kuimarishe ili shughuli zao ziendelee kwa ufanisi zaidi;

(iv) Kutekeleza Mpango wa Jamii wa Uhawilishaji Fedha kwa kaya maskini sana katika Halmashauri za majaribio za Wilaya za Bagamoyo, Chamwino na Kibaha ili kuongeza kaya zinazonufaika kutoka 4,985 za sasa hadi kufikia kaya 20,000 zikiwa na walengwa 100,000;

(v) Kukuza uelewa wa wananchi wanaotekeleza miradi kuhusu Kanuni na Taratibu za utekelezaji wa miradi kwa kutumia vipindi vyta redio, televisheni na machapisho mbalimbali;

(vi) Kuimarishe mifumo ya taarifa kwa kufanya marekebisho na kujenga mifumo mipyta itakayoendana na mahitaji ya Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii;

(vii) Kufanya ukaguzi wa fedha za mradi ili kujiridhisha na matumizi ya fedha, ubora wa miradi inayoteklezwa na kujiridhisha kuwa miradi inatekelezwa kwa kuzingatia miongozo ya sekta husika; na

(viii) Kufuatilia na kufanya tathmini ya miradi inayotekelezwa ili kubaini hatua zilizofikiwa katika kuondoa umaskini kwa walengwa walionufaika na msaada kutoka *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF). Katika mwaka 2012/2013, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kutoa huduma ya mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati Mijini na Vijijini;

(ii) Kuendelea kutoa huduma ya ushauri na mafunzo ya kibashara kwa wateja kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali zinazotoa mafunzo ili kuongeza ufanisi katika biashara zao; na

(iii) Kuendelea kujenga uwezo kwa wadau/watendaji na wafanyakazi ili kuweza kutoa huduma za viwango vya juu na kuongeza tija katika utoaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uongozi katika mwaka 2012/2013, Taasisi ya Uongozi imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuainisha na kutayarisha kozi 18 zikiwa ni sehemu ya programu ya ufanisi katika usimamizi wa sekta ya Umma. Mafunzo yatatolewa katika programu nne za Ufanisi katika Usimamizi wa Sekta ya Umma, Mkakati wa Uongozi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu,

Menejimenti inayozingatia Matokeo na Kutafakari Matokeo ya Uongozi na Kuchukua Hatua;

(ii) Kuainisha na kutayarisha kozi tano (5) mpya katika programu zifuatazo: Mkakati wa Uongozi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu, Menejimenti inayozingatia Matokeo na Kutafakari Matokeo ya Uongozi na Kuchukua Hatua;

(iii) Kufanya tafiti mbili (2) zinazohusu hali ya uongozi nchini na katika nchi sita katika Bara la Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na maendeleo ya utawala bora Tanzania;

(iv) Kufanya mahojiano na Wakuu wa Nchi waliopo madarakani na waliostaafu ndani na nje ya nchi na Wataalam mbalimbali kuhusu uongozi na maendeleo endelevu ili kukuza uelewa na kupata uzoefu kwa viongozi na kurusha mahojiano hayo katika televisheni;

(v) Kuandaa mikutano ya majadiliano itakayowahusisha viongozi na wataalamu kuzungumzia masuala mbalimbali ya uongozi na maendeleo endelevu;

(vi) Kutengeneza mtandao wa ndani (intranet) na kuzindua rasmi tovuti ya Taasisi;

(vii) Kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Mwasiliano ya Taasisi ya Uongozi; na

(viii) Kuchapisha ripoti tano (5) za tafiti zinazohusu Hali ya Uongozi Nchini; Usimamizi Bora wa Maliasili Barani Afrika; Tathmini ya Utawala Bora katika Taasisi za Umma; Vigezo vya Utawala Bora Afrika; na Tathmini ya Hali Halisi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake. Ili kutekeleza Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma inatarajia kutumia jumla ya Sh. 42,431,553,000.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo Sh. 20,021,986,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 22,409,567,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. katika mwaka wafedha 2012/2013 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa umma zinazingatiwa na Watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi wanapotoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itarekebisha mishahara ya watumishi wake kwa kuzingatia uwezo wa bajeti na makubaliano yaliyofikiwa na Baraza la Majadiliano ya Pamoja Katika Utumishi wa Umma lilitoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja Katika Utumishi wa Umma Sura Namba 105 ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Serikali inatarajia kutumia Sh. 3,781,100,000,000 kugharamia malipo ya mshahara, upandishwaji vyeo na kulipia madai ya malimbikizo na mapunjo ya mishahara kwa Watumishi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Wakala na Taasisi za Serikali. Kiasi hicho kimeongezeka kwa Sh. 510,807,000,000 ambacho ni sawa na asilimia 15.6 ya kiasi kilichokuwa kimepangwa kutumika mwaka wa fedha 2011/2012. Kwa hiyo wale wote wenyewe madai mbalimbali watalipwa madai yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua za kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma Serikali itaendelea kutekeleza Sera ya Malipo ya Mshahara na Motisha katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia mkakati wake wa utekelezaji, ambapo inatarajiwa kazi kubwa katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 ni kuandaa mwongozo wa kutoa motisha kwa watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Aidha, Serikali itafanya utafiti kuhusu mishahara na maslahi ya wafanyakazi baina ya sekta binafsi na Serikali kwa lengo la kuwanisha na kuoanisha mishahara ya watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 56,678 ambapo kipaumbele kitakuwa katika sekta za Elimu, Afya, Kilimo pamoja na Mifugo. Nafasi hizi hazijumuishi nafasi mpya za baadhi ya vyombo vyadola. Aidha, Serikali inatarajia kuwapandisha vyeo

watumishi 42,419 wa kada mbalimbali. Kwa rejea zaidi nawaomba Waheshimiwa Wabunge waangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kusimamia matumizi sahihi ya rasilimaliwatu pamoja na kuratibu ajira katika Utumishi wa Umma kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kukamilisha usambazaji na kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Serikali; na

(ii) Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa Orodha ya Malipo ya Mishahara na Matumizi ya Rasilimaliwatu ili kuhakikisha watumishi waliopo wanatumika kwa ukamilifu na wanalipwa mishahara kulingana na stahili zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuwahudumia Viongozi Wastaafu wa Kitaifa kwa mujibu wa Sheria ya Mafao ya Viongozi Sura Namba 225. Aidha, ujenzi wa msingi wa Kituo cha Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na hayati Sheikh Abeid Amani Karume) utaanza katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutatua tatizo la uhaba wa ofisi na gharama kubwa za pango, Serikali itaandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Ofisi ili kutoa mazingira bora ya kufanyia kazi kwa watumishi

wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI; Tume ya Utumishi wa Umma; Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; na Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma Sura Namba 105 kwa kuratibu uendeshaji wa Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, Mabaraza ya Majadiliano ya Pamoja ya Kisekta, Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma na Mabaraza ya Wafanyakazi mahali pa Kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine zitakazotekelawa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni pamoja na:-

(i) Kuhuisha na kuwianisha Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali zinazosimamia utendaji katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kuratibu uanzishwaji na uendelezaji wawakala wa serikali na kuhuisha miundo, mifumo ya utendaji kazi na viwango vya kimenejimenti vinavyolenga katika kuboresha utoaji wa huduma katika utumishi wa umma;

(iii) Kusimamia mifumo ya utendaji kazi iliyoanzishwa kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utoaji huduma katika utumishi wa umma;

(iv) Kukamilisha taratibu za kuwezesha kutumika kwa Kituo cha Taifa cha kuhifadhi Kumbukumbu Tuli kilichopo Dodoma;

(v) Kuendelea na ujenzi wa Kituo cha kuhifadhi Kumbukumbu Tuli Kanda ya Ziwa - Mwanza;

(vi) Kuweka mfumo mpya wa utunzaji kumbukumbu(keyword system) katika Masijala za Ofisi 30 za Wakuu wa Wilaya na Wakala wa Serikali 4;

(vii) Kuweka mfumo wa Utunzaji wa Majalada ya Watumishi katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa 21;

(viii) Kuboresha mifumo ya utunzaji kumbukumbukatika Ofisi nne (4) za Ubalozi;

(ix) Kuimarisha mifumo ya taarifa, mawasiliano ya habari Serikalini, matumizi ya TEHAMA na kuhakikisha kuwa inatoa taarifa zilizo sahihi zitakazosaidia watendaji kufanya maamuzi yaliyo sahihi;

(x) Kuendelea kutoa huduma saidizi za kitaalam (*technical support services*) kwa watumiaji wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala na Taasisi nyingine za Serikali;

(xi) Kuunganisha Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara na miundombinu ya

mawasiliano ya Mfumo wa *Epicor* katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xii) Kuunganisha Taasisi zote za Serikali zilizoko Dar es Salaam katika Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali kwa kuzingatia matokeo ya upembuzi yakinifu uliofanyika;

(xiii) Kusimamia uendelezaji wa stadi za uongozi na kuwaendeleza watumishi wa umma kitaaluma kwa kuzingatia makundi maalum;

(xiv) Kufuatilia na kuzijengea uwezo Kamati za UKIMWI za Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali kwa kuzipatia mafunzo ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yake;

(xv) Kukuza na kusimamia uzingatiaji wa maadili katika utumishi wa umma kwa lengo la kupunguza malalamiko na kero mbalimbali za wananchi zinazotokana na kukiukwa kwa maadili ya kazi; na(xvi) Kuendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuendeleza Mabadiliko katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Utumishi wa Umma (*TPSC*). katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kitakeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuwajengea uwezo watumishi wa Chuo wapatao 75 katika fani mbalimbali;

- (ii) Kuandaa na kuendesha koz 84 kwa washiriki 7,035 wa fani mbalimbali;
- (iii) Kutoa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya *Diploma* na Cheti kwa washiriki 14,739;
- (iv) Kufanya tafiti 16 katika masuala mbalimbali;
- (v) Kuendesha shauri za kitaalam 32;
- (vi) Kuandaa machapisho 24, majarida mawili (2)na kuandika vitabu tisa (9); na
- (vii) Kuimarisha ushirikiano na Vyuo vya ndani na nje ya nchi na taasisi nyingine zikiwemo Chuo cha Utumishi Canada (*IPAC*); *Institute of Public Administration India*; *INTANMalaysia*; Chuo cha Utawala cha Uingereza; Chuo Kikuu cha Afrika (*Africa University – Zimbabwe*); *Africa Capacity Building Fund (ACBF)*; *AMDIN*; Chuo Kikuu Mzumbe; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; *ESAMI* na Taasisi ya Uongozi kwa lengo la kujenga uwezo pamoja na kuboresha utoaji wa huduma za mafunzo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (*TaGLA*). Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (*Tanzania Global Learning Agency (TaGLA)*) ni Wakala wa Serikali 61ulioundwa kwa Sheria ya Wakala za Serikali Sura Namba 245. Wakala huu unachukua majukumu ya kilichokwuwa Kituo cha Kutoa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (*Tanzania Global Distance Learning Centre (TGDLC)*). Lengo la kukibadilisha Kituo hiki kuwa Wakala ni kukipa mamlaka

ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandoa itatekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Ummana Sekta Binafsi 1,500 katika maeneo ya Utawala Bora, Kupunguza Umasikini, Uongozi, Jinsia, Afya, Mazingira, Kilimo na Masoko, Matumizi ya Teknolojia ili kuboresha Utendaji Kazi Serikalini na katika Sekta binafsi;
- (ii) Kuwawezesha Watanzania kushiriki katika Midahalo 40 ya Kimataifa ya Maendeleo kwa njia ya mtando;
- (iii) Kuhakikisha kwamba huduma za Wakala zinawafikia Watanzania wengi na hivyo kuwzesha matumizi ya teknolojia mpya zinazopatikana nchini na nje ya nchi kwa kuingia ubia na taasisi nyingine zenyе majukumu yanayofanana; na
- (iv) Kuwajengea uwezo watumishi watano (5) wa Wakala ili kukidhi mahitaji ya umma na matumizi ya teknolojia.

Wakala wa Serikali Mtando (e-GA). Wakala wa Serikali Mtando ni Taasisi ya Serikali iliyoundwa kwa Sheria ya Wakala za Serikali Sura Namba 245. Wakala wa Serikali Mtando ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtando kwa Wizara, Wakala, Idara Zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji na utoaji wa

huduma kwa wananchi kwa haraka na kwa viwango na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wakala wa Serikali Mtandao itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutengeneza miongozo na viwango kwa ajili ya utekelezaji wa mifumo ya Serikali Mtandao;

(ii) Kuboresha na kujenga uwezo wa Rasilimaliwatu kwa ajili ya kuendeleza utawala wa ndani wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika nyanja za utaalamu wa kiufundi;

(iii) Kutekeleza mfumo jumuishi wa mawasiliano ya Serikali;

(iv) Kuongeza ufahamu kwa wadau juu ya Serikali Mtandao na ushiriki wao katika mipango ya kuanzisha programu mbalimbali na miradi inayohusiana na Serikali Mtandao; na

(v)Kuanzisha na kuhimiza matumizi ya viwango na miongozo ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utekelezaji wa Serikali Mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa umma. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba jumla ya Sh. 7,390,692,000 Kati ya fedha hizo, Sh. 5,923,437,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya

Kawaida na Sh. 1,467,255,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kupokea na kufanya uchambuzi na uchunguzi wa awali wa malalamiko ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili dhidi ya Viongozi wa Umma;
- (ii) Kuandaa na kusambaza Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma 8,972 na kufanya uhakiki wa Rasilimali hizo;
- (iii) Kuwaelimisha Viongozi wa Umma na wananchi kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (iv) Kuendelea kukuza na kusimamia uendelezaji wa stadi za Uongozi wa Watumishi wa Taasisi kitaaluma;
- (v) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili;
- (vi) Kuboresha mifumo ya upokeaji, utunzaji na upatikanaji wa kumbukumbu katika Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (vii) Kuboresha miundo na mifumo ya utoaji wa huduma bora kwa Taasisi;

(viii) Kuhuisha Mpango Mkakati wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(ix) Kufanya utafiti kuhusiana na suala lakutenganisha Uongozi wa Umma na Biashara; na

(x) Kuendelea kufanya uratibu wa marekebisho ya Sheria ya Maadili Sura Namba 398.

Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Ili kutekeleza Mpango wa mwaka 2012/2013, Sekretarieti ya Ajira inatarajia kutumia jumla ya Sh.2,494,524,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendesha usaili kwa nafasi wazi za kazi 18,105 katika Utumishi wa Umma kwenye: Wizara na Idara Zinazojitegemea 7,896; Sekretarieti za Mikoa nafasi 1,339; Halmashauri za Wilaya nafasi 7,892; Taasisi na Wakala za Serikali nafasi 978. Nafasi hizi ni nje ya nafasi zinazohusu Wizara ya Kilimo, Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Elimu, Afya na Mifugo;

(ii) Kufungua ofisi Zanzibar kwa ajili ya ajira za Muungano;

(iii) Kuendelea kuimarisha Kanzidata na kutunza Takwimu za wahitimu kutoka kwenye Vyuo mbalimbali kwa urahisi wa rejea;

(iv) Kuendelea kutembelea waajiri na wadau mbalimbali kwa ajili ya kujitangaza na kupata mrejesho wa shughuli zake; na

(v) Kujaza nafasi za watumishi 96 zilizo wazi katika Sekretarieti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma. Ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kutumia Sh.7,938,210,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kuandaa na kuratibu mikutano ya kila robo mwaka ya Tume, kutoa maamuzi ya Rufaa na Malalamiko kadri yatakavyopokelewa;

(ii) Kufanya ukaguzi wa rasilimaliwateru kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu; kufuatilia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za usimamizi wa Rasilimaliwateru katika Utumishi wa Umma;

(iii) Kuendelea kuelimisha wadau kuhusu shughuli za Tume kupitia njia mbalimbali kama vile vyombo vyahabari, maonesho na ziara;

(iv) Kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kisheria kupitia Idara ya Utumishi wa Walimu kama Mamlaka ya ajira na nidhamu kwa walimu nchini;

(v) Kuendelea kufanya tafiti kulingana na mahitaji ya Tume na wadau wake;

(vi) Kuendelea kutoa elimu kwa watumishi wa Tume kuhusu maadili ya kazi na kujiepusha na

mazingira hatarishi kwa maambukizi ya VVU/UKIMWI na mapambano dhidi ya rushwa; na

(vii) Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa Tume katika ngazi zote kwa kuwapatia vitendea kazi na kuwajengea uwezo kitaaluma watumishi 60.

Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma. Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma ni chombo kilichoundwa chini ya Ibara ya 36(1) ya Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977. Uanzishwaji wake umefanyika kwa Hati ambayo ilitolewa kupitia Tangazo la Serikali Na.162 la tarehe 3 Juni, 2011. Majukumu ya Bodi hiyo ni kama yafuatayo:-

(i) Kufanya tafiti juu ya hali ya mishahara ikilinganishwa na hali halisi ya uchumi ili kutoa mapendekezo yanayohusiana na marekebisho ya mishahara pamoja na maslahi;

(ii) Kukusanya, kulinganisha na kuchambua taarifa zinazohusiana na masuala ya gharama za maisha, nyumba na vigezo vingine vinavyohusiana na malipo ya posho na maslahi mengine;

(iii) Kutoa mapendekezo juu ya kiwango cha mishahara, posho na maslahi kwa ajili ya Mihimili mitatu ya Dola;

(iv) Kutoa ushauri kuhusu Misingi ya Miundo ya Mishahara katika Utumishi wa Umma; na

(v) Kushauriana na Taasisi husika za Serikali juu ya bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya malipo ya mishahara na maslahi ya Watumishi wa Umma.

Ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2012/2013 kwa ufanisi, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma inatarajia kutumia Sh. 2,387,259,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kujenga uwezo wa Watumishi 41 wa Bodi;
- (ii) Kuandaa Kanuni za Utendaji, Mpango Mkakati na Mpango Kazi;
- (iii) Kutoa elimu ya uelewa kwa wadau kuhusu majukumu ya Bodi;
- (iv) Kuweka Mfumo wa Teknolojia ya Mawasilianokwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Bodi;
- (v) Kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusiana na uwiano baina ya tija, mishahara na maslahi;
- (vi) Kufanya tafiti, kuchambua na kutoa ushauri kuhusiana na mishahara na maslahi kwa Kamati za Kudumu za Utendaji, Mahakama, Bunge na Vyombo vya Ulinzi na Usalama;
- (vii) Kuandaa vikao vya Bodi na taarifa mbalimbali;

(viii) Kuandaa mfumo utakaotumika kukadiria mishahara na maslahi kwa Watumishi wa Umma; na

(ix) Kuhuisha mishahara na maslahi kwa kuzingatia tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabla ya kuwasilisha rasmi Maombi ya Fedha kwa mwaka 2012/2013, naomba nichukue fursa hii kuwasilitizia watumishi wote wa umma kuhusu umuhimu wa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi katika Maendeleo ya Taifa linalotarajiwa kufanyika kuanzia Agosti 26, 2012. Ili kufanikisha zoezi hili kwa ufanisi, natoa wito kwa Watendaji wa Taasisi zote za Umma, kuwahamasisha watumishi walioko katika Taasisi zao kushiriki kikamilifu katika zoezi hili muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi iwe na uchumi imara na endelevu tunahitaji pamoja na mambo mengine Utumishi wa Umma unaozingatia misingi ya utawala bora ambapo Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zinatumika katika kusimamia uchumi na uendeshaji wa shughuli za umma.

Taasisi zenyе jukumu la kuhakikisha mazingira haya yanakuwepo ni Ofisi za Rais - Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Umma, na Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma.

Hivyo, Mipango ya Utekelezaji ya mwaka 2012/2013 ya Taasisi hizi za Serikali inalenga kufanikisha majukumu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza mapitio ya Mipango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na Mipango ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naomba kuwasilisha rasmi Mapendeleko ya Maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

(a) Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu

Matumizi ya Kawaida	Sh.
9,146,327,000/=	
Jumla	Sh.
9,146,327,000/=	

(b) Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

(i) Matumizi ya Kawaida.....	Sh. 217,100,430,000/=
(ii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh. 50,382,037,000/=
Jumla	Sh. 267,482,467,000/=

(c) Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

(i) Matumizi ya Kawaida	Sh.
20,021,986,000/=	

(ii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo..... Sh.
22,409,567,000/=
Jumla Sh. 42,431,553,000/=

(d) Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

(i) Matumizi ya Kawaida Sh. 5,923,437,000/=
(ii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo..... Sh.
1,467,255,000/=
Jumla Sh. 7,390,692,000/=

(e) Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida Sh. 2,494,524,000/=
Jumla Sh. 2,494,524,000/=

(f) Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida Sh 7,938,210,000/=
Jumla Sh. 7,938,210,000/=

(g) Fungu 9: Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida Sh. 2,387,259,000/=
Jumla Sh. 2,387,259,000/=

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo,
niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa

kunisikiliza na ninaomba hotuba yangu kwa ujumla yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri mwenye dhamana ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kutoka Ofisi ya Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Waziri wakati unasoma hotuba yako ulikuwa unarejea vifungu vilivyokuwa vinatoa ufanuzi ukurasa mmoja baada ya mwingine, kumetokea tatizo kidogo kurasa zako ulizokuwa umezisema ziliwu haziendani sambamba na kurasa ambazo ziko katika kitabu cha hotuba.

Kwa hiyo nitaomba tu ututayarishie *addendum* itakayoweza tusaidia kurekebisha pale uliposema ukurasa wa 54 mpaka 55 kwa mfano ukitoa ufanuzi wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake kazi zilizopangia kufanya, lakini unazikuta kazi hizo ukurasa wa 58 na 59 mpaka ukurasa wa 60.

Kwa hiyo unaona kwamba mwongozo uliokuwa unatupa maudhui na maneno yote yako sawasawa

kabisa. Lakini tatizo kidogo lilikuwa ni zile kurasa jinsi ulivyoziandaa vizuri kwenye hotuba yako na jinsi zilivyojitokeza kwenye kitabu chako cha Bajeti.

Kwa hiyo hili kuweka hizo kumbukumbu sawa na sahihi kabisa kwenye *Hansard* na kuziweka sawasawa katika matumizi ya Ofisi ya Bunge, lakini matumizi pia ya Waheshimiwa Wabunge nitaomba tu uchukue *Hansard* uipitie vizuri uweze kutengeneza *addendum* uweke marekebisho katika maeneo hayo ili kumbukumbu hizo ziweze kuwa rasmi kwa ajili ya Ofisi yetu ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa mawasilisho yake kabla sijamwita Waziri aliyefuata nimepewa msisitizo sana wa kikao cha leo cha Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Lwanji ameniomba sana na ameleta tangazo hapa niwaambie Waheshimiwa Wabunge hata kule nje na mahali popote mlipo, kwamba leo pia saa 7.00 mchana Kamati hiyo itakuwa na kikao Ukumbi Na. 227.

Kwa hiyo naomba niwasitisize sana Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge, Katiba, Sheria na Utawala kwamba mtakuwa na kikao muhimu sana leo saa 7.00. Tangazo hili lilichelewa kuletwa, kwa hiyo naomba lichukuliwe kama tangazo rasmi na Waheshimiwa Wabunge naomba mjiandae kwenda kwenye Kamati hiyo.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Waziri anayefuata sasa nitamwita Mheshimiwa George

Mkuchika atasoma hotuba kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)(K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema nimesimama hapa kusoma hotuba ya Mheshimiwa Stephen Massatu Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Rais, Tume ya Mipango. Kama tunavyofahamu Mheshimiwa Wassira amefiwa na Mama yake Mzazi na sasa yuko jimboni kwake Bunda kwa shughuli za msiba. Tunampa pole Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Stephen Wassira, kwa msiba uliompata na tunamtakia Marehemu Mwenyezi Mungu aweke roho yake mahali pema peponi, Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa tangu nimekwenda Wizara mpya, napenda nichukue nafasi hii tena kuwashukuru Wapiga kura wangu wa jimbo la Newala, kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao. Aidha, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Jakaya Kikwete, kwa kuendelea kuniamini, kuendelea kunitfea katika Wizara mbalimbali na safari hii amenipanga nimsaidie katika Ofisi yake katika masuala yanayohusu Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kuishukuru familia yangu hasa mke wangu Anna Ernestina Mkuchika, watoto wangu wote, watano na wajukuu zangu wawili Evelyn na Ethan kwa ushirikiano wanaonipa. Ninajua wanankosa sana

ninapokuwa ninatekeleza majukumu ya Kitaifa, lakini naambiwa wanafurahi sana wanaposikia baba yao au babu yao anafanya mambo mazuri anapotekeleza majukumu ya nchi. Ahadi yangu kwa Wapiga kura wa Newala, ahadi kwa Mheshimiwa Rais, na ahadi kwa Watanzania wote ni kuendelea kuwatumikia kwa juhudhi na maarifa ili kuhakikisha kwamba nchi yetu Tanzania panaendelea kuwa mahali pazuri pa kuishi, kwa amani na utulivu, lakini tukizingatia Utawala Bora ambazo ndiyo shughuli zangu za sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja kwamba kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango (Fungu 66), Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Mipango, kwa Mwaka 2011/2012. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali Kujadili na Kupitisha Makadirio ya Tume ya Mipango, kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2012/2013. Aidha, naomba kuishukuru Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wake Mtemi Mheshimiwa Andrew Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi kwa ushirikiano na ushauri mzuri iliyotupatia wakati wa kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka

2011/2012 na makadirio ya fedha kwa mwaka 2012/2013, hatua ambayo imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha Bungeni hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Dkt. Philip Mpango, Naibu Makatibu Watendaji na watumishi wote wa Tume ya Mipango, ambao wamefanya kazi kubwa ya kuwezesha hotuba hii kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2011/2012 kama ifuatavyo:-

Utekelezaji wa ahadi za Serikali Bungeni ahadi zilizotolewa Bungeni chini ya Fungu 66 – Tume ya Mipango, kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 zimetekelizwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuitangaza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/2016).

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudhi mbalimbali zilifanyika za kuitangaza Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025) na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa wadau mbalimbali. Jithada zilizofanyika ni pamoja na kuandaa na kutoa machapisho, makala na vipeperushi vifuatavyo:-

(a) Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025: Tume ya Mipango ilisambaza vitabu vya Dira 2025 na

vipeperushi vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

(b) Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012–2015/2016: Tume ya Mipango ilichapisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 -2015/2016 na muhtasari wake; na pia vipeperushi vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango ilitumia maadhimisho ya miaka 50 ya uhuru wa Tanzania Bara kuitangaza Dira 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012- 2015/2016) kwa kuandaa vipindi vyta televisheni na radio kuelimisha umma. Vipindi hivyo vilishirikisha baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Viongozi wa kitaifa wastaaafu, viongozi wastaaafu wa iliyokuwa Tume/Wizara ya Mipango na wataalam wengine wa Uchumi na Mipango nchini. Machapisho ya Dira 2025 na Mpango wa Miaka mitano yamewekwa kwenye tovuti ya Taifa na ile ya Tume ya mipango ili kuweza kuwafikia wadau wengi kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango ilipata nafasi ya kutoa mada kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano katika: Semina Elekezi ya Viongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Semina ya mafunzo ya Makatibu Tawala wa Mikoa; Mkutano wa Watanzania wanaoishi ughaibuni (*Diaspora*) Marekani na Kanada; na semina ya mafunzo ya Wakuu wa

Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Makatibu Tawala wa mikoa wapya.

Pia, semina ya mashirika yasiyo ya kiserikali, hususan Baraza la Maendeleo la Kilimanjaro (*Kilimanjaro Development Forum (KDF)*); Washirika wa Maendeleo; na Baraza la Wafanyakazi wa UTUMISHI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuitangaza Dira 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano inaendelea sanjari na utekelezaji wake. Aidha, kazi ya kuhariri na kutafsiri Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012-2015/2016) kwa lugha ya Kiswahili imekamilika, ikiwa ni pamoja na kujumuisha ushauri na maoni ya Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango imekamilisha Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/2012 - 2025/2026). Mpango huu umejadiliwa katika ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Wadau ndani ya Serikali, Sekta Binafsi, Taasisi za Elimu ya Juu na za Utafiti, Washirika wa Maendeleo na Asasi Zisizo za Serikali.

Pia Waheshimiwa Wabunge wote walipatiwa nakala ili watoe maoni na ushauri. Tume ya Mipango imekamilisha kazi ya kuboresha rasimu hiyo kwa kuzingatia maoni na mapendekezo ya wadau na tayari Mpango huo umeridhiwa na Serikali na pia Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuibua na kufanya tafiti kuhusu masuala ya uchumi na ustawi wa jamii. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, tafiti tatu katika maeneo ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi zilipangwa kufanyika. Hata hivyo, kutokana na kutopatikana fedha kwa wakati, tafiti hizo zilichelewa kuanza, kwa sasa mikataba ya kutekeleza tafiti hizo imesainiwa. Tafiti hizo ni:-

(i) Uendelezaji wa taaluma na ujuzi unaohitajika kuiwezesha Tanzania kuwa na nguvu za kiushindani kiuchumi ifikapo 2025: Matokeo ya Utafiti huu yataisaidia Serikali kubaini mapungufu yaliyopo katika mfumo wa utoaji elimu na mafunzo ya ufundi nchini, ambayo ni kikwazo katika maendeleo ya sekta za kiuchumi na kijamii;

(ii) Muundo wa kitaasisi kwa ajili ya kuharakisha maendeleo ya sekta ya viwanda nchini: Lengo la utafiti huu ni kuelekeza sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vyatagifundishwa na kipaumbele;na

(iii) Miundombinu ya kilimo cha kisasa na cha kibiashara Tanzania: Utafiti huu unalenga kuainisha mapungufu ya miundombinu inayohitajika na kutoa mapendekezo ya namna ya kuiboresha na kuiendeleza ili kufanya kilimo kuwa cha kisasa zaidi na cha kibiashara, tafiti zote hizo zinatarajiwa kukamilika katika mwaka 2012/2013. Utafiti pekee uliokamilika ni kuhusu "Jinsi Tanzania inavyoweza kunufaika kutokana na Mahusiano ya Kiuchumi na Biashara ya Kikanda na Kimataifa". Mapendekezo yanayotokana na utafiti yatawasilishwa Serikalini katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango kwa Kushirikiana na Kituo cha Kimataifa cha Kupunguza Umaskini cha China (*International Poverty Reduction Center of China (IPRCC)*) zimefikia makubaliano ya kushirikiana kuendesha tafiti kuhusu masuala ya maendeleo na ustawi wa jamii, na kuanzisha kituo cha IPRCC hapa nchini, kituo hicho kitaanza kazi mwaka 2012/2013. Aidha, Tume ya Mipango inaendelea na mazungumzo na Kituo cha Kimataifa cha Ukuza ji wa Uchumi (*International Growth Centre (IGC)*) kuhusu kuandaa na hatimaye kutekeleza agenda ya pamoja ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga/kuimarisha uwezo wa watumishi. Pamoja na juhudu kadhaa zilizobainishwa awali, katika mwaka 2011/2012, Tume ya Mipango imeajiri watumishi wapya saba, ikiwa ni pamoja na kujaza nafasi ya Naibu Katibu Mtendaji - Klasta ya Uchumi Jumla, iliyokuwa wazi kwa muda mrefu. Aidha Watumishi 12 walioajiriwa mwezi Mei 2011 walifanyiwa upekuzi na kupata mafunzo ya awali (*Induction Course*) kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa umma. Vilevile, nafasi 5 za Katibu Mahsus Daraja la III zimepata kibali cha ajira. Katika kuimarisha uwezo wa watumishi, watumishi 10 wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu, kati ya hao, 2 ni wa shahada ya uzamivu (*Ph.D.*), 6 shahada ya uzamili, na 2 ni wa shahada ya kwanza. Aidha, watumishi 37 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi ili kujifunza zaidi ufuatiliaji na tathmini, uchambuzi wa sera, usimamizi/ukaguzi wa matumizi ya rasilimali fedha, udereva na ukatibu muhtasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ilitoa maagizo kwa utekelezaji. Maagizo hayo yalikuwa ni pamoja na:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kurekebisha Sheria ya Tume ya Mwaka 1989, katika mwaka 2011/2012, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango ilikamilisha utafiti kuhusu "Marekebishi ya Muundo wa Tume ya Mipango ili Uendane na Majukumu yake Mapya". Kutokana na utafiti huo, Tume imeandaa rasimu ya marekebishi ya Sheria Na. 11 ya mwaka 1989 iliyounda Tume ya Mipango katika kutekeleza maagizo ya Kamati ya Fedha na Uchumi. Rasimu hiyo kwa sasa inaendelea kujadiliwa na wadau mbalimbali ili kuitolea maoni ya kuiboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzisha Idara ya kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kazi ya kurekebisha muundo na kuanzisha idara iliyopendekezwa itafanyika sanjari na marekebishi ya Sheria Na. 11 ya mwaka 1989 iliyounda Tume ya Mipango ili kuwezesha muundo huo kukidhi mahitaji ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 - 2015/2016. Mwaka 2011/2012 ulikuwa ni mwaka wa mpito katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2011/2012 - 2015/2016, ambapo utaanza kutekelezwa rasmi kupitia Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/2013.

Katika mwaka 2011/2012, Tume imefanya tathmini ya jumla ya mafanikio na changamoto za utekelezaji wa miradi iliyokuwa inaendelea. Tathmini ya utekelezaji wa Mpango imeelezwa kwa kirefu katika sura ya pili ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/2013 ambao umekwisha jadiliwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa kutumia uzoefu wa nchi ya Malaysia, Tume ya Mipango imeanza kuandaa mfumo wa utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mpango wa maendeleo ambao utawasilishwa Serikalini kwa uamuzi katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano kati ya Tume na Wizara ya Fedha. Ushauri huo ulizingatiwa ipasavyo. Katika mwaka 2011/2012, Tume ya Mipango imeendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2012/2013, ambapo Tume ya Mipango ilikuwa na Wajumbe katika Kamati husika na kutoa Mwenyekiti Mwenza katika Kamati hiyo. Aidha, Wizara ya Fedha ilitoa wataalam wawili kwa muda wote kufanya kazi pamoja na Tume ya Mipango wakati wa maandalizi ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/2013 ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa miradi ya kimkakati na bajeti ya miradi hiyo. Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha kwa pamoja, pia wameandaa Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2011 na ipo dhamira ya dhati ya kukuza ushirikiano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwezesha na kujenga mazingira ya kuvutia watumishi wenye weledi. Ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi ulizingatiwa na unaendelea kufanyiwa kazi. Kazi ya kupitia muundo wa Tume na kuhuisha pale panapostahili inaendelea. Shughuli hii ya kuandaa mapendekezo ya kuhuisha muundo wa Tume inatarajiwa kuwasilishwa katika ngazi husika katika mwaka 2012/2013. Hata hivyo, kwa hivi sasa bado kuna changamoto kubwa ya kuendelea kujenga mazingira bora ya kuvutia wataalam wenye weledi na waliobobea na kuwapatia vitendea kazi kama vile kompyuta, vitabu, majarida, mafunzo, na fedha za kutosha kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango imefanya jitihada mbalimbali kwa madhumuni ya kujenga uwezo wa kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo na *International Poverty Reduction Centre of China (IPRCC)* na kukubaliana kushirikiana na wataalam wa taasisi hiyo katika kufanya tafiti mbalimbali na kutoa fursa za mafunzo kwa wataalam wa Tume ya Mipango nchini China. Makubaliano hayo yanatoa fursa nzuri kwa Tume ya Mipango kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kutumia uzoefu wa China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazungumzo pia yanaendelea na wahisani wengine kwa lengo la kuwashawishi wakubali kuchangia maeneo kadhaa ya Bajeti ya Tume ya Mipango, hususan kusaidia kujenga uwezo wa Tume na kupatiwa vitendea kazi kama vile vitabu, majarida mbalimbali, kompyuta, *printa* na

vifaa vya kufanya mikutano kwa njia ya video. Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) tayari limetenga Shilingi bilioni 2.1 katika bajeti ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2012/2013 kusaidia baadhi ya mahitaji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine za kitaalam zilizoteklezwa katika mwaka 2011/2012 ni pamoja na:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha ilikamilisha kazi ya kuandaa Mfumo wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2012/13. Mfumo huo uliridhiwa na Serikali na hatimaye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili 2012. Mfumo huo ndio uliotumika kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2012/2013.

Kamati ya Ushauri ya Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati (*National Strategic Investment Committee*), Kamati hii inaongozwa na Gavana wa Benki Kuu. Tume ya Mipango ni Sekretarieti ya kamati hiyo na inaundwa na wajumbe kutoka katika wizara na taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi. Wajumbe hawa waliteuliwa na Rais kwa kuzingatia weledi na taaluma zao katika kutekeleza majukumu ya kamati. Katika mwaka 2011/2012, Kamati hiyo ilifanya uchambuzi na kuishauri Serikali kuhusu miradi ya kitaifa ya kimkakati. Baadhi ya miradi hiyo imejumuishwa katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ubua wa Ukuaji Uchumi kati ya Tanzania na Marekani (*Partnership for Growth*). Katika hatua ya kwanza ya ushirikiano huo, ulifanyika uchambuzi wa kubaini vikwazo vikuu kwa ukuaji wa uchumi na uwekezaji wa sekta binafsi nchini Tanzania. Hatua ya pili ilihuisha kufanya uchambuzi wa kina wa vikwazo vikuu vitatu kwa ukuaji uchumi wa Tanzania na sababu zake. Vikwazo hivyo ni:-

(i) ukosefu wa umeme;

(ii) miundombinu duni ya barabara vijijini; na

(iii) upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa ndani na nje. Hatua ya tatu na ya mwisho inayoendelea ni kuandaa Mpango-kazi kwa ajili ya utekelezaji wa ubia wa kukuza uchumi kati ya Tanzania na Marekani (*Joint Country Action Plan (JCAP)*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano na Benki ya Dunia. Katika mwaka 2011/12, Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Benki ya Dunia iliendelea na kazi ya kuchambua aina ya viwanda ambavyo Tanzania inaweza kuvutia wawekezaji hususan kutoka China, India, Malaysia, Korea Kusini, na Vietnam, kazi hii ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji.

Mara baada ya kazi hiyo kukamilika na kuridhiwa na Serikali, Waheshimiwa Wabunge watapatiwa taarifa ya kazi hiyo ambayo tunaamini itasaidia kuongeza kasi ya maendeleo ya viwanda nchini na kupanua fursa za ajira.

Mheshimiwa Mwanyekiti, Ushirikiano na PEMANDU – Malaysia. Tume ya Mipango imeanza ushirikiano na Kitengo kinachoitwa *Performance Management and Delivery Unit (PEMANDU)* ambacho kipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu wa Malaysia ili kusaidia kutengeneza mfumo madhubuti wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika mazingira ya Tanzania kwa kutumia uzoefu wa Malaysia.

Mheshimiwa Mwanyekiti, Tume ya Mipango ilishiriki semina na mafunzo kuhusu mfumo huo mwezi Novemba 2011 huko Malaysia. Ujumbe wa Tanzania katika semina hiyo uliongozwa na Katibu Mtendaji-Tume ya Mipango, akiambatana na wataalam waandamizi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Sekretariat ya Baraza la Mawaziri, Wizara za Uchukuzi, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Nishati na Madini, na Tume ya Mipango Zanzibar.

Lengo la semina hiyo ilikuwa ni kujifunza mfumo unaotumiwa na *PEMANDU* katika ufuutiliaji na tathmini ya mipango ya maendeleo, mfumo ambao umeiwezesha Malaysia kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Kama sehemu ya ushirikiano kati ya *PEMANDU* na Tume ya Mipango, hivi sasa unaandalisha mkutano wa kazi wa Baraza la Mawaziri ambao unatarajiwani kufanyika hapa Dodoma tarehe 4-5 Agosti 2012 ili kuliwezesha Baraza la Mawaziri kujifunza na kuona namna mfumo huo wa Malaysia unavyoweza kutumika katika mazingira ya Tanzania, hususan ili kuimarisha

utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Dkt. Idris Jala, Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Afisa Mtendaji Mkuu wa *PEMANDU*, ataongoza jopo la watoa mada katika mukutano huo.

Mapendekazo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2012/2013. Baada ya maelezo ya utekelezaji kwa mwaka 2011/2012, sasa ningependa kuchukua fursa hii kuainisha kwa muhtasari maeneo ambayo Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango itayapa kipaumbele katika mwaka wa Fedha 2012/2013, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwanyekiti, Kurekebisha Sheria ya Tume ya Mwaka 1989. Katika mwaka 2012/2013, Tume ya Mipango itaendelea kuwashirikisha wadau katika kujadili rasimu ya mapendekazo ya marekebishi ya Sheria Na. 11 ya mwaka 1989 iliyounda Tume ya Mipango ili kuitolea maoni yatakayoboresha sheria husika. Marekebishi ya Sheria hiyo yatawasilishwa Bungeni Mwezi Novemba 2012 baada ya kuidhinishwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutayarisha Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2013/2014. Katika mwaka 2012/2013, Tume ya Mipango itaandaa Mfumo wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2013/2014.

Baada ya kuridhiwa na Bunge lako Tukufu katika kikao cha Bunge cha Mwezi Feburari 2013, Mfumo huo utatumika kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2013/2014, utakaojumuisha uchambuzi wa

kina wa mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/2013 na maeneo ya kimkakati ambayo yatapewa kipaumbele katika mwaka 2013/2014. Ufutiliaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2012/2013 na wa Miaka Mitano, 2011/2012 – 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango itafanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa 2012/2013, na mafanikio na changamoto za utekelezaji zitatumika katika kuandaa Mpango wa 2013/2014. Aidha, kwa kutumia uzoefu wa nchi ya Malaysia, Tume ya Mipango itaandaa mfumo wa ufutiliaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambao utawasilishwa Serikalini kwa uamuzi katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Kutangaza Dira ya Taifa 2025, Mpango Elekezi wa Miaka kumi na tano, na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza mwaka 2011/2012, Tume ya Mipango itajipanga upya katika kuitangaza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano. Nguvu zitaelekezwa katika kutumia vyombo vya habari ikiwemo Televisheni, tovuti, radio, simu na magazeti kuwafikishia ujumbe Watanzania wote na wadau wengine ili wajue nafasi yao katika kutekeleza Dira na Mpango wa Maendeleo. Aidha, kitabu cha Mpango Elekezi kitachapishwa na kusambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine kulingana na fedha/bajeti itakavyoruhusu.

Pamoja na hatua hizo, tayari Serikali imezitaka wizara zote kutayarisha mpango kazi wa utekelezaji wa Mpango Elekezi unaoonyesha malengo, viashiria vyatmafani, mahitaji ya rasilimali na ratiba ya utekelezaji kwa vipindi vyatmafani mitano, mwaka mmoja mmoja na kila robo mwaka. Kazi hii inatakiwa kuwa imekamilika mwisho wa mwezi Julai 2012. Mpango kazi wa kila Wizara ndiyo utakuwa msingi utakaotumiwa na Tume ya Mipango kufuatilia utekelezaji wa mipango ya Taifa.

Mheshimiwa Mwanyekiti, kuhusu Kuibua na kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwanyekiti, katika mwaka 2012/2013, msisitizo utawekwa katika kukamilisha tafiti zilizoanza kutekelezwa mwaka 2011/2012. Tafiti hizo zimetajwa katika aya ya 11 ya hotuba yangu. Aidha, Tume itaendelea kuibua tafiti nyingine zitakazotoa majibu ya kukabiliana na changamoto za kiuchumi na kijamii zinazowagusa Watanzania.

Mheshimiwa Mwanyekiti, katika mwaka 2012/2013, Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Kituo cha Kimataifa cha Ukuza *International Growth Centre (IGC)* itaandaa na kufanya kazi agenda ya pamoja ya utafiti. Moja ya maeneo yanayopendekezwa ni kufanya utafiti juu ya namna ambayo Tanzania itaweza kuijandaa kutumia vizuri fursa mbalimbali zitakazotokana na shughuli za utafutaji, uchimbaji na matumizi ya gesi-asili kukidhi mahitaji ya majumbani, viwandani na kuuza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya makubaliano ya ushirikiano kati ya Tume ya Mipango na Kituo cha Kimataifa cha Kupunguza Umaskini cha China (*International Poverty Reduction Center of China (IPRCC)*):-

- (i) kitaanzishwa kituo cha IPRCC hapa nchini ambacho pia kitahudumia nchi zote za Afrika Mashariki;
- (ii) Kutafanyika warsha na mafunzo kwa ajili ya kujenga uwezo wa vijana na wanataluma wa Kitanzania katika nyanja za maendeleo vijiji na kupunguza umasikini.Hii itakuwa pamoja na Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano wa tatu wa Baraza la China-Africa (*Third China-Africa Poverty Reduction and Development Forum*), ambao utafanyika Dar-es-Salaam tarehe 28 Julai, 2012. Dhana ya mkutano huo ni "Kilimo cha Kisasa kwa ajili ya Kupunguza Umasikini";
- (iii) Tume ya Mipango na IPRCC watashirikiana kufanya utafiti kuhusu changamoto mbalimbali za kiuchumi na kijamii;
- (iv) Zitafanyika ziara za mafunzo China na hapa nchini; na
- (v) Utatekelezwa mradi wa kijiji cha mfano (Peapea, Wilaya ya Kilosa) kuwawezesha wananchi kujifunza kwa vitendo mbinu zinazotumiwa na wakulima huko China kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuratibu Kamati ya Ushauri ya Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati. Katika mwaka 2012/2013, Kamati ya Ushauri ya miradi ya kitaifa ya kimkakati itaendelea kufanya uchambuzi na kuishauri Serikali kuhusu miradi ya kitaifa ya kimkakati itakayojumuishwa katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kuratibu Ubia wa Ukuzaji Uchumi kati ya Tanzania na Marekani (*Partnership for Growth*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea na hatua ya tatu ya ushirikiano ya kukamilisha Mpango-kazi kwa ajili ya utekelezaji wa ubia wa kukuza uchumi kati ya Tanzania na Marekani (*Joint Country Action Plan (JCAP)*) na kuanza utekelezaji wake baada ya kuridhiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuratibu Ushirikiano na Benki ya Dunia. Katika mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea kukamilisha kazi ya kuchambua aina ya viwanda ambavyo Tanzania inaweza kuvutia wawekezaji hususan kutoka China, Korea Kusini, India, Malaysia na Vietnam. Mara baada ya kazi hiyo kukamilika na kuridhiwa na Serikali, Bunge litapatiwa taarifa ya kazi hiyo kupitia Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuratibu Ushirikiano na PEMANDU – Malaysia. Tume ya Mipango itaendelea kuratibu ushirikiano kati ya Serikali na PEMANDU (Performance Management and Delivery Unit) ambapo katika mwaka 2012/13, itaandaliwa warsha ya Baraza la Mawaziri ili kujenga uelewa wa pamoja na

ukubali (buy-in) wa mfumo wa ufuatiliaji unaotumika nchini Malaysia chini ya uratibu wa *PEMANDU*. Mfumo huo utatekelezwa kwa kuzingatia mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuendelea kujenga uwezo wa Tume ya Mipango. Katika mwaka 2012/13, Tume ya Mipango itaendelea kujenga uwezo wa Tume kwa kuajiri watumishi wapya 21 na kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi 51. Aidha, Tume itaendelea kujenga mazingira bora ya kuvutia wataalam wenye weledi na waliobobea na kuapatia vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sensa ya Watu na Makazi 2012. Kabla ya kuhitimisha naomba uniruhusu kusitiza umuhimu wa kila mwananchi kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika tarehe 26 Agosti mwaka 2012 chini ya kaulimbiu "*Sensa kwa Maendeleo: Jiandae Kuhesabiwa*". Zoezi la Sensa ni muhimu kwa ajili ya kuwa na mipango mizuri ya maendeleo katika nchi yetu. Hakuna mipango mizuri bila ya kuwa na takwimu sahihi na za kuaminika. Takwimu za Sensa zinatumika katika kuandaa mipango ya maendeleo na kupima hali ya maisha ya watu katika ngazi ya taifa, mkoa, wilaya hadi ngazi ya kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sensa ya mwaka 2012 inatarajiwa kutupatia picha halisi ya taarifa muhimu kwa maendeleo ikijumuisha takwimu za umri; jinsia; hali ya elimu, afya, na upatikanaji wa maji; uraia; ulemavu na aina ya ulemavu; uhamiaji; na watu wanaoishi ughaibuni (*diaspora*). Aidha, taarifa za kiuchumi zitajumuisha takwimu za uzalishaji kama vile kilimo (mazao, mifugo, uvuvi), na idadi ya kaya husika;

viwanda vidogo; shughuli nyingine za uzalishaji mali; biashara; na mapato na matumizi ya kaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya Sensa yanaendelea vizuri na kazi muhimu ya kutenga maeneo imekamilika pamoja na kuanza mafunzo katika ngazi ya kitaifa kwa wakufunzi ambao watatoa mafunzo kwa wadadasi (enumerators) katika ngazi ya mikoa na wilaya. Aidha, kazi zinazoendelea kwa sasa ni pamoja na kuhamasisha Watanzania kushiriki kikamilifu katika zoezi hii, usafirishaji wa vifaa vyta Sensa kwenda mikoani na ukamilishaji wa kituo cha kupokea taarifa za Sensa (*Data Centre*) kilichopo Kibaha mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini na maombi yangu kwa Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Serikali na Dini, na vyombo vyta habari kuwa mabalozi wazuri katika kuhamasisha na kuwahimiza wananchi wajiandae na washiriki kikamilifu katika kuhesabiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha mapendekezo ya bajeti ya Shilingi Bilioni Nane, Milioni Saba, Elfu Hamsini na Sita tu (8,007,056,000/=). Mchanganuo wa Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida (*Reccurent Budget*) ni Shilingi Bilioni Tano, Mia Nane Themanini na Mbili Milioni, Mia Tatu Ishirini na Tatu Elfu tu (5,882,323,000/=), kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Moja, Mia Nne Kumi na Sita Milioni, Mia Tano Kumi na Nne Elfu tu (1,416,514,000=) ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi Bilioni Nne, Mia Nne Sitini na Tano

Milioni, Mia Nane na Tisa Elfu tu (4,465,809,000/=) ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (*OC*) ikiwa ni pamoja na kugharamia tafiti; na

(ii) Bajeti ya Maendeleo ni Shilingi Bilioni Mbili, Mia Moja Ishirini na Nne Milioni, Mia Saba Thelathini na Tatu Elfu tu (2,124,733,000/=) ambapo zote ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue tena nafasi hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha kwa niaba ya kaka yangu Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, ambaye ndiyo Waziri anayehusika Wizara ya Mahusiano na Uratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Mkuchika, Waziri mwenye dhamana ya Utawala Bora. Kwa niaba ya Mheshimiwa Stephen Wasira. Umewasilisha Hotuba ya Makadirio ya Bajeti kwa ajili ya Wizara yake anayoisimamia.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono kwa mujibu wa Kanuni na basi mara baada ya hoja hiyo kutolewa na kuungwa mkono tunaendelea na hatua inayofuata na sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi.

Waheshimiwa Wabunge Wizara hii kama mlivyosikia pamoja na kusomwa Hotuba za Mawaziri,

Kamati zilivochambua Mapendekezo ya Wizara hii ni mbili. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kwa sababu ya Hoja ya Mipango Kamati ya Fedha na Uchumi pia ilihusika katika kuchambua hotuba hii. Baada ya hapo nitakuja na Msemaji wa Kambi ya Upinzani leo nilitaka kumpa *priority* lakini kwa mujibu wa Kanuni yeye atafuata baada ya kuwasikia hao.

Kwa hiyo, tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, atafuatiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi na baada ya hapo tutakwenda kwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Nitaomba anilitee hapo mwongozo kama alivyowasilisha hati kwa maeno yote mawili yeye mwenyewe pake yake. Sasa tutapenda pia meza yangu ifahamu kama hotuba yake inaunganisha Wizara zote mbili ili tujue tunaugawaje muda wetu. Kwa hiyo, naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na itawasilishwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mbunge mzoefu, Mheshimiwa John Paul Lwanji. (*Makof!*)

MHE. JOHN P. LWANJI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Mwanyekiti, nakushukuru kwa maneno mazuri. Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru wananchi wangu wa Manyoni Magharibi kwa kuniamini tena kwa mara nyingine kuwawakilisha katika jengo hili na pia bila kuisahau familia ambayo imekuwa karibu nami katika kufanya kazi hii ngumu ya kuwawakilisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni Na 99(7) na 114(11), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako

Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwanyekiti, Ofisi ya Rais inahusisha Mafungu Saba, Fungu 20 – Ofisi ya Rais (Ikulu); Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Fungu 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma na Fungu 9 – Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwanyekiti, katika kutekeleza majukumu yake tarehe 5 Juni, 2012, Kamati ilikutana Dar es Salaam, kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais. Katika kikao hicho Kamati ilipokea maelezo ya Serikali Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, kwa Mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Celina Kombani,(Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwanyekiti, miongoni mwa mambo ambayo Kamati ilielezwa ni kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais (Ikulu) na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, pamoja na Taasisi zilizo chini ya

Ofisi ya Rais. Mtoa hoja alieleza pia kuhusu Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Kipindi cha Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwanyekiti, utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa Mwaka 2010/2011. Wakati wa Kuchambua Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka 2011/2012, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa na kufanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

Serikali ichukue hatua za haraka ili kuondoa tatizo la Watumishi wa Umma kutobadilika kifikira (*change of mindset*) ili kuleta ufanisi. Kamati ilielezwa kuwa Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa Watumishi wa Umma wanatekeleza wajibu wao kwa bidii na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, na taratibu zilizowekwa, kama ilivyoainishwa katika Awamu ya Pili ya Program ya uboreshaji katika Utumishi wa Umma (*PSRP II*).

Serikali iongoze Bajeti zaidi kwa TAKUKURU ili iweze kufanya shughuli zake Kisayansi zaidi kuliko hivi sasa. Kamati ilielezwa kuwa katika Mwaka 2011/2012 Serikali iliongeza Bajeti ya TAKUKURU kutoka Sh.47.6 billion hadi Sh. 51.9 bilioni sawa na ongezeko la 9%. Aidha, Mwaka wa Fedha 2012/13 Bajeti ya TAKUKURU ni Tsh. 54.1 bilioni ambazo ni ongezeko la 4%. Kati ya hizo, Sh.1.1bilioni ni fedha toka kwa Wadau wa Maendeleo (*UNDP na DFID*).

TAKUKURU ifanye Utafiti zaidi na kuishauri Serikali kuhusu mianya ya rushwa, hasa rushwa kubwa kwenye

Madini, Maliasili na kwenye Mikataba ambayo Serikali imekuwa inapata hasara na kulikosesha Taifa Mapato. Kamati ilielezwa kwamba moja ya majukumu ya TAKUKURU kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007 ni kufanya utafiti juu ya masuala ya rushwa. Aidha, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (*PPRA*) TAKUKURU inakamilisha taratibu za Zabuni kwa ajili ya kupata Mshauri Mwelekezi wa Utafiti unaotegemewa kukamilika mwaka wa fedha 2012/2013.

Serikali isambaze mpango wa MKURABITA kwa nchi nzima kuliko inavyofanyika hivi sasa ambapo Wilaya huchaguliwa kwa kutumia vigezo vilivyofanyiwa tathmini.

Kamati ilielezwa kuwa nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba utekelezaji wa MKURABITA unafanyika nchi nzima badala ya kutumia vigezo kama ilivyo sasa. Matumizi ya vigezo yametokana na ukosefu wa fedha. Ili kukabiliana na tatizo hilo, mpango mkakati wa miaka mitano umeandaliwa ili kuiwezesha MKURABITA kutafuta fedha nje ya Bajeti ya Serikali.

Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, iwezeshe kukamilishwa kwa Masijala za Ardhi za Vijiji na hivyo kuwawezesha wananchi kupata Hati Miliki zitakazotumika kama dhamana ya kupata Mikopo kwenye Mabenki. Kamati ilielezwa kwamba Masijala ya Ardhi ya Kijiji ni Sehemu ya Ofisi ya Kijiji na hivyo ujenzi wa Ofisi ya Kijiji ni jukumu la Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeendelea kuhimiza Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba ujenzi wa Ofisi

za Vijiji unakamilika. Masijala hizi zitawezesha Wananchi kupata Hati Miliki zitakazotumika kama dhamana katika kupata mikopo.

Mgongano wa Sheria unaosababisha upungufu katika Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114, na Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya 2007 ambazo ni mionganini mwa Sheria zinazotumika katika kusimamia Sekta ya Ardhi nchini.

Kamati ilielezwa kwamba maandalizi ya maboresho ya Sheria ya Ardhi na Biashara yalikamilika Mwaka 2008 na kuwasilishwa katika Wizara za Kisekta ambazo ni Wizara za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Viwanda na Biashara, na TAMISEMI. Vikosi kazi viliundwa vikijumuisha MKURABITA pamoja na Wizara ya Kisekta ili kuchambua kwa undani maboresho haya. Kikosi kazi kilichoundwa kati ya MKURABITA na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuchambua na kupendekeza mabadiliko ya Sheria Ardhi, Sura ya 113, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Sura ya 114 na Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya 2007 kimekamilisha kazi na kutoa Taarifa yake.

Mapendekezo yanayohusu Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 na yale ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura 114, yanaendelea na mchakato wa Maandalizi ya Muswada. Aidha, mapendekezo yanayohusu Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya 2007 yameandaliwa Muswada wa Sheria unaoitwa "*The Business Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2011*, Sehemu ya VI, Kipengele cha 43 -77. Muswada huu umepitishwa na Bunge la Mwezi Aprili, 2012.

Serikali iweke Vivutio maalum kwa kada mbalimbali ili kuimarisha maadili ya Watumishi wa Umma na kupambana na tatizo la rushwa na kuvujisha siri za Serikali. Kamati ilielezwa kuwa Serikali imeandaa mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Malipo ya Mshahara na motisha katika Utumishi wa Umma (2010) ambapo suala la kuweka vivutio maalum ili kuimarisha masilahi ya Watumishi wa Umma ni sehemu ya utekelezaji wa sera.

Mheshimiwa Mwenyeki, Serikali ifuatilie utendaji kazi wa Watumishi wa Umma wasiowajibika. Kamati ilielezwa kwamba Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 ya Mwaka 2002, Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2003 na Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma za Mwaka 2003 zimewapa Waajiri mamlaka juu ya Watumishi wao likiwemo suala la kusimamia Utendaji wa kazi zao za kila siku. Waajiri wana Mamlaka ya kuwapangia kazi Watumishi na kutathmini Utendaji wao kwa kutumia utaratibu wa upimaji wa Utendaji kazi wa Wazi (*OPRAS*). Aidha, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kwa Watumishi wasiowajibika. Hadi kufikia Mwezi Machi 20121 kulikuwa na Watumishi 287 waliochukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na Watumishi 111 walifukuzwa kazi, watumishi 28 walirejeshwa kazini na Watumishi 146 mashauri yao bado yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema maslahi ya Watumishi yakaangaliwa upya kwa kuoanisha hali ya maisha ya sasa ili kuwapunguzia makali ya maisha Watumishi wa Serikali na kuongeza uwajibikaji zaidi.

Kamati ilielezwa kwamba Serikali imeendelea kuboresha Mishahara ya Watumishi wa Umma kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi wa nchi na uwezo wa Bajeti ya Serikali. Katika kipindi cha Miaka Mitano tangu 2007/2008 kima cha chini cha mshahara kimeongezeka kwa asilimia 86 kutoka Sh.80,760 hadi 150,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondokana na gharama kubwa za ukodishaji na ukarabati wa majengo, Wizara/Taasisi ambazo hazina majengo yao, kwanza zifanye jitihada za kupata Viwanja Dar es salaam na Dodoma ambapo ni Makao Makuu ya Nchi. Kamati ilielezwa kwamba Serikali imeanza juhudi za kutambua mahitaji ya Ofisi kwa ajili ya Wizara na Idara zinazojitegemea zote katika Mji wa Serikali wa Dodoma. Kwa kuanzia, Serikali inafanya mchanganuo wa kupata mahitaji halisi ya Watumishi katika Wizara na Idara zinazojitegemea kulingana na ngazi na Vyeo vyta Watumishi. Lengo ni kupata mahitaji halisi na Ukubwa na aina za Ofisi zinazohitajika kwenye Mji wa Serikali wa Dodoma. Aidha, kibali kwa ajili ya Kujenga jengo la Ofisi ambalo litatumwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Umma, Sekretariati ya ajira katika Utumishi wa Umma, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma, na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kimepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie suala la utoaji wa vibali vyta ajira mapema kwani linachelewesha maendeleo kwa kukosa rasilimali watu ambao ni muhimu sana.

Kamati ilielezwa kwamba suala la utoaji wa vibali linazingatia uwezo wa Serikali kifedha na kipaumbele kimewekwa katika ajira za Kada muhimu zaidi kama vile Afya, Elimu, Mifugo na Kilimo. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya wahusika kuchelewa kuwasilisha maombi ya vibali. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 Serikali imeshatoa nafasi ya ajira mpya 47,1642 kama ifuatavyo:- Wizara ya Elimu (Walimu wa Sekondari) nafasi 13,636, Wizara ya Elimu (Walimu wa Shule za Msingi) nafasi 11,379, Sekta ya Afya nafasi 9,391, Sekta ya Kilimo nafasi 4,400, Sekta ya Mifugo nafasi 1,090 na Watumishi wengine nafasi 7,152.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali irudishe Mfumo wa Vijana, kuhudhuria mafunzo ya JKT pindi wamalizapo Elimu ya Sekondari au Vyuo. Hii ni pamoja na kuingiza somo la Uzalendo katika Mitaala ya Elimu ya Msingi na Sekondari hadi Vyuo Vikuu.

Kamati ilielezwa kwamba Serikali imetua uamuzi wa kurudisha Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mujibu wa Sheria na Taratibu za kudahili Vijana wa kujitolea zimeanza. Aidha, mkakati wa kuboresha Mtaala wa Uraia kwa kufundisha somo la Maadili na Uzalendo mashuleni unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za haraka zichukuliwe ili kufungua Ofisi za Sekretariat ya ajira Mikoani na kwenye Kanda ikiwa ni pamoja na kuwapata Watumishi wenyewe sifa Kamati ilielezwa kwamba katika Mwaka wa Fedha 2011/2012, Sekretariati ya ajira imefanikiwa kupata Ofisi katika Mikoa ya Morogoro, Tabora, Mwanza, Mbeya, Manyara na Mtwara. Hata hivyo, Ofisi hizi hazijaanza

kufanya kazi kutokana na ufinyu wa Bajeti. Sekretariati ya ajira imeendelea kufanya usaili katika Mikoa ya Tanzania Bara pamoja na Zanzibar ili kuwapunguzia gharama waombaji wa kazi wanaotoka maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Ajira iachie jukumu la kuajiri Watumishi wa Kada ya Uhudumu na Madereva kwenye Mamlaka husika. Kamati ilielezwa kwamba suala hili limekubaliwa na hatua za kurekebisha Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya Mwaka 2002 katika kuzingatia suala hili linafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti maoni, maagizo na mapendekezo ya kamati napenda kutoa Maoni, Maagizo na Ushauri kwa Ofisi ya Rais kama ifuatavyo:- Katika Ofisi ya Rais, menejimenti ya utumishi wa umma pamoja na taarifa ya Serikali kwamba inaendelea kuboresha Mishahara ya Watumishi wa Umma, bado ipo haja ya kufanya juhudzi zaidi ili Serikali ioanishe masilahi ya Watumishi wa Umma na gharama za maisha zilivyo kwa hivi sasa. Ni ukweli usiopingika kwamba gharama za Maisha zimezidi kuongezeka na hivyo kufanya watu hasa wa kipato cha chini kuathirika na kuumia zaidi. Kamati inaiomba Serikali kufanya utafiti wa sababu za kupanda kwa gharama hizi za maisha na kisha kutafuta ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kulipa madeni ya Watumishi wa Umma ambapo ilielezwa kwamba madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa Umma 48,006 yenye thamani ya Sh.49,341,313,554.07

yamelipwa na madai ya watumishi 1,353 yenye thamani ya Sh.1,665,872,789.81 yamekwisha ingizwa kwenye mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimali Watu (*Human Capital Management Information System-HCMIS*). Hata hivyo bado kumekuwepo na malalamiko mengi ya Watumishi kuhamishwa vituo vyao vya kazi pasipo kuzingatia utaratibu na hivyo kuzalisha madeni mengi zaidi. Kamati inaagiza waajiri wote kuhakikisha kuwa Serikali haiendelei kuwa na madeni kwa kufuata maelekezo yaliyotolewa kupitia Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2009 ili kudhibiti ongezeko la madeni ya Serikali kwa Watumishi wa Umma. Aidha, Kamati inaagiza Serikali kutoa ufanuzi wa madai ya watumishi 8,134 yenye thamani ya Sh. 8,262,967,665.92 yanayoendelea kuhakikiwa yatalipwa lini na fedha hizo ziko katika mafungu gani ya bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya uzalishaji wa madeni ya Serikali kwa Watumishi wa Umma ni ajira mpya, ambapo Watumishi wapya hukaa kwa muda mrefu pasipo kulipwa Mishahara na Mafao yao mengine kutokana na sababu zinazoelezwa kwamba mipango na taratibu za ajira yao zinakuwa zinatayarishwa. Katika zama hizi za sayansi na teknolojia Kamati haikubaliani na sababu za aina hii, hivyo tunaishauri Serikali kuanzisha utaratibu ambao mara tu mtu anapopata ajira, taarifa inatoka mara moja na hivyo mshahara na mafao mengine ya Mwajiriwa huyo mpya yanaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefurahishwa na Taarifa ya Serikali kwamba imeanza juhudzi za

kutambua mahitaji ya Ofisi kwa ajili ya Wizara na Idara zote zinazojitegemea katika Mji Mkuu wa Serikali Dodoma. Hata hivyo, pamoja na taarifa hiyo, bado Kamati haioni juhudini yoyote inayofanywa na Serikali kuhamia Dodoma. Pia, Kamati inapenda kupata ufanuzi ni kwa nini Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma haijatengewa fedha za ndani kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa na Taarifa kwamba bado kuna Watumishi wa Umma wanajihuisha na Siasa Makazini na hivyo kuchukua muda mwangi na hata kutumia magari ya Serikali kwenye Mambo ya Siasa huku wakiacha kutekeleza majukumu yao. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua kali dhidi ya Watumishi hawa. Aidha, Kamati inatoa rai kwa Watumishi wote wa Umma kufuata Sheria na Kanuni za Ajira zao ili kuleta tija sehemu zao za kazi, na kwa wale watumishi wanaodhani siasa ni sehemu ya majukumu na taaluma zao, ni vema wakajiondoa kwenye Utumishi wa Umma ili waweze kutekeleza jukumu la kufanya siasa pasipo vipingamizi vyovyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma, Kamati iliwahi kutoa tamko la kuunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, la kutaka Mfumo wa kutenganisha Biashara na Uongozi. Mfumo huo ambao unaweka dhana ya uwajibikaji pasipo vikwazo vya maslahi binafsi ni muhimu kwa ustawi wa Jamii yetu. Kamati inapenda kupata ufanuzi ni kwa kiasi gani dhana hiyo ya kutenganisha Uongozi na Biashara imetekelizwa hadi sasa. Umekuwepo mtindo

wa kuhamisha Watumishi pindi wanapokumbwa na kashfa au tuhuma za ubadhilifu katika eneo lingine. Hali hii imekuwa inasababisha ubadhilifu kuendelea maeneo ambayo Watumishi hao wanahamishiwa. Kamati inaagiza Serikali kuchukua hatua za Kisheria na Kinidhamu mara moja kwa Watumishi wote wanaovunja Sheria na Kanuni za ajira zao na siyo kuwahamishia maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutembelea maeneo mbalimbali ya Wizara na Idara zinazojitegemea, Kamati imegundua kwamba bado kuna Watumishi wa Idara mbalimbali ambao wanakaimu nafasi mbalimbali. Kamati inaishauri Serikali ifanye mipango ya kuwapa Madaraka Kamili au kutafuta Watumishi wanaoweza kushika nafasi hizo kwani kukaimu kwa muda mrefu kunapunguza tija katika maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua mabadiliko ya Baraza la Mawaziri Mwezi Mei, 2012. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu ambao ni endelevu wa kupima utendaji wa Viongozi na Watendaji wa Serikali (*Performance Contract*) utakaoendelezwa hadi Uongozi wa ngazi za chini. Aidha, Kamati inashauri na kusisitiza kuwa hatua zaidi zinatakiwa kuchukuliwa kwa Watendaji wa Umma waliotajwa kwenye Ripoti ya Mkaguzi na mdhibiti Mkuu wa Serikali kwamba wamehusika kwa njia moja au nyingine kutenda, au kuzembea kutenda mambo ambayo yalisababisha hasara kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekretariati ya ajira katika utumishi wa umma - fungu 67 Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri wa Kamati wa kuachia jukumu la kuajiri Watumishi wa Kada ya Uhudumu na Madereva ili jukumu hilo lilekelezwe na Mamlaka husika. Hata hivyo, kwa kuwa jukumu hili limekuwa likitekelezwa kisheria, ni vema Serikali ikaleta Bungeni mapema iwezekanavyo sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya Mwaka 2002 ili ifanyiwe marekebisho na hivyo kuwezesha Mamlaka hizo kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefurahishwa na Taarifa za Serikali kwamba imeanzisha mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimali Watu (*Human Capital Management Information System-HCMIS*) kwa lengo la kuwa na kumbukumbu muhimu za Rasilimali Watu ikiwa ni ushauri uliotolewa na Kamati yangu kwa Mwaka jana. Kamati inashauri Serikali kutumia vyema mfumo huo kwani utarahisisha kupata takwimu za Watumishi waliopo, walioachishwa kazi, walioacha kazi na waliofukuzwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Sekretariati hii inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti kwani kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali iliidhinishia jumla ya Sh.2,939,650,000 kama matumizi ya kawaida na hadi kufikia Mei 31,2012 ni kiasi cha Sh.1,610,088,636 tu zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kwa mwaka 2012/2013 jumla ya Sh. 2,494,524,000 zimetengwa. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaiwezesha Sekretariati hii bajeti ya kutosha ili iweze kukamilisha malengo yake kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi ya Rais, mahusiano na uratibu. MKURABITA (Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za wanyonge Tanzania) Mpango wa MKURABITA ulianzishwa kwa lengo la kuwasaidia wananchi hasa wa hali ya chini ili kuwezesha mali walizonazo kuwa na thamani. Iwapo Mpango huu utatekelezwa kwa kadri ulivyo kusudiwa, itakuwa ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wanyonge kwani wataweza kutumia rasirimali zao kama dhamana dhidi ya mahitaji yao ya kijamii. Kamati inaiomba Serikali kuhakikisha inatenga bajeti ya kutosha ili mpango huu uweze kutekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inazidi kusisitiza Serikali kusambaza mpango wa MKURABITA kwa nchi nzima ikiwa ni pamoja na kukamilisha mpango mkakati wake wa miaka mitano ili kuiwezesha MKURABITA kutafuta fedha nje ya Bajeti ya Serikali. Hii itasaidia hasa Wananchi ambao wamekuwa wanashindwa kuaminika kwa kutokuwa na kitu chochocte kutumia ardhi yao kama dhamana kwa shughuli za Kibenki, Mikopo na mahitaji mengine ya Kijamii. Aidha, Serikali iharakishe uanzishwaji wa Benki ya Kilimo na kuimarisha Benki ya Akina Mama ambazo ni Benki za Wananchi zinazoweza kukubali hata dhamana za Hati za Kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuitia Mamlaka ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwamba kila kunapoanzishwa Kijiji, ni vema ikaanzishwa Masjala ya ardhi kama sehemu ya Ofisi ya Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa utekelezaji wa MKURABITA bado umeendelea kuwa mgumu kutokana na mgongano wa Sheria unaosababisha mapungufu mengi, Kamati inazidi kuhimiza Serikali kuharakisha na hivyo kuleta Bungeni Sheria ya Ardhi, Sura 113, na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura 114 ili ziweze kufanyiwa marekebisho ikiwa ni pamoja na kusambaza mpango wa MKURABITA kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko wa rais wa kujitegemea (*PTF*). Madhumuni la kuanzishwa kwa Mfuko huu ni kusaidia jitihada za serikali za kuwakwamua watu wa hali ya chini kwa kuwawezesha kupata mitaji ya kuanzisha na kuendeleza miradi na shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuongeza kipato na ajira kwa madhumuni ya kupunguza umasikini na kuongeza uzalishaji katika nyanja mbalimbali za kiuchumi Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wajasiriamali wadogo na wa kati Mijini na Vijijini ambao ni wadau wa mfuko huu kwamba mfuko bado unatoza riba kubwa kwa Wanachama wake. Kamati inaamini lengo la mfuko huu ambalo ni kuwahamasisha wananchi hasa vijana na wanawake wanaopenda na kuthamini kuendesha miradi ya kujiletea na kuongeza vipato vyao kwa njia za kujiajiri na hatimaye kujitegemea, halijafikiwa. Kamati inazidi kuihimiza Serikali kujitahidi kusambaza huduma za mfuko huu kwa nchi nzima na kutafuta vyanzo vyao Mtaji wenye masharti nafuu, pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji ili kupunguza tatizo la riba kubwa ya 10% kwa wanachama wake. Aidha,

Kamati inaiagiza Serikali kutoa ufanuzi wa utekelezaji wa Mikopo ya Uwezeshaji au maarufu kama Mabilioni ya JK ambayo ni moja ya shughuli za Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TASAF. Kamati inaamini kwamba malengo ya TASAF II hayajafanikiwa kwani bado inakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo maombi mengi ya miradi ya jamii yenyeye thamani kubwa kuliko uwezo wa TASAF II. Aidha, Kamati ilibaini tatizo la baadhi ya wanasiasa kuzuia jamii kuchangia miradi wanayoibua hivyo kukiuka dhana ya ushirikishaji jamii na umiliki wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuna tatizo la baadhi ya Halmashauri za Wilaya kutozingatia taratibu za matumizi ya fedha za miradi. Kamati inaamini kwamba utendaji huu usioridhisha wa TASAF unatokana na shughuli za TASAF kuhamishiwa kwenye Halmashauri wakati Serikali haijawaandaa Wananchi na watumishi hivyo kuleta uwajibikaji hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile hivi sasa TASAF III inategemea kuanza, Kamati inashauri mipango madhubuti iandaliwe kwa ajili ya utekelezaji wa TASAF III ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa utekelezaji wa shughuli za TASAF III unakuwa chini ya usimamizi wa TASAF wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala Bora. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuijunga na Mpango wa Kimataifa wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (*Open Government Partnership (OGP)*). Aidha, Kamati imefuatilia kwa makini utendaji wa Serikali na

kugundua kwamba upo uwezekano wa kuunganisha baadhi ya Wizara na Idara ili kupunguza ukubwa wa Serikali na hivyo kuleta ufanisi na kupunguza gharama kubwa za uendeshaji wa Serikali kama ilivyo kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya Mawaziri 30, Manaibu Waziri 25, Makatibu Wakuu 26 na Manaibu Katibu Wakuu 26 ni kubwa mno kwa nchi inayoendelea kama yetu. Kamati inashauri kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza kwa kuunganisha baadhi ya Wizara na Idara zinazoshabihiana bila kuathiri utendaji wa shughuli za Serikali. Aidha, Kamati inapendekeza nadharia (*concept*) ya “*Peter Principle*”. (*Never promote somebody to his/her highest level of incompetence*) kutumika wakati wa uteuzi wa Viongozi wa ngazi za juu wa Serikali. Kamati inakubaliana na nadharia hiyo kwa imani kwamba tunapozungumzia uwezo wa mtu kumudu majukumu yake tuisahau kwamba uwezo huo una ukomo kutokana na uwezo wa kiakili (*IQ*), sifa na uzoefu. Hivyo mamlaka ikikosea na kumteua mtu kushika madaraka asiyositahili, ni wazi kwamba mhusika atashindwa kumudu Madaraka aliopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Secretarieti ya Maadili ya Uongozi wa Umma. Kamati inapenda kurejea ushauri wake ilioutoa Mwaka jana, kwamba ni vema Serikali ikafikiria kurekebisha Sheria na Kanuni za Sekretarieti ya Viongozi wa Umma ili iweze kufanya kazi Kisayansi zaidi na ikibidi kuweka utaratibu wa kuwabana Watumishi wengine wa umma ambao sio Viongozi. Aidha, Kamati inashauri Sekretariati ifikirie uwezekano wa

kuweka taarifa za mali za Viongozi wazi kwa umma kwenye mitandao kama wanavyofanya kwa nchi nyingine kama vile Kanada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 kiasi cha Sh.3,507,991,172 ziliidhinishwa kwa ajili ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambapo Sh.2,597,991,172 zilikuwa fedha za matumizi ya kawaida, na Sh.910,000,000 zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi Mwezi Mei, 2012 jumla ya Sh.2,526,559,541 zilikuwa zimepokelewa wakati fedha za maendeleo zilikuwa bado hazijapokelewa. Kwa Mwaka 2012/2013 Sekretariati imeidhinishiwa kiasi cha Sh.7,390,691,600 ambapo Sh.5,923,436,600 ni Fedha za Matumizi ya Kawaida na Sh.1,467,255,000 ni fedha za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti zaidi kwa ajili ya Sekretariati hii ikiwa ni pamoja na kuimarisha Ofisi za Kanda ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi kuliko hivi sasa ambapo Sekretariati inafanyia shughuli zake kwa kutumia Ofisi ya Makao Makuu Dar es Salaam tu na hivyo kutotekeleza majukumu yake ipaswavyo kama inavyojidhirisha kwa mfano Mwaka 2011 Sekretariati iliweza kushughulikia mashauri 23 tu ya Viongozi wote walioshindwa kutekeleza Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, kwa Mwaka 2011 ni Madiwani 1,032 tu waliotekeleza Sheria ya Sekretariati na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya Madiwani 1,844 ambao hawakutekeleza Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU. Kamati inatambua kazi inayofanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Hata hivyo, Kamati inaamini kwamba Taasisi hii inawajibika kufanya zaidi ya ilivyo kwa sasa ili kuziba mianya ya rushwa ambayo kwa kiasi kikubwa inaliingizia Taifa hasara kubwa pamoja na kupoteza Mapato.

Kamati inaielekeza Serikali kufuatilia kwa karibu maeneo yote yenye harufu na yanayotajwa kujihusisha na rushwa na pale inapothibitika kuwepo na ushaidi hata wa mazingira, sheria ichukue mkondo wake na watuhumiwa kufikishwa kwenye Vyombo vyá Sheria. Aidha, Kamati inashauri Serikali kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa Wafanyakazi wa Taasisi hii ili kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi na hivyo, kupunguza uwiano wa kesi zilizoshindwa Mahakamani dhidi ya kesi zilizoshinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kwamba maeneo kama vile Mikataba ya Maliasili, Madini pamoja na kwenye Manunuzi ya Umma ndiko kwenye mianya mingi ya rushwa na kusababisha Taifa kukosa mapato huku tukiendelea kuwategemezi bila sababu yoyote.

Kamati inashauri TAKUKURU kwa kushirikiana na PPRA kukamilisha mapema taratibu za Zabuni kwa ajili ya kupata mshauri mwelekezi na utafiti katika miundombinu ya Barabara, Sekta ya Maliasili na Madini na kuchukua hatua za kisheria kwa yejote anayeonekana kujihusisha na vitendo vyá rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Misamaha ya kodi ni moja ya maeneo ambayo yamekuwa yakilalamikiwa kuhusika na vitendo vya Rushwa. Kamati inaagiza Serikali hususan Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kufuatilia undani wa misamaha hiyo ili palipo na mwanya wa rushwa paweza kuzibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho. kwa kuhitimisha, napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha Maoni ya Kamati yangu. Aidha, tunakupongeza kwa busara zako katika kuliongoza Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru kwa dhati, Mheshimiwa Celina Kombani, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Mb, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Idara, Vitengo na Maafisa wote, kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano walioutoa wakati wote Kamati tulipochambua Makadirio ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Wabunge wote wanaonisikiliza na kipekee Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka 2012/2013. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu Sekta za Sheria, Utawala, Haki za Binadamu na

Utawala Bora, umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa John Paul Lwanji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wengine wa Kamati ni Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Mohamed S. Mohamed, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Fakharia K. Shomar, Mheshimiwa Zahra A. Hamadi, Mheshimiwa Mussa H. Kombo na Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali.

Wengine ni Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Azza H. Hamad, Mheshimiwa Mustapha B. Akunaay, Mheshimiwa Jaddy S. Jaddy, Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu, Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Jasson S. Rweikiza, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah na Mheshimiwa Dkt. Hadji H. Mponda. Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashilllah - Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, namshukuru Ndugu Peter Magati - Katibu wa Kamati hii kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja, Mheshimiwa Celina Kombani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Lwanji - Makamu Mwenyekiti wa wa Kamati, naona hata Wajumbe wenzako wa Kamati wanakupigia makofi, naamini wanaunga mkono hoja yako kama Makamu Mwenyekiti.

Baada ya kupokea uchambuzi na maoni ya Kamati ya Katiba Sheria na Utawala kama ilivyowasilishwa hapa mbele na Mheshimiwa Paul Lwanji, naomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kama nilivyotoa taarifa hapo awali kwamba makadirio haya yamechambuliwa na Kamati mbili za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge - Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi atawasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati yake.

MHE. ANDREW J. CHENGE-MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba

kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, Wajumbe wa Kamati wanatoa mkono wa pole kwa Mheshimiwa Stephen Wasira - Mbunge na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) kwa kufiwa na mama yake mzazi. Tunamwomba Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema amweke mama yetu mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikusalimu wewe binafsi na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jina la wananchi wa Jimbo la Bariadi Magharibi ambao ndio wameniwezesha kuwa mbele yenu hapa. Nawaahidi wananchi wa Bariadi Magharibi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa uadilifu mkubwa ili kuhakikisha maendeleo ya Jimbo letu, Wilaya yetu pamoja na Mkoa wetu mpya wa Simiyu na kwa Taifa letu kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Vikao vya Kamati vilivyofanyika Dar es Salaam kati ya tarehe 28 Mei na tarehe 8 Juni mwaka huu, Kamati ilipokea taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Fungu Na. 66 kwa mwaka 2011/2012 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ya Ofisi hiyo. Kamati ilipokea na kujadili taarifa hiyo kwa kina na hatimaye ikatoa ushauri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyakati tofauti, Kamati ya Fedha na Uchumi imekuwa ikitoa ushauri na maagizo mbalimbali kwa Tume ya Mipango ambayo yamekuwa yakizingatiwa ipasavyo na Tume hiyo katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango imeweza kutekeleza ahadi mbalimbali zilizotolewa wakati Bajeti ya Ofisi hiyo kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 ilipowasilishwa Bungeni kama ifuatavyo:-

- Tume ya Mipango imeweza kuitangaza Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/2012 mpaka 2015/2016) kwa kuandaa na kutoa machapisho, makala na vipeperushi mbalimbali pamoja na kufanya semina kwa Waheshimiwa Wabunge, Makatibu Tawala wa Mikoa, Watanzania wanaoishi ughaibuni hasa Marekani na Canada, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na pia kwa Washirika wetu wa Maendeleo, Watumishi wa Wizara za Serikali na Viongozi mbalimbali wa Mikoa na Wilaya.
- Tume ya Mipango imeweza kufanya tafiti mbalimbali za masuala ya uchumi na ustawi wa jamii, pamoja na kukamilisha rasimu ya Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Miaka 15 (*Tanzania Long Term Propective Plan* (2011/2012 - 2025/2026)).
- Tume ya Mipango imeendelea kujenga na kuimarisha uwezo wake kwa kuajiri wataalam

mbalimbali wa uchumi, wachambuzi wa sera, Wahandisi na kada mbalimbali.

- Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, imeweza kuandaa na kukamilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2012/2013 ambao uliwasilishwa Bungeni na Waziri mwenye dhamana.
- Tume ya Mipango imefanya uchambuzi na kuishauri Serikali kuhusu miradi ya kitaifa ya kimkakati inayotakiwa kutekelezwa kwa kipindi cha mwaka huu wa fedha.
- Kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango ilifanya uchambuzi juu ya miradi ya kimkakati na bajeti ya miradi hiyo.
- Kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango iliandaa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011.
- Tume ya Mipango imekamilisha majadiliano na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) ambalo limekubali kuchangia maeneo kadhaa ya Bajeti ya Tume hiyo katika kuijengea uwezo pamoja na kuipatia vitendea kazi. Kwa kuanzia, katika mwaka wa fedha 2012/2013, *UNDP* na *UNFPA* wamekubali kuchangia Bajeti ya Tume kiasi cha Shilingi bilioni 2.1.
- Tume ya Mipango imeanza ushirikiano na Serikali ya Marekani katika kuandaa Mkakati wa Ukuzaaji wa Uchumi (*Partnership for Growth*) kati ya nchi yetu na Marekani. Pia imeanzisha ushirikiano na nchi ya

Malaysia ili iweze kusaidia katika kutengeneza mfumo wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Serikali imekuwa ikitenga Bajeti ndogo kwa Tume hii na hivyo kuifanya Tume ishindwe kugharamia shughuli zake.
- Bado kuna upungufu wa wafanyakazi hasa katika upande wa wachambuzi wa sera na kada nyinginezo muhimu.
- Bado kuna ushirikiano hafifu kati ya Tume ya Mipango na Wizara nyingine, Mikoa pamoja na Wilaya.
- Kutokuwepo na uhamasishaji wa kutosha kwa Watanzania kuweza kushiriki katika miradi ya ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*PPP*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Fedha na Uchumi imekuwa mstari wa mbele katika kutoa maoni na ushauri kwa Tume ya Mipango hasa wakati wa kupitia, kujadili na kuandaa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na Ushauri wa Kamati unaotolewa katika Taarifa hii ni mwendelezo wa maoni yaliyotolewa wakati wa mijadala ya maandalizi ya Mipango hiyo. Hata hivyo, Kamati inapenda kuweka msisitizo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango ina jukumu kubwa la kusimamia rasilimali za Taifa na kuishauri Serikali kuhusu matumizi bora ya rasilimali hizo. Aidha, Tume ina jukumu la kusimamia na kutoa miongozo kuhusu masuala ya kiuchumi na kijamii pamoja na kusimamia mipango ya Serikali na kuchambua sera zake za uchumi. Kwa kuwa Tume ya Mipango ndiyo *think tank* ya Serikali, na ni chombo chenye uwezo wa kiutendaji katika kuandaa mipango ya maendeleo katika nchi yetu, Kamati inaitaka Tume iwe inawasilisha mara kwa mara mbele ya Kamati Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa kila mwaka. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha miradi yote iliyopendekezwa na Tume ya Mipango kwenye Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2012/2013 itekelezwe na Wizara husika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Tume ya Mipango kuhakikisha kuwa inashirikiana kikamilifu na Wizara ya Fedha pamoja na Wizara nyingine zikiwemo Taasisi za Serikali ili kuhakikisha inasimamia na kuratibu ipasavyo miradi ya maendeleo inayotakiwa kutekelezwa katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa kwa miaka mitano (2011/2012 – 2015/2016). Aidha, tathmini ya utekelezaji wa miradi hiyo lazima ifanyike kila baada ya miezi sita kwa

madhumuni ya kupima utekelezaji wa Mpango uliofikiwa na Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kushauri kwamba, ushirikiano kati ya Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha uimarishwe zaidi hasa katika kuweka vigezo vya mgao wa Bajeti ya Serikali ya kila mwaka ili kuhakikisha kuwa vipaumbele vya kitaifa na vya kimkakati vinatengewa fedha za kutosha.

Mheshimiwa wa Spika, Kamati inashauri kuwa, mfumo wa kutoa na kupata taarifa uboreshwe kwa kiwango cha juu kwa sababu Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2012/2013 uliowasilishwa na Serikali Bungeni, hautoi picha halisi kulingana na kazi zilizoainishwa katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kwa mfano, katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2012/2013, Mpango huo hauainishi ushiriki na mchango wa sekta binafsi katika kutekeleza shughuli zinazotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto zilizoainishwa ni kutokuwepo kwa uhamasishaji wa kutosha kuwawezesha wananchi kuelewa na kushiriki katika kutekeleza miradi ya ubia na sekta binafsi. Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa, vitengo vya uwekezaji katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Fedha, vipewe jukumu la kutoa elimu juu ya miradi yote iliyoinishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2012/2013 pamoja na mipango yote iliyomo katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa (2011/2012 - 2015/2016).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha utekelezaji kwa wakati wa miradi ya kitaifa ya kimkakati na miradi mingine ambayo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, Kamati inashauri Serikali iachane na utamaduni uliozoeleka wa kufanya uhamisho wa fedha (*reallocations*) kwenye mafungu yenyе fedha za miradi ya maendeleo pindi yanapojoitokeza mahitaji ya fedha yaliyo nje ya Bajeti ya Serikali. Kamati, kwa msisitizo mkubwa, inashauri Serikali iweke mfumo utakaohakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zinalindwa (*ring fenced*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango imekuwa ikijikita katika kufanya tafiti mbalimbali kama alivyoeleza mtoa hoja, ambazo kimsingi ni tafiti muhimu katika kuhakikisha zinasaidia kuleta uelewa katika kukamilisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mfano wa tafiti hizo ni pamoja na zifuatazo:-

- (i) Uendelezaji wa taaluma na ujuzi unaohitajika kuiwezesha Tanzania kuwa na nguvu za kiushindani ifikapo 2025;
- (ii) Muundo – Taasisi kwa ajili ya kuharakisha maendeleo ya Sekta ya Viwanda nchini; na
- (iii) Maendeleo ya Miundombinu Msingi kwa kilimo cha kisasa na cha kibashara Tanzania.

Tafiti zote hizi zinahitaji fedha za kutosha ili Tume ifanye kazi zake kufuatana na mazingira halisi ya sasa yanayotawaliwa na *TEHAMA*. Kwa vile majukumu ya Tume ni pamoja na yale ya kuelekeza na kuongoza

Mipango na Uchumi wa Taifa, fedha zinazotengwa kwa Tume ya Mipango bado ni kidogo. Kamati inasilitiza Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha ili kazi zote za Tume ikiwa ni pamoja na tafiti, zikamilike kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hairidhishwi na hali ya sasa ya utegemezi katika bajeti ya Tume ya Mipango. Utaona katika Kitabu cha Maendeleo Vol. 4, fedha zote za miradi ya maendeleo zinazoombwwa kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013 ni fedha kutoka nje.

Kamati inaona eneo hili ni vyema Serikali tukaanza kujijengea uwezo wetu wa ndani kuweza kutenga fedha za maendeleo kwa Tume hii muhimu. (*Makofi*)

Aidha, Kamati inashauri Tume iongeze katika orodha ya tafiti zinazokusudiwa kufanywa, utafiti ukaoweza kufahamu ni namna gani nchi yetu itaweza kujiaandaa vizuri kutumia fursa mbalimbali katika Sekta ya Madini na zile zinazotokana na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa gesi asili na hatimaye mafuta hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati bado inaishauri Serikali kushughulikia kwa haraka maombi ya Tume ya kuongezewa idadi ya watumishi ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake. Kwa kuwa Tume ni chombo cha ushauri katika masuala ya kiuchumi na kijamii hapa nchini, ni muhimu ikapata wataalam waliobobea katika nyanja mbalimbali pamoja na uwezo wa kujenga mtandao wa kitaalam kitaifa na kimataifa. Aidha, Kamati inashauri kuwa programu za

kuwapatia mafunzo na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Tume, ziendelezwe kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwapata watumishi waliobobea katika nyanja mbalimbali ni kitu kimoja, na kuendelea kuwa nao katika ajira ya Tume ni kitu kingine. Kwa kutambua ukweli huo, Kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa kuijengea Tume mazingira wezeshi yatakayowavutia wataalam wenye ujuzi na uzoefu wa hali ya juu, watakaolipwa vizuri, watakaopewa vitendea kazi na fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya tafiti. Wahenga walisema, "Kitunze, kidumu". (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na uamuzi wa Tume wa kuanzisha katika muundo wake, Idara ya Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyoshauriwa na Kamati kwa kipindi cha bajeti kilichopita. Hii itasaidia kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, hasa miradi ya kipaumbele. Kamati inashauri Tume iangalie uwezekano wa kutumia uzoefu wa nchi kama Malaysia, India, China, Vietnam na kwingineko kwa suala zima la kuweka mfumo mzuri wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo usiokwenda sambamba na kuwepo kwa mfumo madhubuti wa kufuatilia na kutathmini miradi kwa wakati, hauna tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kuwa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango ikamilishe haraka marekebisho ya Sheria inayounda Tume hiyo ili yaweze kuwasilishwa Bungeni haraka iwezekanavyo katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Marekebisho ya Sheria hii yataiwezesha Tume kuwa na nguvu ya kuweza kusimamia na kufuatilia miradi yake yote kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati bado inaendelea kusitiza kuwa Tume ya Mipango lazima iangalie namna itakavyofanya kazi zake katika ngazi mbalimbali kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Hivyo basi, Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) pamoja na Wizara nyingine, isimamie utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa kila mwaka katika ngazi zote. Hii itasaidia kugundua na kuibua fursa za uchumi zilizoko katika maeneo ya ngazi mbalimbali na kuweza kuzihusisha katika mpango wa maendeleo. Utaratibu huu utarahisisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa kueleweka vizuri katika ngazi zote na kusaidia kufuatilia utekelezaji wake. Dhana hii lazima iendane na kuweka mazingira wezeshi yatakayosaidia kuibua fursa mpya katika ya vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) - Mheshimiwa Stephen Wasira, na kwa namna ya pekee Mheshimiwa George H. Mkuchika - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora) kwa kuwasilisha kwa umahiri mkubwa kwa niaba ya

Mheshimiwa Stephen Wasira Hotuba ya Ofisi ya Rais, Mipango kama tulivyomsikia asubuhi hii.

Kamati inamshukuru Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango - Dkt. Philip Mpango pamoja na wataalamu wa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa kuwa tayari kutoa ufanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ambao wameweza kutoa maoni na michango mbalimbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba nitumie nafasi hii kuwatambua Wajumbe wote kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula - Makamu Mwenyekiti, na Wajumbe ambao ni Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Eustas O. Katagira, Mheshimiwa Maulidah A. V. Komu, Mheshimiwa Devotha M. Likokola, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu L. N. Madelu, Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Aboot, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman A. Mbewe, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere,

Mheshimiwa Amina Abdulla Amour, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina na mimi Mwenyewe Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mtemi Andrew John Chenge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru wewe binafsi na nimshukuru Spika, wetu na nampa pole kwa yote yaliyompata, Mwenyezi Mungu amuimarishe katika kipindi hiki kigumu, namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati hii ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati hii. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas D. Kashillilah, Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi - Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoanza kukusalimu wewe, nimalizie sasa kwa kusema haya, kwamba sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango Fungu la 66, kama alivyowasilisha mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge kwa niaba ya Kamati, lakini pia ukiwa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi.

Waheshimiwa Wabunge, natoa mwongozo kidogo, lakini kabla ya hapo, nina tangazo nililopewa na Mheshimiwa Hussein Mzee, likiomba kwa msisitizo kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM wafike katika Ofisi za CCM pale Bungeni na kila mmoja ahakikishe anachukua ratiba na miongozo maalum ambayo iko pale katika Ofisi kwa shughuli zake za kiutendaji.

Mheshimiwa Hussein Mzee - Katibu Msaidizi ananisisitiza sana niwasisitize Wabunge wote wa CCM kujali agizo hilo na kulitekeleza haraka iwezekanavyo.

Baada ya hapo Waheshimiwa Wabunge, naomba niseme kwamba maombi niliyoyapokea ya wachangiaji wetu wa leo yako maombi kadhaa. Lakini katika orodha, mchangiaji ambaye atapewa kipaumbele kwa mujibu wa utaratibu na kanuni zetu ambaye hajawahi kuchangia hata mara moja katika Mkutano huu ni Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na yeye ndiye atakayeanza kuchangia katika hotuba hii kwa maelekezo niliyopewa hapa Mezani. Baada ya yeye, kuna orodha itakayofuata, na hawa wengine watapewa nafasi ya kuchangia kwa mujibu wa orodha iliyoandaliwa. (*Makof*)

Sasa kama nilivyokuwa nimetoa taarifa hapo awali, mawasilisho ya leo ya Hati Mezani yalikuwa yanahu su Ofisi ya Rais, lakini ikijumlisha Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma nayo ikiwa inaongozwa na dada yetu Mheshimiwa Celina Kombani, hotuba hiyo pia iliunganishwa na Ofisi ya

Rais, Utawala Bora inayosimamiwa na Mheshimiwa George Mkuchika.

Hata hivyo, Hati iliyowasilishwa Mezani leo, pia ilikuwa inamhusu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uhusiano na Utawala Bora ambayo imesomwa na Mheshimiwa George Mkuchika, lakini Wizara hiyo inaongozwa na Mheshimiwa Waziri Stephen Wasira.

Sasa baada ya kupokea taarifa za uchambuzi za kikamati, tumebakizwa na eneo moja la kumsikiliza Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

Sasa kwa mujibu wa Kanuni namba 62 (d) inasema Msemaji wa Upinzani anayewasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani atawasilisha maoni hayo kwa muda usiozidi dakika 30. Hapo ndipo nilipokuwa nataka kutoa mwongozo Waheshimiwa Wabunge ili muelewe nini kitakachofanyika jioni. Msemaji huyu ambaye amewasilisha Hati leo asubuhi, mliona ni Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi amewasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kwa maana ya hati zote mbili zilizowasilishwa kwa Wizara mbili tofauti.

Sasa kwa mujibu Kanuni, Profesa anastahili kupewa saa moja na siyo dakika 30. Sasa kwa hali hiyo, muda hauturuhusu kumpa Profesa nafasi ya kumtendea haki kwa mujibu wa Kanuni. Kwa hiyo, tutakapokuja hapa Saa 11.00 Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi ataanza kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani na atatumia muda wa saa moja na baada ya hapo sasa, tutaanza na ule uchangiaji wa jumla.

Baada ya kutoa mwongozo huo, sasa nasitisha shughuli za Bunge kwa asubuhi hii ya leo na ninaomba Waheshimiwa Wabunge tukutane tena hapa ndani saa Saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.58 mchana Bunge liliahirishwa mpaka
saa 11.00 jioni)*

(Saa 11. 00 jioni Bunge lilitrudia)

Mwenyekiti (Mhe. Sylvester M. Mabumba) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyotangaziwa mchana kwamba tutaanza na kupokea hotuba ya Msemaji Rasmi wa Kambi ya Upinzani kwenye eneo hili, kwa hiyo, naomba kumkaribisha sasa Mheshimiwa Profesa Kahigi, Mheshimiwa Kahigi tafadhal!

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI - MSEMADI
MKUU WA KAMBI YA UPINZANI - OFISI YA RAIS:**
Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru lakini kabla sijaanza kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, napenda kutanguliza pole zangu kwa nlaba yangu na kwa ya Kambi ya Upinzani kwa Mheshimiwa Wasira aliyefiwa na Mama na kwa Mheshimiwa Spika aliyefiwa na Bibi yake. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pole hiso, naomba nianze kutoa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mapendekezo ya mapato na matumizi kwa ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la mwaka 2007, Kanuni ya 99(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, natoa shukrani kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwa imani kubwa alio nayo kwangu na hivyo kunikabidhi majukumu ya kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi katika Ofisi ya Rais kwa upana wake. Nami natoa ahadi kwake kuwa nitajitahidi kwa kadri itakavyowezekana kutimiza majukumu yangu ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, nawapongeza na kuwashukuru wafuatao:-

Kwanza kabisa, familia yangu yote, mke wangu Celina Tibagololwa, watoto wangu Kwelikilwa, Kekutogwa, Kwesiga na Kwizigizia. Pili, wanachama wote wa CHADEMA pamoja na wale wasio wanachama wa CHADEMA katika Jimbo langu la Bukombe. Nawaomba wananchi wote wa Bukombe tuendelee kushirikiana na kushikamana katika azma yetu ya kuleta mabadiliko katika maisha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Ikulu. Ofisi hii ndiyo yenyeye dhamana ya kuangalia usalama wa nchi na hivyo Idara ya Usalama wa Taifa ipo chini ya Ofisi hii. Kambi ya Upinzani katika hotuba zake za nyuma tumekuwa tukiitaka Idara hii ya Usalama kuzingatia

jukumu lake la msingi la kuhakikisha maslahi ya nchi yanalindwa, badala ya kulinda maslahi ya viongozi kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imeingia katika kashfa mbalimbali zinazohusu rasilimali za nchi hii kuporwa au viongozi waandamizi katika Serikali kuijingiza na kushiriki katika mipango ya kuwaibia walipa kodi, lakini Usalama wa Taifa hatujawahi kusikia popote kuwa wamehusika katika kuzuia mchakato huo japokuwa wanakuwa na taarifa za kutosha. Jambo hili linapelekea wananchi kukosa imani na Idara hii na pengine kufikia hata kusema kuwa Idara hii ndio mshiriki mkuu katika kufisadi rasilimali za nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nchi yetu kiusalama si salama kama ambavyo Serikali inataka kuwaaminisha wananchi. Kitendo cha Wahabeshi kuingia tokea huko walikotoka hadi kuja kuonekana wamefia katikati ya nchi, ni ushahidi wa moja kwa moja kuwa usalama wa nchi uko mashakani. Hivi Usalama wa Taifa na Vikosi vyote vya Ulinzi na Usalama vilikuwa wapi hadi Wahabeshi wakavuka mpaka na kuendelea na safari hadi Kongwa? Aidha, kitendo cha kutekwa na kuteswa kwa Kiongozi wa Chama cha Madaktari nchini, Dkt. Steven Ulimboka na Vyombo vya Usalama viro, ni dhahiri kuwa hali ya usalama ni ya mashaka. Hali ya usalama ni tete pia katika mipaka ya Mikoa ya Kigoma na Kagera hususani kuhusiana na wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasema hayo kwa kuwa Rais ndiye Amiri Jeshi Mkuu

wa Vyombo vyote vya Usalama hapa nchini lakini kwa matukio hayo Ofisi ya Rais hajatoa kauli ya kina Bungeni ni kwa vipi watu wanaingia toka nje na wanasafiri hadi katikati ya nchi bila kujulikana. Au kuna mtando wa Vyombo vya Usalama unaojihusisha na biashara hiyo ya kusafirisha watu, jambo ambalo ni hatari kwa usalama wa nchi yetu? Huu ni udhaifu mkubwa kwa Idara ya Usalama wa Taifa. Je, ni kutokana na watendaji kupata kazi bila ya kuzingatia vigezo vya weledi katika kazi husika au kutokujua umuhimu na maana halisi ya Idara hiyo kwa Taifa letu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuiunda upya Idara hii ya Usalama wa Taifa ili iendane na dhana husika ya kulinda maslahi ya nchi na wananchi wake. Ni muhimu kuwa watumishi waajiriwe kwa vigezo vya weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaraka ya Rais, Mfumo wa Uongozi wa Nchi na Mchakato wa Katiba Mpya. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa mamlaka makubwa sana kwa Rais, kuwa yeye ndiye mamlaka ya uteuzi na kufukuza kwa nafasi za juu katika sekta nzima ya Utumishi wa Umma. Wahusika katika nafasi hizo za uteuzi kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakizitumia kwa kuifurahisha zaidi mamlaka ya uteuzi badala ya kuitumikia jamii. Nafasi hizo ni pamoja na: Makatibu wakuu, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Watendaji Wakuu wa taasisi mbalimbali, Mkuu wa Majeshi, Mkuu wa Jeshi la Polisi, Mabalozi, Wenyeviti wa Bodi mbalimbali za taasisi za umma na kadhalika. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inatoa rai kwa Watanzania

kuwa jambo hili liwe ni hoja katika mchakato wa utoaji wa maoni ili Katiba mpya iweke mfumo mpya wa uteuzi ambao utasimamia ufanisi wa utendaji wa viongozi na watendaji wa kuteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa mwaka wa fedha 2011/2012 tulihojî uhalali wa taasisi zinazoanzishwa na wake wa Marais kuwa zao binafsi na sio za Serikali; hivyo, utumishi wa umma kwa Marais unapokoma, wao wanahama na taasisi hizo, jambo hili hupelekea mke wa Rais ajaye kuanzisha upya taasisi nyingine badala ya kuendeleza kazi za ile iliyokuwepo. Nanukuu sehemu ya hotuba hiyo:-

"Mheshimiwa Spika, kumeibuka mtindo wa wake za marais kuanzisha taasisi zao binafsi zisizo za KiSerikali; lakini zinazotumia magari, jina na hadhi ya kiSerikali (ya kuwa Mke wa Rais), kuvuta fedha za wafadhili kwa ajilli ya kufanya kile kinachoitwa "kusaidia jamii". Mifano ya taasisi hizi ni Taasisi ya Maendeleo ya Wanawake (WAMA) ya Mama Salma Kikwete na Mfuko wa Fursa Sawa kwa wote (EOTF) wa Mama Anna Mkapa.

Mheshimiwa Spika, tabia ya kila mke wa Rais kuanzisha taasisi yake tena baada tu ya mumewe kuingia madarakani, inatoa picha mbaya kuwa taasisi hizi huanzishwa kwa maslahi binafsi zaidi kuliko kusaidia jamii; kwa kuwa Mke wa Rais ni taswira ya Rais mwenyewe ambaye ndiye Kiongozi wa Nchi. Kambi ya Upinzani tunaona ipo haja kwa Serikali kuandaa utaratibu rasmi wa kuwa na taasisi moja tu yenye nguvu itakayokuwa inaongozwa na mke au mume wa rais aliye madarakani kama mlezi, na kupokewa na

wake au waume wa marais wajao, ili kuondoa picha hii mbaya ya kila mmoja kujianzishia taasisi au mfuko wake". Mwisho wa Kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya hoja hii katika kitabu cha maelezo ya hoja kilichotolewa na Ofisi ya Rais ukurasa wa 1-4, hayaridhishi kwani kwa bahati mbaya wamelinganisha vitu ambavyo kwa hali ya kawaida huwezi kuvilinganisha. Chungwa na Nanasi yote ni matunda lakini huwezi kuyalinganisha! Huwezi kulinganisha mke wa Rais wa Tanzania na mke wa Rais wa Marekani, hawa wote ni wake wa Marais lakini mfumo wa utawala wa Marekani ni tofauti na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa majibu ya hoja hiyo, Serikali ilisema, nanukuu:-

"Ushauri wa kuundwa kwa Taasisi moja itakayoratibiwa na wake au wanaume wa Marais umepokelewa na utafanyiwa kazi." Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge utekelezaji wa ushauri huu umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Taasisi hii muhimu ipo chini ya Ofisi ya Rais na inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na rushwa kuathiri maendeleo ya nchi yetu kwa kiasi kikubwa, Kambi ya Upinzani tunasisitiza kuwa ni wakati muafaka sasa kwa

Taasisi hii kuwa chombo huru kiutendaji na hata katika uteuzi wa Mkurugenzi wake ili kuondoa dhana ya kukosa nguvu ya kuwachukulia hatua wala rushwa wakubwa au hata viongozi wa siasa wanaojihusisha na vitendo vya kifisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunapendekeza kuwa uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hii ufanywe na Kamati ya Taifa ya Uteuzi na athibitishwe na Bunge. Pia taarifa za taasisi hii ziwe zinawasilishwa Bungeni kila mwaka na kujadiliwa na Bunge kama ilivyo sasa katika kujadili taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*). Tunatoa mwito kwa Watanzania wafikirie jambo hili ili iwe ni mojawapo ya hoja zitakazozingatiwa katika mchakato wa kuandikwa kwa Katiba mpya ambao ukusanyaji wa maoni unaanza rasmi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunaendelea kusisitiza kuwa bado kasi ya utendaji kazi wa Taasisi hairidhishi kutokana na kuwa na mlundikano wa tuhuma mbalimbali za rushwa na kushindwa kufanyia kazi taarifa mbalimbali za rushwa kama zinavyowasilishwa hasa kipindi cha uchaguzi. Mathalani katika mwaka wa fedha unaoisha, TAKUKURU ilichunguza tuhuma 3,456 ambapo kati ya hizo ni tuhuma 727 tu ndio zilizokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kuna taarifa mbalimbali zilizotolewa na vyombo vya habari kwenye gazeti la *The Citizen* la tarehe 23/06/2012 na gazeti la Mwananchi la tarehe 26/06/2012 kuwa kuna baadhi ya viongozi wa Serikali na baadhi ya wafanyabiashara

nchini wenyе akaunti mbalimbali katika benki nchini Uswisi na kuna fedha kiasi cha shilingi bilioni 315 ambazo ziliingizwa na makampuni mbalimbali ya uchimbaji madini na utafutaji mafuta zinazofanya kazi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hizi ni nzito, sio za kupuuzwa hasa na Idara yetu ya Usalama wa Taifa pamoja na TAKUKURU. Pamoja na Waziri Mkuu kuiagiza TAKUKURU kufanya uchunguzi, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali itumie uzoefu wa nchi nyingine, kwa kuiomba Mahakama ya Uswisi izilazimishe benki za huko walikoweka fedha zitoe majina ya wahusika na kiasi cha fedha walichonacho katika benki hizo, ili wananchi wafahamu. Hii ni hatua ya kwanza. Hatua ya pili ni kuangalia je wamevunja sheria gani ya nchi? Kama ni viongozi wa umma ziangaliwe fomu za maadili ya umma kama fedha hizo walizitaja, kama ni za wizi basi zirejeshwe nchini; fedha hizo zinaweza kutumika kuboresha elimu au hata kuwalipa wazee wetu pensheni kama tulivyopendekeza kwenye hotuba yetu kuhusu bajeti ya mwaka 2012/2013 kwani zinahitajika shilingi bilioni 318.691 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa hiyo Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu katika Mkutano huu wa Bunge unaoendelea wamiliki wa fedha hizo, zimepatikaje na hatua gani ambazo serikali itachukua dhidi ya watu hao. Pia tunaitaka Serikali kupanua wigo wa uchunguzi ili kuzihusisha nchi za Afrika Kusini na nchi za Falme ya Kiarabu (UAE) ambapo mafisadi wengi wanatuhumiwa kuficha fedha na mali katika nchi hizo. Pia kila kiongozi

wa kisiasa mwenye fedha na mali nje aangaliwe kama alitoa taarifa ya mali na fedha hizo kwenye fomu za maadili alizokwisha kuzijaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua ya sasa na jinsi rushwa inavyoathiri nchi hii, ni vema Serikali ikazingatia ushauri wetu wa mwaka uliopita kwenye hotuba ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuwa Idara ya Usalama wa Taifa pamoja na kazi zake nyingine ifanye ujasusi wa kiuchumi (*economic espionage*) kwa ajili ya kupata taarifa za wawekezaji mbalimbali ambao wanakuja nchini kuwekeza ili kuepukana na makampuni ya mifukoni kama ilivyokuwa Richmond. Ujasusi huu wa kiuchumi ujumuishie utafutaji wa fursa za kiuchumi kwa ajili ya nchi yetu katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la rushwa linaloigusa Serikali hii ndio msingi wa pendelekezo la Kambi ya Upinzani la mara kwa mara kuhusu kufanya maboresho ya Idara ya Usalama wa Taifa. Taarifa za rushwa kubwa (*grand corruption*) kama kashfa ya rada, rushwa ya Richmond, sakata la *EPA* na ujisadi wa *IPTL*, ni ishara kuwa Idara hii sio tena Usalama wa Taifa bali Usalama wa Viongozi wa Serikali, Chama chao na Familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa mwaka uliopita, tuliomba maelezo kuhusu watumishi waliohusika katika wizi wa *Deep Green*, Kagoda na mkataba wa *IPTL* na ujisadi mwingine. Naomba ninukuu sehemu ya hoja hiyo kama ifuatavyo:-

"Mheshimiwa Spika, aidha jitihada za dhati hazijaonekana za kushughulikia watumishi wa umma waliojotajwa kwenye orodha ya mafisadi waliohusika na kashfa za Kagoda, Meremeta, Deep Green, Richmond, IPTL na mikataba mingine inayoendelea kulitia hasara Taifa letu". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo, Serikali kwenye ukurasa wa 32 wa kitabu cha majibu ya ofisi ya Rais ilisema na nanukuu:-

"Uchunguzi dhidi ya kashfa ya Kagoda, Meremeta na Deep Green unaendelea. Aidha, IPTL uchunguzi umepiga hatua kubwa". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa taarifa kwa Bunge hili uchunguzi wa ubadhirifu huo. Je, utakamilika lini na watuhumiwa kufikishwa katika vyombo vyahabari? Kwani hivi sasa ni takribani miaka 10 toka kashfa ya Meremeta, Deep Green na Kagoda itolewe hadharani na IPTL ni takribani miaka 17. Huu ni muda tosha kabisa kwa taasisi makini kukamilisha kazi ya uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge kuhusishwa na vitendo vyahabari. Kumekuwepo na vitendo vyahabari ambapo zimetolewa tuhuma kadhaa na vyombo vyahabari pamoja na Waheshimiwa wenyewe kutuhumiana na wengine kukamatwa kwa tuhuma za rushwa. Ni dhahiri hata katika mchakato wa kuchagua Wabunge la Afrika ya Mashariki kauli za vitendo vyahabari zilitolewa na

Waheshimiwa Wabunge. Kambi ya Upinzani inaitaka TAKUKURU kuhakikisha kuwa pamoja na kuwakamata watuhumiwa wengine, iendelee kuchukua hatua kulisafisha jina la Bunge katika kashfa hii nzito inayoliondolea heshima mbele ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la David Jairo. Katika Bunge la Bajeti la mwaka uliopita wakati wa kujadili bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini tuhuma za aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndugu David Jairo kukusanya fedha bila utaratibu kwa ajili ya kupitisha bajeti ziliibuliwa na kulifanya Bunge kuazimia kuunda Kamati Teule kwa ajili ya kuchunguza suala hili. Pamoja na Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma yaani Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi kumsafisha Jairo na wenzake na hatimaye Jairo kurudishwa tena ofisini, Bunge lilitekeleza jukumu lake na kupitia Kamati Teule uliyoiundwa na Mheshimiwa Spika, Bunge lilithibitishiwa kuwa utaratibu wa ukusanyaji wa fedha zile haukuzingatia sheria na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunahoji ni hatua gani ambazo TAKUKURU wameshachukua juu ya tuhuma dhidi ya Jairo na wenzake ambazo zilithibitishwa na Kamati ya Bunge lako Tukufu? Kama hatua hazitachukuliwa dhidi yake ni dhahiri taasisi hii haitalitendea haki Taifa hili na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*). Mfuko wa Maendeleo ya Jamii kulingana na malengo yake ya kupunguza umaskini bado umeshindwa kujikita kwa walengwa kutokana na

kukumbwa na changamoto za ubadhirifu wa rasilimali tengwa. Ubadhirifu huu umebainishwa katika Ripoti ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya miradi ya maendeleo iliyotolewa tarehe 30Juni, 2011 kuhusu ukaguzi wa taarifa za fedha za miradi ya maendeleo kifungu cha 5.3.1 juu ya manunuzi ya vifaa ambavyo havikupokelewa. Changamoto zilizopo ni kutokuwepo kwa ushindani, kufanya manunuzi bila mipango, huu ni udhaifu wa Ofisi ya Rais kwa kusababisha hasara ya shilingi 50,275,000. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzingatia upungufu huu na hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya waliohusika na ubadhirifu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*PTF*). Lengo la Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*PTF*) ni kuwasaidia wananchi wa kipato cha chini kwa kutoa mikopo yenyе riba nafuu. Hata hivyo, mfuko umeshindwa kufikia malengo yake ikizingatiwa kwamba mikopo hutolewa kwa riba inayolingana na taasisi nyingine za kifedha. Kama mfuko huu unakopa katika benki kwa riba na baadaye kukopesha *SACCOS*, ni kwa nini Mfuko huo usifanye kazi ya kutengeneza mazingira mazuri ya ukopeshwaji ili *SACCOS* na watu wengine wakope kwenye mabenki moja kwa moja? Kwani hapa inaonyesha kuwa Serikali inafanya kazi ya Udalali na hivyo mzigo wa riba kuangukia kwa mkopaji wa mwisho ambaye ni mwananchi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuheshimu dhamira ya kuwasaidia wananchi wa hali ya chini kiuchumi na kutekeleza dhana ya kuanzishwa kwa mfuko huu ikiwa ni pamoja na kuwanufaisha

walengwa na kutotoza riba za kibashara kama hali ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurabita. Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (*MKURABITA*) umekuwa ukitekelezwa kwa kasi ndogo kwa kuzingatia vigezo na tathmini zinazofanywa. Hii hupelekea Wilaya nyingi kutofikiwa na mpango huu. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kusambaza mpango wa MKURABITA kwa nchi nzima kuliko utaratibu ulivyo sasa. Tunaitaka Serikali iandae mpango mkakakti wa MKURABITA utakaoonesha jinsi Mpango huu utakavyotekelawa nchi nzima hatua kwa hatua. Kadhalika Serikali, igharimie zoezi la urasimishaji kwa kutenga bajeti inayotosheleza zoezi zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa matatizo yanayokabili MKURABITA ni tatizo la mgongano wa kisheria kwa kipindi kirefu unaosababisha ugumu katika utekelezaji wa mpango huu. Sheria hizo ni Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114 na Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya Mwaka 2007, ambazo ni miongoni mwa Sheria zinazotumika katika kusimamia sekta ya ardhi. Mchakato wa kufanya marekebisho ya sheria hizi ulianza miaka iliyopita mpaka sasa haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iliyotolewa katika randama ya Ofisi ya Rais katika mafungu 20,30,32,33,67,94 na 9 ukurasa 36 imeainisha na nanukuu:-

"maandalizi ya maboresho ya Sheria za Ardhi na Biashara yalikamilika mwaka 2008".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuharakisha mchakato wa Miswada ya Sheria hizi za Ardhi na kuzileta Bungeni ili zihadiliwe. Maboresho ya sheria yataondoa dosari nyingi na kurahisisha utekelezaji wa MKURABITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Tatizo la watumishi hewa. Kada ya Utumishi wa Umma imekumbwa na kashfa kubwa ya watumishi hewa. Tarehe 23 Machi, 2011, Rais Jakaya Kikwete, alinukuliwa na Magazeti ya *The Guardian Namba ISSN 0856- 5422* toleo 5083 na *Daily News Namba ISSN 0856 – 5422* toleo 10,302 akiagiza ukaguzi ufanyike katika Idara zote za Serikali baada ya taarifa kwamba shilingi bilioni tisa (9 bilioni) za mishahara zimelipwa kwa watumishi hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watumishi hewa ni mbinu nyiningine ambayo mafisadi ambao kimsingi ni wahujumu uchumi wanaitumia kutafuna fedha za umma bila jasho. Licha ya tatizo hilli la watumishi hewa kuathiri malengo mahsus ya bajeti ya Serikali, pia linapunguza ufanisi katika kada hii ya utumishi wa umma na hivyo kulisababishia Taifa hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inalaani wizi huu wa fedha za umma unaofanywa katika utumishi wa umma huku viongozi waliopewa dhamana ya kusimamia fedha za umma wakibaki na

mshangao badala ya kutoa majibu ya kiuwajibikaji. Kambi ya Upinzani inataka Serikali, itoe taarifa rasmi ya hatua madhubuti ilizochukua kukomesha tatizo la watumishi hewa Serikalini, ikiwa ni pamoja udhibiti wa malipo na tunatoa rai kwamba wahusika wa kashfa hii wachukuliwe hatua mara moja ili liwe fundisho kwa yejote aliye na nia ya kuchezea fedha za walipa kodi wa nchi hii. Kadhalika hii ni dalili wazi ya udhaifu wa Serikali kutokuwa na kumbukumbu sahihi za watumishi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Ajira. Serikali iliamua kuachana na sera yake ya *D by D* na hivyo kufanya ajira zote za umma kupitia Sekretarieti ya Ajira. Uamuzi huo kwa bahati mbaya sana umeanza pia kugusa ajira za Vyuo Vikuu vya Umma! Kambi ya Upinzani tunaona mpango huu wa Sekretarieti ya Ajira ni vyema ihusike tu na watumishi wa umma wa Serikali Kuu na sio Serikali za Mitaa au taasisi zingine za Serikali. Kwani uamuzi huo ni dhahiri unakinzana na Sheria zilizoanzisha taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Ajira kuchukua jukumu la kuajiri watumishi bila kujali ni wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa au taasisi za Serikali, ni jambo la hatari la kuhodhi madaraka na ukiritimba usiotakiwa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba chombo hicho kina kazi chache kama mfumo wa ugatuaji wa madaraka ungekuwa unafanya kazi kwa kadri ya uanzishwaji wake. Rai yetu ni kwamba taasisi ambazo kisheria zina mamlaka ya kuajiri ziachwe ziendelee kuajiri kama ambavyo zimekuwa zikifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya uzeeni yenye utata. Malipo ya uzeeni kwa watumishi wa umma wastaafu ni jambo linahitaji uangalizi makini kwani linaweza kutumiwa vibaya na watendaji na hivyo kupoteza fedha za umma. Kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2011, ukokotoaji wa fedha za malipo ya uzeeni ulizidi kwa kiasi cha shilingi 539,201,733.63 na kiasi kilichopunjwa ni shilingi 106,007,774.81. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, ameeleza kwamba, kama malipo ya uzeeni yangelipwa bila kukaguliwa basi Serikali ingepata hasara ya shilingi 539,201,733.63 na vilevile wazee wangelipwa pungufu ya shilingi 106.007, 774.81.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inakemea vikali hali ya watendaji wa Serikali ya kutokuwa makini katika kutekeleza majukumu muhimu hasa yanayohusu fedha za umma. Kambi ya Upinzani inashawishika kuamini kwamba fedha nyingi za walipakodi wa Tanzania zinapotea kwa sababu ya uzembe wa watendaji wa Serikali. Tunaitaka Serikali kutoa taarifa ya hatua ilizochukua hadi sasa kutokomeza uzembe kama huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pensheni kwa Wahadhiri Wastaafu wa Vyuo Vikuu vya Umma. Hawa ni wale waliokuwa kwenye Utaratibu wa SSSS. Suala hili lilzungumzwa mwaka jana katika hotuba ya Kambi ya Upinzani. Utaratibu huu uliwalhusu Wahadhiri na Maprofesa walioajiriwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kabla ya Julai 1978. Kwa mujibu wa utaratibu huu, mstaafu alipata malipo ya mkupuo mmoja tu na hapati pensheni ya kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa SSSS ulifutwa kuanzia Machi 2011. Hata hivyo, katika hatua hiyo Serikali haikuwafikiria Wahadhiri waliostaafu kabla ya tarehe hiyo. Serikali, katika majibu yake mwaka jana, ilisema kuwa Serikali ilitaka kuwahamisha lakini Wahadhiri wakakataa kuhama toka SSSS kwenda taratibu nyingine za hifadhi za jamii miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa hakuna mahali popote wala wakati wowote ambapo Serikali hii iliwaliza wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya Umma jambo kama hili. Kwa hiyo, dai hilo la Serikali lilikuwa si sahihi na sisi tunaelekea kuamini kuwa lilikuwa na lengo la kukwepa jukumu au kuudanganya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba toka miaka ya 1990 hadi Machi 2011, Wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya Umma, kuitia Vyama vyao, walihangaika na suala hili bila mafanikio. Ni jambo la aibu kwa Maprofesa/Wahadhiri wazima kuhangaika baada ya kustaaafu kwa kosa ambalo si lao wakati wanafunzi wao hawapati shida ya pensheni ya kila mwezi na wote wakiwa wamefanya kazi chini ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tayari Serikali imeshaunda Mamlaka ya Udhibiti wa Hifadhi za Jamii na kwa kuwa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu walifanya juhudhi mapema kubadilisha utaratibu huo kuanzia miaka ya 1990 bali mafanikio yakaja yamechelewa kwa wengi wao waliostaafu kabla ya Machi 2011, na

kwa kutambua mchango mkubwa ambao hawa watumishi wa Vyuo Vikuu wameutoa kwa taifa, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuielekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Hifadhi za Jamii kuanza kupanga jinsi ya kuwapatia pensheni ya kila mwezi wastaa fu hawa. Tunaomba suala hili lichukuliwe kwa umuhimu wake, kwani hakuna mtu anayependa kuona anafanyiwa ubaguzi wa mafao kwa makosa ambayo si yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali. Kwa muda mrefu sasa Kambi ya Upinzani tumekuwa tukipinga ongezeko la matumizi ya Serikali hasa katika gharama za uendeshaji. Ukiangalia mfumo mzima wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma utaona kuwa muundo wake unaongeza gharama ambazo zingeweza kuepukwa. Kwa mfano shughuli za kada hii ya Utumishi wa Umma zinaratibiwa na vyombo vifuatavyo: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma. Kazi za taasisi hizi zinazofanywa kwa ujumla ni zilezile za usimamizi wa Utumishi wa Umma na vilevile hazitimizi majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa jinsi taasisi hizi zisivyotimiza wajibu ipasavyo. Sekretarieti ya Ajira iliyoanzishwa baada ya marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Na.18 ya 2007, pamoja na mujukumu mengine, ina majukumu yafuatayo: kuwatafuta wataalamu na kuwa na kanzidata kwa ajili ya ajira na kusajili wahitimu na wataalamu kurahisisha ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uzoefu unaonesha kwamba Sekretarieti hii imekuwa ikitoa matangazo ya kazi tu bila hata kufanya usaili, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuonesha idadi ya wataalamu ambao wameshatafutwa na Sekretarieti ya Ajira na idadi ya wahitimu na wataalamu ambao tayari wamesajiliwa na wapo kwenye hiyo kanzidata ambayo imetajwa na sheria husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa na chombo kimoja kitakachoratibu mambo yote ya utumishi wa umma. Faida ya kuwa na chombo kimoja ni kwamba usimamizi wake utakuwa ni rahisi na kwa jinsi hiyo kitakuwa na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro baina ya Serikali na watumishi wake. Ingawa kuna sheria mbili nzuri, yaani Sheria Namba 19 ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2003 inayoitaka Serikali kuwashirikisha watumishi katika maamuzi kuhusiana na utumishi wa Umma na Sheria ya Mahusiano Kazini ya mwaka 2004, Serikali inasuasua katika utekelezaji wake na hivyo kusababisha migogoro na wafanyakazi na kuathiri huduma muhimu kwa jamii. Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, akiwasilisha Bungeni makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2009/2010, aliahidi mbele ya Bunge kutekeleza maagizo ya Sheria hizi lakini matokeo yake hayatoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inajali huduma kwa jamii hivyo inaitaka Serikali kuzingatia sheria hizi na ishirikishe watumishi wa umma katika maamuzi yanayowahusu watumishi hasa maslahi yao. Aidha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ioanishe Sheria hizi iwe moja itakayoshughulikia na kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya watumishi wa umma yameongezeka kwa kasi huku yakichukua sura mpya ya migomo kama nyenzo ya kuishinikiza Serikali kutatua madai yao. Siku za hivi karibuni tumeshuhudia migomo ya Madaktari ambayo licha ya kuathiri uwajibikaji na ufanisi katika utumishi wa umma, imesababisha vifo vya Watanzania maskini wasio na hatia. Hata sasa kuna dalili za mgomo baridi kwa Madaktari ambapo hali ya huduma katika hospitali zetu sio nzuri hata kidogo. Pia kumekuwa na matishio ya migomo hasa watumishi wa kada ya Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya watumishi hawa ni pamoja na nyongeza ya mishahara kwa wale wenye stahili, malimbikizo ya mishahara (*salary arrears*) ambazo hucheleweshwa sana hadi mtumishi kusahau stahili zake, fedha za usumbufu wa uhamisho, feha za likizo, mafao ya uzeeni kwa wastaaifu, kupunguza kiwango cha kodi (*PAYE*) katika mishahara na kuweka mazingira bora ya utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumesikia kauli za upande mmoja tu wa Serikali, Bunge liingilie kati kuthibitisha kama madai haya ni halali au si halali. Kambi ya Upinzani inatoa ushauri wa bure kwa Serikali

kuharakisha kushughulikia madai haya kwani dalili za migomo kwa watumishi wa umma zinazoendelea hivi sasa sio nzuri kwa uchumi wa nchi yetu na pia sio dalili nzuri kwa amani ya nchi yetu. Ni matumaini ya Kambi ya Upinzani kuwa Serikali hii ya CCM ambayo imekuwa ikijiita sikivu basi na isikie sasa na kutatua madai ya watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kunukuu kauli ya Mtendaji Mkuu wa *ESRF* kuhusiana na mgomo wa Madaktari:-

"Maoni ya wengi kutokana na mgomo wa Madaktari wa Februari 2012, yalilenga zaidi kwenye kuboresha uwajibikaji wa viongozi katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kushughulikia maslahi ya wafanyakazi wake; pamoja na kuangalia upya suala zima la malipo na mafao ya wafanyakazi katika sekta zote". (Chanzo, Tovuti ya ESRF, <http://esrf.or.tz/madaktari.pdf>)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuiangalia kwa makini jambo hili kwani uwajibikaji wa viongozi katika sekta mbalimbali ni suala la msingi sana. Kwamba Serikali isiyowajibika kwa wananchi wake katika utoaji wa huduma za msingi na huduma za msingi ni kauli pana sana, maana yake ni kuwa Serikali hiyo inakuwa imekosa uhalali wa kuitawala jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali isiishie kwenye kuwawayibisha viongozi wa Wizara husika, bali ilishughulikie suala la

malipo na mafao kwa makini. Serikali isiishie tu kwa Madaktari, bali iharakishe utekelezaji wa azma inayotajwa ukurasa wa 16 wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (Toleo la Kiswahili Juni 2011) ya kupitia mishahara na marupurupu katika Utumishi wa Umma. Aidha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iyafanyie kazi mapendekezo yaliyo katika Ripoti ya Tume ya Ntukamazina iliyowasilishwa kwa Rais Januari 2007. Lengo la Tume lilikuwa ni kuboresha mishahara na maslahi katika sekta ya utumishi wa umma, lengo hili likamilishwe na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Majadiliano ya Pamoja ya mwaka 2003 na Sheria ya Mahusiano ya Kazi ya mwaka 2004, zinatoa mwongozo wa uwepo wa Mabaraza ya Mashauriano kati ya Serikali na watumishi. Kambi ya Upinzani inasikitika kuona kuwa kipindi hiki chote ambacho kumekuwa na tishio la migomo toka kwa watumishi wa umma, Mabaraza ya Majadiliano ya Watumishi katika sekta ya elimu, afya, Serikali za Mitaa na Serikali Kuu yalimaliza muda wake mwaka 2011. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inatoa rai kwa Serikali iharakishe kuhuisha upya Mabaraza hayo ili yafanye kazi. Sambamba na hilo, Mabaraza yakishaundwa yaache tabia iliyokuwepo awali ya kutokutimiza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maagizo ya Bunge kwa Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Katika kikao cha kujadili mapendekezo ya mpango na bajeti kwa mwaka 2011/2012 cha Juni, 2011, Bunge kupitia Kamati yake ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala iliiagiza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

kutekeleza pamoja na mambo mengine majukumu yafuatayo:-

- (i) Kupanua wigo wa upatikanaji wa wataalamu na kuweka vivutio ili kuimarisha maadili ya watumishi wa umma.
- (ii) Kuangalia upya maslahi ya watumishi kwa kuoanisha hali ya maisha ya sasa ili kuwapunguzia makalli ya maisha watumishi wa Serikali na kuongeza uwajibikaji.
- (iii) Kutilia mkazo mfumo wa "*Open Performance Appraisal System*" (*OPRAS*) kusaidia kurudisha nidhamu ya uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuwa na muda wa kutosha na kutengewa fedha katika bajeti iliyopita bado hajatekeleza kikamilifu maagizo haya. Serikali ilichokifanya ni kutoa majibu mepesi kama vile "tunaandaa mkakati wa kutekeleza" ikiwa ni mwaka mmoja tangu maagizo yatolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maslahi ya watumishi yanayoendana na hali ya maisha ya sasa, majibu ya Serikali ni kwamba inaendelea kuboresha maslahi na kwamba imeongeza kima cha chini hadi kufikia shilingi 135,000/= kwa mwezi. (Na kwamba kwenye mwaka wa fedha 2012/2013 kinatarajiwa kuongezeka mpaka shilingi 170,000/-). Kambi ya Upinzani inaona kuwa Serikali sasa inakwenda kinyume kabisa na kauli mbiu yake ya "maisha bora kwa kila

Mtanzania" kwani kiwango cha 135,000 ni kidogo sana na hakiendani kabisa na hali ya maisha ya sasa kutokana na mfumuko wa bei kuwa juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwa kiwango kidogo cha maslahi kwa watumishi namna hii huchangia kwa kiasi kikubwa utovu wa uwajibikaji na ufanisi wa kiwango cha chini katika utumishi wa umma. Kwa kutambua umuhimu wa mchango wa watumishi wa umma katika kujenga uchumi wa nchi yetu, kambi ya upinzani imekuwa ikipigania kima cha chini cha mshahara kipande hadi kufika shilingi 315,000 lakini kwa masikitiko makubwa Serikali hii ya CCM inayojiita sikuu haijasikia hili hadi sasa. Rai yetu kwa watumishi wote wa umma, waiunge mkono Kambi ya Upinzani katika kupigania haki zao na ili kufanikisha hilo, watupatie ridhaa kuongoza nchi ifikapo mwaka 2015. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutilia mkazo Mfumo wa Tathmini Wazi ya Utendaji "*Open Performance Appraisal System*" (*OPRAS*) ni kwamba mfumo huu bado hautumiki ipasavyo tofauti na Serikali inavyosema. Uzoefu unaonesha kuwa bado taasisi nyingi za Serikali hazitumii mfumo huu na taarifa za mtumishi bado zimekuwa zikishughulikiwa kwa siri na mtumishi hana nafasi ya kuona na kuhoji taarifa zilizopo kwenye jalada lake. Matokeo ya tatizo hili ni mtumishi kukosa haki zake hasa pale anapopandishwa cheo/mshahara na kutopewa stahili hizo pamoja na kwamba taarifa zipo kwenye jalada. Wengine hupunjwa mafao yao ya kustaafuli kwa kuwa taarifa zao sio sahihi. Kama mtumishi angekuwa anapata fursa ya kuangalia jadala lake angepata nafasi ya kutoa

taarifa sahihi na hivyo kupata stahili zake ipasavyo. Inasikitisha kuwa kuna watumishi hadi wanastaafu hawajawahi kuona majalada yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa na tabia ya kutekeleza kikamilifu maagizo inayopewa na Kamati za Bunge na ilete taarifa ya utekelezaji halisi yaliyofanyika na sio kuleta taarifa ya kwamba "mchakato unaendelea..." (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Utendaji (*Performance Management*). Miiongoni mwa matakwa ya msingi ya ufanisi katika utumishi wa umma ni kwa watumishi kufanya kazi kwa bidii na kwa kujituma. Lengo hasa la utumishi wa umma ni kuisaidia Serikali ambayo ndiyo mtumishi mkuu wa umma kutekeleza majukumu ya kusambaza huduma za jamii na kujenga uchumi wa nchi yetu. Ili kutimiza azma hii ni lazima utumishi uwe na ufanisi. Ufanisi katika Utumishi wa Umma unapatikana endapo watumishi watafanya kazi kwa bidii na kwa kujituma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunapata wasiwasi kwamba kumekuwa na desturi ya kufanya kazi kwa mazoea yaani kutokuwa na bidii ya kazi na kujituma katika sekta ya umma. Hali hii inasababishwa hasa na ukosefu wa usimamizi madhubuti wa utendaji kwa watumishi lakini pia kukata tamaa kwa watumishi kutokana na mshahara kutowiana na gharama za maisha. Matokeo ya maslahi kutokidhi mahitaji halisi ya watumishi kunasababisha watumishi kubuni njia mbalimbali za

kujipatia kipato na hivyo kukosa ufanisi katika ajira zao katika utumishi wa umma. (Kwa mfano Walimu wa shule za msingi hufanya biashara mashulen i wakati wa masomo na Wahadhiri Waandamizi katika Vyuo Vikuu vya Umma kufanya kazi za muda mfupi "*part-time jobs*" katika vyuo vingine tofauti na vile walivyoajiriwa). Yote haya yanapunguza tija kwa kiasi kikubwa sana katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi kujiridhisha na kuwa na watendaji wenye sifa (*qualifications*), lakini ni lazima kujenga mfumo wa usimamizi wa utendaji wa watumishi hawa wenye sifa ili utendaji wao uwe na tija kwa taifa. Mfumo huu sio wa "kinyapara" wa kumsimamia mtumishi na kiboko ndipo afanye kazi, bali mfumo ambao utamjengea mtumishi utamaduni wa kuwajibika na aone fahari kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza mfumo shirikishi ambao mtumishi pamoja na mkuu wake wa kazi watakuwa na mahusiano ya karibu na sio uhusiano ule wa bwana na mtwana (*superior Vs subordinate*) uliopo sasa hivi. Hali iliyopo sasa hivi ni kwamba wakubwa wamejifanya "miungu watu" na hivyo watumishi wanawaogopa mabosi wao na hivyo huwakwepa. Hali kama hii haiwezi hata mara moja kuongeza ufanisi katika utendaji kwa kuwa hakuna mawasiliano ya karibu kati ya watumishi na mabosi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, motisha wa vitu (*material incentives*) na motisha wa kauli (*moral incentives*) vimeelezwa na wanazuoni wengi katika tasnia ya

menejimenti ya rasilimali watu kuwa vichocheo vikubwa vyta utendaji mzuri wa watumishi. Kwa kuwa watumishi wengi hujishughulisha na kazi nyingine nje ya ajira zao muda uleule wanaopaswa kuwa kwenye vituo vyao vyta ajira, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuongeza mishahara ya watumishi kwa kulingana na hali halisi ya maisha ili watumishi wafanye kazi kwa moyo na kuongeza tija na ufanisi katika kazi zao. Pia ni muhimu kuondoa malimbikizo ya mishahara kwa kuwalipa watumishi stahili zao kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya bajeti Iliyopita. Mwaka uliopita wa 2011/2012, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilitengewa shilingi 33,361,247,000 na mwaka huu wa fedha 2012/2013 wanaomba shilingi 42,431,552,870 ikiwa ni ongezeko la shilingi 9,070,305,000 sawa na asilimia 27.2. Ongezeko hili ni kubwa ukizingatia majukumu yanayotekelizwa hayana tofauti sana na yale ya mwaka jana. Pia baadhi ya kazi zimeandikwa kwa ujumla mno jambo ambalo linatoa mwanya wa kutofanya kazi hiyo kwa ufanisi: Kwa mfano "Kuandaa tafiti 5 katika masuala mbalimbali" (Fungu 32 ukurasa 11 na. xiv) Hii haioneshi shughuli mahsus na hivyo kukaribisha utashi wa mtu binafsi badala ya utashi wa mwongozo. Tunaitaka Serikali ieleteze hizi tafiti ni tafiti gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Utumishi wa Umma. Kumbukumbu zinaonyesha kuwa tangu kuanzishwa kwake kama Wakala wa Serikali mwaka 2000, Chuo cha Utumishi wa Umma kimeendelea kukua na kujiimarisha katika utoaji wa huduma katika nyanja za utumishi, utawala, menejimenti na uongozi

kwa utumishi wa umma. Kambi ya Upinzani inasema kama chuo hiki kipo ni kwa vipi viongozi wateule wanashindwa kutenda kazi zao za kiuongozi? Baadhi ya viongozi wa umma wanajikita kutenda kazi zao kwa misingi ya unazi na ushabiki wa kisiasa jambo ambalo linaleta mitafaruku isiyo na maana mionganini mwa wanaowaongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wetu wengi ama hawafuati kwa dhati au hawaelewi miiko ya uongozi; ndiyo maana vitendo vya wizi na ubadhirifu wa mali za umma vinaendelea. Aidha, kuna upendeleo katika utoaji wa zabuni na mambo yasiyozingatia uadilifu wa utendaji katika sekta ya umma. Rushwa iliyokithiri katika sekta ya umma ni kielelezo tosha kuwa sekta ya umma kwa sasa haifundishwi miiko ya uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uenevu wa ujisadi unabainishwa na nukuu toka taarifa ya utafiti uliofanywa na TAKUKURU kuhusu ujisadi na utawala wa kitaifa ya mwaka 2009:-

"... pamoja na juhudi zilizoorodheshwa hapo juu, ujisadi umeenea na ni kikwazo kikubwa cha juhudi za maendeleo; sababu kubwa ya ujisadi ni ulafi mionganini mwa watumishi wa umma na wafanyakishara; katika baadhi ya vitengo vya utumishi wa umma ujisadi umegeuka kuwa njia ya maisha; asasi ambazo ni za msingi katika kulinda utawala bora kama Polisi na Mahakama ndizo zinazoongoza kwa kushiriki ujisadi." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka TAKUKURU kutoishia kufanya utafiti tu bali iende mbele zaidi kuweza kung'oa mizizi ya rushwa maeneo ambayo imeyafanyia utafiti, kinyume na hapo itakuwa ni kila mara kufanya tafiti za maeneo yanayoongoza kwa rushwa lakini hakuna suluhisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 69.6% ya watumishi wa umma ndio wanaodai rushwa ili watoe huduma kinyume na taarifa kuwa wananchi ndio wanaoanzisha au kushawishi utoaji wa rushwa na mara zote watumishi wa umma rushwa imebatizwa majina kama vile, malipo yasiyo rasmi na jina hili ni lina umaarufu wa asilimia 94.4%, rushwa ya ngono ni asilimia 57.4%. (Chanzo, Taarifa ya Utafiti kuhusu Ufisadi na Utawala kwa Taifa ya Mwaka 2009, juzu 3: utafiti wa watumishi wa umma).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kusitiza ufundishwaji wa maadili na miiko ya utumishi wa umma. Taaluma ya utawala tu haitoshi. Maadili na miiko inayosimamia utendaji lazima ifunzwe vivilvyo. La sivyo sekta ya utumishi wa umma itaendelea kushindwa kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kubadilisha au kusitiza ufundishwaji wa maadili na miiko ya utumishi wa umma, kwani mtu anaweza kuwa ana taaluma ya utawala lakini hana maadili na haelewi miiko inayosimamia utendaji, hii

itakuwa ni kazi bure na sekta ya utumishi wa umma itashindwa kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kambi ya Upinzani kuitia kwa Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe mwaka 2008, 2009 na 2010 tulileta Muswada Bungeni kwa ajili ya kuboresha Sheria ya Maadili ya Viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huo ulipigwa danadana kwamba Serikali inafanya kazi Muswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi lakini mpaka leo Muswada huo haujawasilishwa Bungeni. Kuna haja kubwa ya kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Maadili ili kuifanya kuwa ya uwazi zaidi na wananchi wawe na haki ya kujua mali wanazomiliki viongozi wao wa kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwazi kwenye fomu za maadili ni moja ya suluhisho la kadhia ya ujisadi. Mgongano wa kimaslahi kati ya viongozi wa kisiasa na biashara zao ndio umetufikisha hapa tulipo leo. Hatusemi wanasiwa wasiwe wafanyabiashara, bali ni lazima kuweka wazi maslahi ya kibiashara ambayo wafanyabiashara walio kwenye siasa wanayo vinginevyo ujisadi utaendelea kushika kasi nchini siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara hii ni muhimu sana hasa ukizingatia kuwa inahusika kuhakikisha kuwa viongozi wa umma wanazingatia maadili ya kazi katika utendaji wao kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi hii ina changamoto kubwa sana ya kuongozwa na watumishi ambao ni wastaafu walio wengi kutoka katika mhimili wa Mahakama. Pamoja na kutambua mchango wa Majaji wastaafu wanaoongoza Idara hii, Kambi ya Upinzani inaona ni muhimu sasa Serikali kuchukua hatua ya kuwa na watumishi wenge nguvu, ambao hawajastaifu kwa ajili ya kuboresha utendaji na ufanisi katika kazi muhimu za idara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine kubwa linaloathiri utendaji wa Idara hii ni kukosa bajeti ya kutosha kwa ajili ya kutimiza kazi zake kwa mujibu wa sheria. Mathalani taarifa zilizonukuliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu katika taarifa ya mwaka 2011 zinaonyesha kuwa waliweza kuhoji viongozi 23 tu waliokiuka taratibu za utumishi wa umma na zaidi ya nusu ya Madiwani wote nchini hawakuweza kuwasilisha taarifa zao na hawajachukuliwa hatua yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha utendaji wa Sekretarieti ya Maadili ni vema Serikali ikawapa uwezo wa kifedha na hivyo kuwafanya kufanya kazi kwa uhalisia ikiwa ni pamoja na kuzifanyia uhakiki taarifa zinazotolewa na viongozi na watumishi wa umma kuhusu uhalali wa mali zao. Aidha, ni vema taarifa zote wanazopokea ziwekwe kwenye tovuti ili wananchi wapate taarifa badala ya kuwa na masharti magumu ya kisheria ya kukagua taarifa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Umma. *Commission* hii wajumbe wake wameteuliwa na Rais na iko chini ya Rais na inawajibika kwa Rais, hivyo ni dhahiri haiwezi kufanya jambo lolote ambalo litakwenda kinyume na matakwa ya Rais. Huu ni upungufu mkubwa unaosababisha sekta ya utumishi wa umma kutokuwa huru na hivyo sekta ya utumishi wa umma kukosa uimara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya Rais Kikatiba kwa kiasi kikubwa yanachangia kuivuruga sekta ya utumishi wa umma, kwa dhana kwamba nafasi nyingi na nyeti zinafanywa kuwa za kisiasa badala ya kiutendaji hivyo uwajibikaji wa watumishi hao unakuwa mgumu na badala yake wanafanya kazi kwa lengo la kumfurahisha mtu aliyefanyia uteuzi huo. Mfano nafasi za, Makamishana Wakuu wa taasisi nyeti, Ukurugenzi na Utendaji Mkuu kwenye taasisi nyingi za Serikali uteuzi wake unakuwa sio wa wazi jambo linalopelekea kuwa hata uwajibishwaji wa watumishi hao na vyombo kama bodi zao unakuwa mgumu. Kambi ya Upinzani inalionna hili kuwa ni kasoro kubwa inahitaji kuangaliwa na hatimaye kuwa jambo la Kikatiba. Tunawaomba Watanzania watoe maoni kwenye mchakato wa kuandika Katiba Mpya kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kwamba, ili kujenga sekta ya umma inayowajibika ni lazima kuwa na mfumo imara wa *check and balance* kwa watendaji na taasisi zenyewe. Hili linatakiwa lianzie kwenye ngazi ya utoaji wa ajira kwa watendaji, hili litaondoa malalamiko ya

kupendeleana, undungu na mambo mengine ya aina hiyo yanayosababisha kuvunjika moyo kwa watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ya sasa haina upungufu wa watendaji wenyewe uwezo, lakini kuna tatizo kubwa katika taasisi zetu nyingi kwa watu ambao wamefikisha muda wa kustaafuli kuongezewa muda na kuendelea kufanya kazi kwa mikataba. Hii ni aina nyingine ya uhujumu wa rasilimali, kwa dhana kuwa tunazidi kupoteza rasilimali na nguvu kazi. Ni ukweli uliowazi kuwa kama umefikisha muda wa kustaafuli hakuna tija yoyote mtu anaweza kuiongeza kwa taasisi zaidi ya kupatiwa mwanya wa kuihujumu taasisi hiyo; tukumbuke kuwa tayari amekwishalipwa mafao yake yote kisheria. Kambi la Upinzani inasisitiza kuwa Serikali ipige marufuku mtindo wa kuongezeana mikataba wakati mtu kaishastaafu kwani inawanyima vijana fursa za kuonyesha vipaji na ubunifu wao jambo linalopelekea kwenda nje ya nchi kutafuta kazi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kunukuu mahojiano kati ya Mtaalam wa Utawala wa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Dokta Bana na Ndugu Andrew Schalkwyk, wa *Innovations for Successful Societies* tarehe 19 November 2008, Nanukuu:-

"Nchini, desturi daima imekuwa kwamba walioiteuliwa kwenye nafasi za makamishna wa utumishi wa umma... hawa ni watu waliostaafu...wastaafu ambao hawajachoka. Lakini unapoajiri mstaafu ili afanye kazi katika chombo muhimu kama Tume ya Utumishi wa Umma, kuna

tatizo... Watu hawa wamechoka... na watu hawa tayari wametimiza muda wao wa kisheria kustaaifu, hivyo hawawezi kutembelea maeneo yote ya nchi yetu". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, "Weberian principles. And secondly it confirmed those serving on probationary terms. It ensured that an employee was confirmed for service. And, essentially, it also ensured that certain categories of staff are promoted on time. And it dealt with disciplinary matters over certain cadres of staff. Those traditional functions have remained intact until today. Most of them have remained intact until today.

And in the country, the tradition has always been that those appointed to serve as the public service commissioners, or in the past civil service commissioners, these were basically retired individuals. I would say retired individuals who are not tired. But when you employ a retiree to serve in a very central organ like the Public Service Commission, there are some setbacks. SCHALKWYK: *Like what?* DR. BANA: *These guys are tired. This guy has reached the statutory retirement age. They can't travel all over the country*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni mtaalamu wetu lakini anaonyesha waziwazi kuwa mara nyingi mtu akiendelea kuongezewa muda wa kazi baada ya kustaaifu ni hakika kuwa utendaji wake unakosa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahusiano ya siasa na dini. Ofisi ya Rais, kupitia Wizara ya Mahusiano na

Uratibu ndiyo yenyekiti la kuangalia na kusimamia mahusiano mema kati ya Serikali na taasisi za dini na asasi za kiraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majumuisho ya hotuba ya Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi, Sera, Uratibu na Bunge akijibu hoja ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na udini, ukabila na ukanda kuingizwa kwenye siasa, alitoa jibu rahisi kuwa wale wote wanaolalamika ndio wanajihusisha na jambo hilo. Huu ni mzaha ambao unaweza kuhatarisha umoja na mshikamano wa nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingi katika Afrika na kwingineko ambako machafuko yametokea kwa kiasi kikubwa yamesababishwa na watu kutumia udini au ukabila katika siasa. Hivyo basi wahusika wakuu katika maeneo haya wanatakiwa kukumbushwa mara kwa mara wajibu na umuhimu wa kusimamia kwa dhati umoja na mshikamano katika taasisi wanazoziongoza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatari ya kuligawa Taifa sasa haiko katika siasa pekee, bali hata ndani ya dini zetu. Yanayowasukuma baadhi ya viongozi wetu wa dini kuendeleza na kukoleza vita hii ya ki-imani ni pamoja na udhaifu wa Serikali kukemea na kuchukua hatua stahiki kadri matukio yanavyojitokeza. Hata gazeti la leo la Mwananchi kuna habari kama hii, kwa hiyo hili ni suala zito sana. (*Makofii*)

Kuna ushahidi tosha vilevile kuwa baadhi ya viongozi wetu wa dini wametumiwa na kufadhiliwa na

watu mashuhuri wakiwepo wafanyabiashara wakubwa kwa niaba ya viongozi wa Kiserikali na Vyama vyatia Siasa kueneza propaganda hizi kwa malengo ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viro vyombo vyatia habari vinavyomilikiwa na taasisi za dini ambavyo wakati mwingine vimakuwa vikieneza uchochezi wa wazi dhidi ya dini nyingine bila mamlaka za Kiserikali kuchukua hatua stahiki. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tamko kukemea hali hii na iahidi ndani ya Bunge kutokuvumilia dini, kiongozi au muumuni yejete wa dini yoyote atakayeshindwa kuheshimu haki ya mwenye imani tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo chochote cha wanasiwa kutumia madhehebu au taasisi za dini ili kukidhi agenda zao za kisiasa ni jambo ambalo kama lisipotafutiwa ufumbuzi ni hatari kwa mustakabali wa uhai wa taifa letu. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa madhehebu ya dini yana haki zote za kuhoji na kushauri utendaji wa Serikali na kutoa mwelekeo wao ni upi katika yale wanayoona ni tatizo na kupongeza wanayoona kuwa yamefanywa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasilitiza ushauri ambao tumekuwa tukiutoa mara kwa mara kuwa sisi sote tuzingatie matakwa ya Sheria ya Usajili wa Vyama vyatia Siasa ya mwaka 1992 (Na. 8, kifungu cha 2) inayokataza Vyama vyatia Siasa kutetea au kuendeleza maslahi ya kidini, kikabila au kikanda. Kambi ya Upinzani inasilitiza aliyosilitiza Baba wa Taifa kwamba masuala ya udini na ukabila yanahitaji

usimamizi makini. Aidha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini wale wote watakaobainika kuwa wanafanya siasa kwa kutumia udini, ukabila na ukanda wachukuliwe hatua kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia matukio mbalimbali ya kuhatarisha amani ya nchi katika mahusiano ya dini na siasa wakati Sheria ya Usajili wa Vyama vya Siasa ilipoanzishwa mwaka 1992 iliweka wazi masharti ya Vyama vya Siasa ili kuweza kupata usajili na kuwa chama halali cha siasa, Sheria Na. 8 kifungu cha 2 nanukuu:-

"Without prejudice to subsection (1) of this section no political party shall qualify for provisional registration if by its constitution or policy— a) it aims to advocate or further the interests of - (i) any religious belief or group; (ii) any tribal, ethnic or racial group; or (iii) only a specific area within any part of the United Republic";

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa na hivyo kuvifuta vyama vyote vinavyotumia dini na udini kwani ni hatari kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais -Tume ya Mipango. Majukumu ya msingi ya Tume ya Mipango ni:-

- (a) Kutoa dira na mwongozo wa uchumi wa Taifa; na

(b) Kubuni sera za uchumi na mikakati ya mipango ya maendeleo ya Taifa pamoja na usimamizi wa uchumi na utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu tajwa hapo juu ni makubwa sana japokuwa rasilimali watu katika ofisi hiyo ni ndogo kukidhi majukumu hayo. Ni ukweli ulio wazi kuwa Tume hii ndiyo iliyotoa Dira ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango, pamoja na kazi hizo za msingi, inahitajika kufanya kazi ya kuhakikisha kuwa inatayarisha mkakati wa kusimamia utekelezaji wa mipango hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za randama zinaonyesha kuwa ina watumishi 122 wakati mahitaji halisi ni watumishi 174. Tatizo hili linapelekea ukwamishwaji au utendaji kazi katika hali ngumu sana, jambo hili linaweza sababisha mipango yetu iwe ya kinadharia zaidi badala ya kiuhalisia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Tume ya Mipango kwa mwaka wa fedha unaomalizika ilikuwa shilingi bilioni 8.039 na mwaka huu wa fedha imetengewa shilingi bilioni 8.007 ikiwa ni pungufu ya ile ya mwaka jana kwa shilingi milioni 32. Mbaya zaidi ni kwamba fedha zote zinazoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Tume ni fedha kutoka nje. Tunapaswa kukumbuka kuwa kwa sasa tuna tatizo kubwa la fedha za nje kutokutolewa kwa wakati, jambo ambalo linapelekea kucheleweshwa kwa utekelezaji wa mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia jambo hili la Tume kupewa mahitaji yake halisi ili ifanye kazi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo dosari mbili ambazo tulizitaja katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Bajeti ya Taifa kwa mwaka 2012/2013. Dosari hizo ni:-

(1) Mpango wa 2012/2013 haukuzingatia kwa ukamilifu Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano.

(2) Bajeti ya mwaka 2012/2013 haikuzingatia viwango na mgawanyo wa fedha kwa mujibu wa Mpango wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Tume ya Mipango, ambayo Mwenyekiti wake ni Rais, kurekebisha dosari hizi ili kuwezesha maendeleo ya haraka ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha na naomba hotuba yangu iingie kama ivyowasillishwa Mezani, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunapokea taarifa hii, sasa napenda kuwatangaza ambao wataanza kuchangia, kama tulivyotangaziwa tutaanza na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Abdallah na Mheshimiwa Kombo

Khamis Kombo ajiandae, pia Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu ajiandae, Mheshimiwa Mbilinyi!

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Napenda kuanza kwa kumshukuru Mungu kwa kila jambo, wakati huo huo nawashukuru wana Mbeya kwa *support* wanayonipa, wanantia nguvu ya kufanya kile ninachofanya na napenda nitumie fursa hii kuwaahidi kwamba tutakavyoanza ndivyo tutakavyomaliza kwa stahili ya nguvu ya umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitachangia zaidi kwenye masuala ya utawala bora ambao ndiyo msingi wa amani na utulivu na kwa kuanza kwa maslahi ya Taifa naomba nitoe rai kwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi hasa vijana, mnapopata nafasi ya kukaa na wazee wenu naomba tafadhali mtumie muda huo vizuri kuwaambia ukweli wazee kuhusu ni nini hasa kinachoendelea mtaani, kwamba mtaani watu hawana furaha na maisha. Acheni upambe wa kisiasa na fikra za kuwaza Uwaziri, ujumbe wa Bodi na kadhalika, wazee wenu wako *detached* ndugu zangu, ni jukumu lenu kuwaweka sawa na kuwasaldia kama tunavyofanya sisi bila kuangalia itikadi za Chama kila tunapopata muda wa kukaa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa nashangaa sana humu ndani vijana Wabunge wa CCM wanasmama wanampongeza Rais kwa kuteua Wakuu wa Wilaya, *are we serious?* Unampongeza Rais kwa kufanya majukumu yake, kesho utampongeza kwa kunywa

maji. Sasa basi si haki kumpongeza Rais kwa kutekeleza majukumu yake na hakika siamini kwamba huwa anapokea pongezi zenu, kabisa siamini kama huwa anapokea pongezi zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niendelee sasa kwenye masuala ya utawala bora ambao ndiyo msingi wa amani na utulivu. Leo nitazungumzia suala ambalo halipo Mahakamani, suala la kutekwa kwa ndugu yangu Daktari Stephen Ulimboka. Hili suala halipo Mahakamani na najua kwamba kesi ya Madaktari ipo Mahakamani, lakini suala la kutekwa Daktari Ulimboka halipo Mahakamani *unless* kutekwa huko ni sehemu ya mgogoro wa Madaktari na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Sasa basi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi naomba nikukumbushe kwamba uongee kwa uhakika kwani utakuja utakiwe kuthibitisha mambo haya. Ahsante. Endelea!

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Yaliyomkuta Daktari Ulimboka kutekwa ni mtiririko wa wallyoyakuta Wabunge wa CHADEMA akina Machemli kukatwa mapanga na huo unaonekana ni utamaduni mpya sasa wa kuendesha mambo katika Taifa letu. Leo hii nchi hii tunang'oa watu meno, tunang'oa kucha watu kwa koleo kwa kuwa tu wana msimamo tofauti na wanadai kitu ambacho wanaamini ni haki yao. Hii siyo sawa kwani binadamu anapigwa mpaka figo zinaacha kufanya kazi. Hili halikubaliki kwa sababu

tukilikalia kimya na inaonekana ni utamaduni mpya, basi kesho watamteka Sugu kwa kusema ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Ofisi ya Rais ndiyo kila kitu na ndiyo jungu kuu, hapa ndiyo sehemu yake ya kulisemea na kulikemea. Hicho mnachofanya na yejote anayefanya katika Mahakama ya Kimataifa *ICC* yaani *International Criminal Court* kinaitwa *torture* na adhabu yake ipo. Rais Bashir wa Sudan hakutumia Jeshi wala Polisi kwa yale anayotuhumiwa bali alitumia *janjaweed*, sasa inaonekana kama hapa kwetu sasa pia halitumiki tena Jeshi wala Polisi wa Taifa bali kuna *element za janjaweed* zinaanza kuteka watu ambao wanaongea ukweli katika Taifa hili, hilo halitakubalika na tutalikemea kwa maslahi ya Taifa na kwa maslahi ya amani

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi naomba ukae. Mheshimiwa Daktari Mary Nagu!

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni namba 68 inasema kwamba, Mbunge yejote ndani ya Bunge hawezি kuongelea jambo ambalo hana uhakika kama ulivyosema wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kama Waziri na kama Mbunge nasikitika sana Daktari Ulimboka kukutwa na matatizo yale, lakini vile vile kwa Kanuni ya 64 kwamba, kila Mbunge humu ndani ataongelea ukweli na jambo ambalo ana uhakika nalo. Naomba

Mheshimiwa Mbunge aliyejikuwa anazungumza sasa hivi aongelee mambo ambayo ana uhakika na mambo ambayo hapotoshi Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mbunge adhihirishe kauli yake.

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Waziri, kama nilivyoanza kuzungumza mwanzo kwamba Kanuni ya 64 (1)(a) naisoma: "Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli." Sasa kwa sababu Mheshimiwa Mbilinyi nilikutahadharisha mwanzo, lakini ukaona uendelee kujenga hoja yako. Nakuomba uthibitishe yale ambayo unayazungumza sasa hivi yaani unaliarifu Bunge, hiki ni chombo kikubwa sana na kama huna taarifa nacho, basi naomba ufute kauli yako.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Kwamba Daktari Ulimboka alitekwa na kuteswa, nina uhakika nalo na Tanzania nzima inalijua hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda wangu naomba unipe fursa sasa niendelee.

MWENYEKITI: Hapana, naomba uketi chini. Umesema ametekwa na *janjaweed*, naomba uwataje hao *janjaweed* kwa manufaa yetu ili Taifa hili, naomba mnyamaze. Kanuni ya 72 inawazuia kuongea bila ruhusa ya Kiti.

Ututajie *Janjaweed* ili Serikali ichukue hatua kwani Serikali nzima ipo hapa, iwashughulikie kwa suala hili la

aibu kwa Taifa letu kumteka na kumdhuru mtu ambaye ni raia wa Tanzania. Tanzania katika Katiba yake inasema kwamba, kila mmoja ana haki ya kulindwa maisha yake. Sasa naomba uwataje *janjaweed* ili washughulikiwe kwa taratibu za kisheria. Tafadhalii naomba uthibitishe ama ufute kauli yako.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo!

MWENYEKITI: Naomba ukae chini!

WABUNGE FULANI: Kaa chini!

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Kwani mnajua nataka kuzungumza nini?

MWENYEKITI: Nimetaka maelezo ya Mheshimiwa...

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani unajua nataka kuzungumza nini?

MWENYEKITI: Tusibishane, kaa chini!

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Kwani unajua nataka kuzungumza nini? Mwenyekiti naomba Mwongozo.

MWENYEKITI: Kwanza nimetaka maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Mbilinyi, kwanza kaa chini!

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Naomba mwongozo!

WABUNGE FULANI: Atoke nje!

MWENYEKITI: Mheshimiwa usije kuni-*provoke* maana yake nimewasikia, jana kwenye semina naweza kumtaja mtu hapa, anasema mnapotutoa nje tunapata umaarufu, sasa suala hili si zuri, tafadhali!

Mheshimiwa Susan Kiwanga nilimwambia alikiuka kubishana na Kiti juzi akasema, naomba nielezee halafu kwanza usibishane na mimi tafadhali.

Akasema mnapotutoa nje tunapata *credit*, sasa hii *tea politics* Watanzania hawahitaji, Watanzania wanataka tuwasemee kero ambazo zinawasumbua ili tupate usuluhisho. Sasa haturuhusiwi kuropoka. Kanuni ya 64(1)(a) inasema usilete taarifa ambazo huna ukweli nazo na kama una ukweli uthibitishe, nimetaka nipate uthibitisho *janjaweed* ni nani, tafadhali. (*Makof*)

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Tafadhali usibishane na mimi.

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Nimeomba Mwongozo.

MWENYEKITI: Naweza kutoa Kambi yote ya Upinzani kama mnakiuka mamlaka yangu, naomba mtii Kiti.

Mheshimiwa Mbilinyi tafadhali thibitisha na kama huna uhakika basi futa kauli yako.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umetoka nje ya *track*, *Hansard* zipo. Sikusema kama kuna *janjaweed* bali nimetoa mfano wa Rais Albashir wa Sudan ambavyo hakutumia majeshi rasmi ya Taifa lake akatumia *janjaweed* kwenda kushambulia *Darfur* na nikatoa mfano kwamba watu waliomshambulia Daktari. Ulimboka tumesikia wamekuja na silaha sasa kama wana silaha na siyo majeshi ya Ulinzi na Usalama, hao ni nani kama siyo *janjaweed*? Kwa hiyo, nilichofanya ni kutoa mfano na nimesema kwamba...

MWENYEKITI: Naomba ukae chini. Nadhani Mheshimiwa unatumia vibaya uhuru wa kujieleza humu ndani. Wewe mwenyewe unasema kwamba umesikia kwani maneno ya kusikia ni ya nini hapa? Tunataka utoe taarifa za uhakika, huwezi kuiambia Serikali unasikia, mambo ya mabarazani usilete humu ndani kwani hii ni sehemu moja kubwa sana ya nchi yetu. Naomba mheshimu Bunge tafadhali, kama huna uhakika tafadhali usiongee kuhusu kusikia watu wenye silaha, huna uhakika tafadhali.

TAARIFA

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Kaa chini, Mheshimiwa Mbilinyi naomba uendelee kuchangia.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniruhusu niendelee, lakini natumaini uta-save muda wangu ambao umepotea.

Mimi ninachosema ni kwamba, yeote aliyejusika na suala la Daktari Ulimboka aache ku-*terrorise this nation* huku tukiendelea kuimba wimbo wa amani na utulivu na iundwe Tume ya Bunge kama Tume ya Daktari Mwakyembe ya *Richmond*, iundwe Tume huru ya Bunge ikiwezekana ili ichunguze suala hili kwa sababu Serikali haiaminiki katika hili, kwani kuna *complications*.

MWENYEKITI: Naomba ukae chini! Suala la Ulimboka kama huna uhakika nalo tafadhali zungumza hoja nyingine, lakini suala la Ulimboka usiendelee nalo kama huna uhakika nalo

Mheshimiwa Tundu Lissu, usibishane kwani hapa siyo sokoni, tafadhali kaa kimya. Mheshimiwa Mbilinyi kama huna uhakika tafadhali naomba ufute kauli yako ama ongelea suala lingine uendelee na mchango wako, *otherwise* naita mchangiaji mwingine aendelee kama huna hoja nyingine.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Nina uhakika kwamba nahitaji Tume huru kwa ajili ya kuchunguza suala la Daktari Ulimboka, hilo nina uhakika nalo na katika hili Serikali haitaaminika, hivi ndivyo nilivyotumwa na wana Mbeya niseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa faida ya amani na utulivu, sasa nahama nakwenda kwenye

Tume ya Maadili. Naunga mkono hotuba ya Upinzani kwamba Tume ya Maadili sasa iwe wazi zaidi pale inapotuchunguza viongozi. Wakija kutuchunguza wawe na mfumo wa kuhakikisha kwamba taarifa zinawafikia wananchi juu ya nani anamiliki nini na chanzo cha fedha ni nini kwa sababu sasa hivi kumekuwa na *too much myths* mtaani, kuna minong'ono mingi mitaani na *rumours*, ni chanzo cha kuvuruga amani hasa pale ambapo wananchi wanakosa kupata maelezo ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limetokea suala la nyumba ya Maige hapa ya dola 400,000 wakati mimi nakwenda Dar es Salaam nimesimamishwa na vijana pale Chalinze, wamenizunguka, wanasema Mheshimiwa nini nyumba ya Maige dola 400,000, twende tukupeleke Msoga ukaone lkulu binafsi ya Mkuu, wengine wanasema sijui kuna *airport* binafsi, wengine wanasema kuna mitaa na kadhalika. Sasa hizo zote ni *myths* ambazo kama hatutazi-control/kama Taifa zitatuyumbisha, Usalama wa Taifa, TAKUKURU, Tume ya Maadili na kadhalika wafanye kazi yao ili wananchi wawe wanapata taarifa za kutosha kuhusu viongozi wao kuondoa manung'uniko ambayo yanavuruga amani na kuondoa *morale* ya wananchi katika Taifa hili.

Sasa basi, sitaki kuamini hayo mambo kwani hayo mambo tulikuwa tunasikia zamani wakati wa akina Mobutu sijui kajenga kasri la vyumba 100 kijijini kwao Gbadolite na kadhalika, ndiyo hizo stori tulikuwa tunazisikia. *Perception* ya watu iko hivi, Nyerere katawala hii nchi miaka 24, kaondoka hana kitu mpaka

kajengewa nyumba na Jeshi, wanashangaa wanapoona vitu vya ajabu. Mimi sijaviona, lakini mamlaka zinazohusika sasa ni jukumu lao kuondoa hizi *myths* ambazo zipo mitaani kwa watu kwa faida ya amani na utulivu. Serikali iweke wazi mishahara, mafao na kila kitu cha viongozi wote akiwemo Rais na ijulikane wazi ili kutoa fursa kwa wananchi kuoanisha kipato halisi cha viongozi pamoja na mali halisi wanazomiliki na hii ni kwa faida ya amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, siungi mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Nakushukuru, naomba kumwita sasa Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo ajiandae.

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni *Chief Whip*, kama unamruhusu *Chief Whip* wa Serikali *surely in a Multiparty Parliament, you can not ignore the existence of the Opposition Chief Whip*.

MWENYEKITI: Aliyeku-*allow* kuzungumza kabla ya kuruhusu mimi ni nani? Naomba ukae chini!

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Nimeomba Mwongozo!

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kuwepo hapa. Lakini pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Tumbe nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa akitoa majumuisho yake tarehe 29/6/2012 alisisitiza juu ya uwajibikaji na kuzuia matumizi yasiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli Serikali imedhamiria kuzuia matumizi yasiyokuwa ya lazima kwa lengo la kuleta au kuongeza fedha za Serikali, Wizara hii kupitia Ofisi ya Utawala Bora imshauri Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwanza apunguze matumizi katika Ofisi yake na ndiyo Wizara nyingine ziweze kufuatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii nimweleze Waziri katika Ofisi ya Utawala Bora amshauri Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwanza apunguze ukubwa wa Serikali yake. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watu wameelezea kwamba ni kubwa mno, kwa maana hiyo kuna haja ya kupunguza ukubwa wa Serikali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, Kenya ina Mawaziri 15 na wenzetu Msumbiji karibu tu hapo wana Mawaziri 26 lakini Tanzania ina Mawaziri 31 na Naibu Waziri 26, ina Makatibu Wakuu 26, ina Manaibu Katibu Mkuu pia 26 kama sikosei. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba ukubwa wa Serikali yote hii ndiyo inayochangia kutumia vibaya fedha za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja ya kuunganisha baadhi ya Wizara zile ambazo zina

maeneo yanayolingana. Kwa mfano, Kenya kuna Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na hii ni Wizara moja lakini hapa kuna Wizara ya Elimu ambayo ina Waziri wake na Sayansi na Teknolojia ina Waziri wake. Kwa hiyo, nadhani hapa kama hii itakuwa ni Wizara moja tunaweza tukabana matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutafanya hivyo tutapunguza gharama za pango au majengo, tutapunguza gharama za ofisi, gharama za magari, gharama za uendeshaji, gharama za wafanyakazi na mambo mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mheshimiwa Rais kupunguza Baraza la Mawaziri kinachofuatia ni ufanisi wa Mawaziri wale. Kwa Tanzania tunategemea baada ya kuchaguliwa Baraza la Mawaziri kuwe na ufanisi wa utendaji kazi na kwa uzoefu tulionao ni kwamba ufanisi huu ni mdogo sana. Kwa nini nasema hivi? Nasema hivi kwa sababu kipindi kilichopita cha awamu ya Mheshimiwa Rais alilazimika kubadili Baraza lake la Mawaziri na hii ni kwa sababu tu kulikuwa hakuna ufanisi katika utendaji wa kazi. Pia kipindi cha pili alilazimika kufanya hivyo hivyo kwa sababu ilikuwa hakuna ufanisi wa utendaji kazi.

Sasa nashauri kwamba, Mheshimiwa Rais lazima aingie mikataba ya utendaji na Mawaziri ili baada ya muda anawaita Mawaziri wale kuweza kujua kila Waziri ametekeleza vipi bajeti yake, matumizi yake yamekuwaje na amekwama wapi. Hili litasaidia kwa kiasi kikubwa kuleta ufanisi wa utendaji kazi katika Serikali yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya ni lazima tuzingatie utawala bora. Utawala bora ni jambo muhimu katika Taifa letu la Tanzania. Utawala bora ndiyo unaleta nidhamu katika matumizi ya kodi za wananchi, nidhamu katika ukusanyaji bora wa mapato na ufanisi wa maadili ya kazi. Lakini pia utawala bora ndiyo unaleta haki na usawa mbele ya sheria. Kama utawala bora utayumba basi Taifa litapoteza dira na mwelekeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba sasa wakati umefika kwa Wizara hii kujua tatizo ni nini hasa. Nikifanya majumuisho ya mazungumzo ni kwamba, kwanza baada ya Mheshimiwa Rais kupunguza Baraza lake la Mawaziri aje katika ufanisi wa utendaji kazi, lakini baadaye asimamie utawala bora. Tukiweza kuyamudu haya yote basi nadhani huko tunakokwenda tutakwenda katika njia ya mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika suala la uhamisho kwa wafanyakazi. Uhamisho kwa wafanyakazi ni jambo la kawaida, lakini linatumika vibaya. Linatumika kwa kukandamiza mfanyakazi mwingine, linatumika kwa kutoridhia maelezo ya mwajiri. Kwa hiyo, unapotaka kumhamisha mfanyakazi ni lazima uzingatie kuwa mfanyakazi anahitaji achunguzwe na halafu aonekane kwamba, anapata haki zake zote za uhamisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme kwamba, kuna suala la ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa. Kabla ya kumwita mchangiaji anayefuata, naomba nimuite Mheshimiwa Tundu Lissu, tafadhali!

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaomba Mwongozo niliokuwa nataka kuutoa, naomba niweke masikitiko yangu katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge kwa jinsi ambavyo mimi kama Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Upinzani nafikiri hatutendewi haki humu ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani nina cheo sawa na Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa eleza hoja ambayo unayo, sasa hotuba ya nini? Elezea *issue*.

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Nilisema niweke haya malalamiko kwenye *record* kwa sababu ninaposimama hapa nina hoja naomba nisikilizwe, halafu hoja yangu ikataliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *any way* naomba niombe Mwongozo wako kuhusu maelekezo ambayo umempa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kwamba,

athibitishe kauli yake kuhusiana na kutekwa nyara na kuteswa kwa Daktari Ulimboka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ambayo umeisema wewe mwenyewe na Kanuni aliyoisema Mnadhimu wa Kambi ya Serikali ni Kanuni ya 64 (1) (a) ya Kanuni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni inayohusika na inayokipa Kiti chako mamlaka ya kumwelekeza Mbunge athibitishe kauli yake ni Kanuni ya 63 fasili ya (6)...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lissu isome Kanuni ya 64(1) (a), hebu isome inasemaje.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Inasema hivi: "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli".

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. Sasa kunapokuwa na hoja kwamba, Mbunge amesema uongo kinachotakiwa cha kwanza kabla hajaambiwa athibitishe kauli yake sijui kama nasikika maana yake Mheshimiwa na wewe umewasha *microphone* yako!

MWENYEKITI: Unasikika, endelea.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Kinachotakiwa kabla Mbunge anayetuhumiwa kusema uongo hajaambiwa

au aifute kauli yake ni yale yaliyoko katika Kanuni 63(4) inayosema kwamba: "Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa fasili ya (3) ya Kanuni atakuwa na wajibu wa kutoa na kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge".

Kwa hiyo, yule aliyetoa hoja kwamba, Mheshimiwa Mbilinyi ametoa kauli ya uongo, kabla ya Mheshimiwa Mbilinyi hajatakiwa kuthibitisha kauli yake au kuifuta, huyo alitakiwa atoe huo uthibitisho chini ya Kanuni ya 63 (4), ili akiishatoa uthibitisho huo, huo mpira wa kuthibitisha ukweli unamrudia sasa mzungumzaji wa kwanza Mheshimiwa Mbilinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba utupe Mwongozo kama hayo maelekezo yako kwa Mheshimiwa Mbilinyi ya kuthibitisha kauli yake juu ya kutekwa nyara kwa Daktari Ulimboka ni sahihi wakati huyo aliyedai ni uongo hajathibitisha uongo huo kwa mujibu wa Kanuni ya 63 (4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu Kanuni hii tullyolsoma ya 64(1)(a) ambayo inazuia kuzungumza kitu ambacho huna ukweli, unajaribu kuipinga kwa maslahi yako kwa kweli unapotosha Watanzania, usitake umaarufu hapa.

Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, tafadhali endelea!

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini naomba niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mgogoni na nahakikisha kwamba, ninachokisema nakisema kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la wafanyakazi hewa. Karibuni wakati nikitoa mchango wangu nilizungumzia suala zima la wafanyakazi hewa na leo nasema kwamba, suala hili lina mtandao mkubwa kuanzia Hazina mpaka zinapofikia fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Tanzania wanataka kujua fedha hizi ambazo zilikuwa zikitolewa kwa ajili ya mishahara ambayo ilikuwa ikisemekana wanapewa wafanyakazi lakini fedha hizi zilikuwa haziwafikii kwa sababu hawapo, Watanzania wanataka kujua zimepelekwa wapi. (*Makofi*)

Fedha hizi Watanzania wanataka kujua upotevu wake ulianzia wapi, zilipelekwa wapi na nani aliyehusika katika kuzipeleka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala ambalo ni baya sana na upotevu huu umepoteza mabilioni ya shilingi za Watanzania. Ni wajibu wa Serikali kuliundia Tume suala hili ili liweze kupatiwa ufumbuzi wa kufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la wafanyakazi wanaoajiriwa. Nashukuru kwamba hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri lilisemwa. Lakini vile vile kuna uzoroteshaji wa wafanyakazi hawa wanaoajiriwa katika kulipwa mishahara yao. Serikali ina

wajibu mkubwa sana wa kujua kwamba, tumeajiri watu wangapi na vilevile wawe na udhibiti wa kuweza kuwalipa mishahara yao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Wafanyakazi wanafikia miezi miwili mpaka sita hawajalipwa mishahara yao na hivyo kupelekea kwamba watu hawa ni matapeli wanaotapeli hata familia zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la kuundwa Sekretarieti ya Maadili kwa Viongozi wa Umma. Katika hili nasema kwamba, viongozi wa umma wasiundiwe Sekretarieti peke yao. Kuna wafanyakazi ambao si mionganoni mwa viongozi wa umma, lakini wanavuruga fedha kuliko hata viongozi wa umma. Leo si ajabu kumkuta mfanyakazi baada ya miaka miwili tu ananyanya majengo ya ghorofa zaidi ya moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie, leo tunaambiwa kuna trilioni za shilingi ziko Uswisi. Hizo zilipaswa zichunguzwe zimefikaje huko? Sasa kuna Wahasibu ambao siyo waadilifu. Kuna Makatibu Wakuu ambao wengine siyo waadilifu. Kuna Naibu Wakurugenzi ambao siyo waadilifu. Pia Taasisi nyingine zinazokusanya fedha na hata hawa watu wa *TRA* wachunguzwe na wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni upandishaji wa vyeo. Serikali katika hili isiangalie watumishi au watendaji wake kwa misingi ya vyama au mtu anapotoka. Mtu anapaswa kupewa cheo kama

mtumishi kwa mujibu wa uwezo wake, si kwa sababu anatoka mahali fulani au ana mkubwa fulani. Hili niseme kwamba, lina malalamiko pande nyingi sana na watu wanallalamikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la Wizara ya mambo ya Nje. Rais wetu tunataka awe wa Watanzania, asiwe Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje. Ameteua Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje ili afanye kazi za Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje. Rais anapoondoka kwenda nje kutakuwa kuna mamilioni ya fedha ambayo yanatumiwa na *delegation* ambayo anaondoka nayo. Kwa hivyo, kazi yake tunataka mara nyingi awepo nchini ili tumtumie Rais wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza!

MWENYEKITI: Ya pili.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Alaa!

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mohamed Mnyaa. Mheshimiwa John Mnyika ajiandae na Mheshimiwa Rajab Mbarouk

ajiandae. Mheshimiwa Mnyaa hayupo, Mheshimiwa John Mnyika tafadhali!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais kwa mwaka wa 2011/2012 na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Nchi yetu Ibara ya 62, Bunge letu lina sehemu mbili; sehemu ya kwanza ni Rais na sehemu ya pili ni Wabunge. Kwa mujibu wa Katiba pia, Ibara ya 63(2) sehemu ya pili ya Bunge ambayo ndiyo sisi Wabunge ndiyo ambayo ni Chombo Kikuu cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambacho kina madaraka kwa niaba ya wananchi kuishauri na kuisimamia Serikali katika mambo yote yanayohusu utekelezaji wa Katiba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba hii vile vile katika Ibara ya 33 inayounda na kutoa majukumu na madaraka kwa Ofisi ya Rais imetaja kuanzia Ibara ya 33 mpaka Ibara ya 50 kutokana na muda sitakwenda kwenye vifungu mahsus, lakini Rais ndiye Kiongozi Mkuu wa Serikali, ndiye Amiri Jeshi Mkuu na kimsingi watendaji na watumishi wote wa umma wanafanya kazi kwa niaba yake. Ibara ya 37 ya Katiba yetu inatamka kwamba, katika kutekeleza majukumu hayo Rais halazimiki kufuata ushauri wa mtu ye yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mujibu wa Katiba hii hotuba ya bajeti ya Rais tunayojadili leo ni

bajeti muhimu na nyeti sana. Sasa katika kufanya mapitio ya utekelezaji nieleze tu maskitiko yangu kwamba, yale ambayo tuliyachangia mwaka jana kwenye Mkutano wa Bunge la Bajeti kwa maneno na mimi binafsi nilichangia hotuba hiyo tarehe 5 na kwa maandishi, kwa kiwango kikubwa sana hayajatekelezwa. Sasa kwa sababu hakuna utekelezaji ndiyo maana Wabunge tunaamua kwa dhati kabisa na Serikali ituelewe katika hili, kuzungumza kwa lugha ya ukali isiyo ya kidplomasia ili Serikali ielewé kwamba, hatuko tayari na wananchi waliotutuma hawako tayari kwamba kuchelewa kwa miaka 50 ya Uhuru kuwe kuchelewa kwa miaka mitano ambayo wametutuma kuja kuwawakilisha. Tunataka kwa niaba ya wananchi waliotutuma Serikali ifanye kwa nguvu zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme machache sana yanayohusu Ofisi ya Rais ambayo ina Wizara tatu nyeti, Wizara ya Utumishi, Wizara ya Uhusiano na Uratibu na vilevile Wizara ya Utawala Bora ambayo ina Taasisi nyeti sana; ina TAKUKURU, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Idara ya Usalama wa Taifa, Sekretarieti ya Ajira na Tume ya Ajira na Vyombo vingine vikubwa sana vyenye mamlaka makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwaka mmoja umepita Serikali tangu ituahidi mwaka uliopita kwamba masuala haya ya uchunguzi wa kashfa kubwa za rushwa za Kagoda, MEREMETA, za *Deep-green* na nyinginez. Sasa ingefika hatua ya kueleza mafanikio, lakini ukipitia katika hotuba hizi hatuelezwi ni akina nani

wamekamatwa kwa kashfa kubwa, mwaka mmoja umepita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Ofisi hii inahusu Amiri Jeshi Mkuu na Kiongozi wa Shughuli za Serikali, tunapata mashaka Waheshimiwa Wabunge kwamba upo uwezekano pengine hivi Vyombo vyta Uchunguzi vinatoa ushauri, lakini kwa kuwa, Katiba inasema Rais hawajibiki kufuata ushauri wa mtu yeote inawezekana ushauri huu unapuuzwa. (*Makof*)

Sasa Ofisi ya Rais kwenye majumuisho ituoneshe kwa vitendo ni kwa vipi Ofisi ya Rais inashughulikia udhaifu wote ambao Waheshimiwa Wabunge tunausema na tunaendelea kuusema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwa sababu vile vile ya mambo yanayohusu Jimbo la Ubungo ambalo ni la wananchi walionituma kuwawakilisha humu ndani ya Bunge. Ofisi hii tunayoijadili inahusu Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Ikulu. Katika Mkutano uliopita wa Bunge nililalamika sana kuhusu mgao wa fedha nyingi kwa upande wa Ofisi hii wakati ambapo Miradi ya Maendeleo imepewa fedha kidogo. Maelezo ambayo yalitolewa wakati ule ni kwamba Ofisi hii inatakiwa ipewe fedha nyingi kwa sababu ya kuongeza nguvu zake kwenye kusimamia Ofisi nyingine zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafahamu kwamba, kwenye Baraza la Mawaziri kulipitishwa Mpango wa haraka wa maji Dar es Salaam wa bilioni

600 na Ofisi ya Rais ikatoa kauli kwamba mpango huu ungetekelezwa ifikapo mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nasikitika Tume ya Mipango ambayo Rais ndiyo Mwenyekiti wake imekaa Mkutano na kuleta Mpango wa Mwaka wa Serikali unaokinzana na Mpango wa Miaka Mitano na nimeeleza kimaandishi katika mchango wangu wa maandishi kiwango gani cha fedha kilipaswa kutengwa mwaka huu kimepitishwa na Bunge hakikutengwa, kiwango gani cha fedha ambacho Bunge lilipaswa kuwa limeletewa cha barabara za pembezoni za Dar es Salaam zilipaswa kuwa na bilioni 100 lakini zimeletwa bilioni 10 peke yake kinyume kabisa na Mpango ambao Mwenyekiti wa Tume ya Mipango ni Rais, Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri ni Rais. Kwa hiyo, nawaomba sana Ofisi ya Rais ifikishe ujumbe huu vizuri zaidi na tofauti na mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ipo katika matatizo, sasa hivi walimu wametoa *notice* ya kutaka kuanza kugoma, muda mfupi kabla ya kuingia hapa nimetazama *ITV* Madaktari Bingwa wametangaza kugoma na Ofisi tunayojadili, Ofisi ya Rais, Utumishi ndiyo wenge dhamana ya Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nitaomba maelezo kutoka kwa Serikali kwa sababu madai ya walimu, kuna mambo ambayo nasikitika kwamba tumefika hatua Bunge limepotoshwa humu ndani na Naibu Waziri ametoa taarifa zisizokuwa za kweli. Ni wakati wa Ofisi ya Rais ambayo ndiyo inayosimamia Mawaziri kuingilia kati tuletewe taarifa za kweli Bungeni

kuhusu madai ya walimu na nini ambacho walimu walikubaliana na Serikali majadiliano yakiongozwa na Ofisi ya Rais, tuletewe taarifa za kweli na Bunge hili ndilo lenye wajibu wa kuisimamia Serikali. Tuletewe taarifa ya Kamati ya Bunge ya Huduma ya Jamii iliyokutana na pande mbili, iliyokutana na Madaktari, iliyokutana na Serikali ili Bunge lifanye kazi yake sasa ya kuisimamia Serikali kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani wananchi wanakufa, maana kuna migomo mingi, kuna migomo ya moja kwa moja na kuna migomo baridi, leo wanafunzi wanafeli kwa ari, kasi na nguvu zaidi kwa sababu walimu wapo kwenye mgomo baridi, wamefikia hatua hata Vyombo vyetu vya Ulinzi kuanza kujiuliza Wahabeshi wanakujaje kufariki wakiwa ndani ya Tanzania, majangili wanafanyaje yote haya, ni kwa sababu hata Askari wetu wana manung'uniko. Serikali ilitoa kauli hapa Bungeni kwamba Askari Polisi wangeongezewa posho kutoka 100,000 mpaka 150,000, toka kauli hiyo itolewe Askari hawajalipwa hizo posho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais itambue walimu wana uwezo wa kujitokeza na kusema kwamba wanagoma, Madaktari wana uwezo wa kujitokeza na kusema kwamba hawaridhiki, lakini Askari wetu, Magereza, Askari Polisi, wenye malimbikizo ya madeni toka mwaka 2009; madeni mbalimbali ya posho na ya mishahara, kundi kubwa la Askari wanadai na kwa sababu hawawezi kujitokeza, wanalamika chini kwa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais inayo wajibu wa kuiongoza Serikali, kuepusha nchi hii na hali tete na wajibu huo haupaswi tu kuwa nje ya Bunge, maana tunazuiwa ndani ya Bunge, wajibu huo uletwe hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makofi*)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya kitu ambacho kinaleta maendeleo katika nchi tukiachilia mbali watu, ardhi, siasa safi, lakini ni uongozi bora. Uongozi bora kwa maana ya Utawala Bora, Wizara ya Utawala Bora ni Wizara ambayo ina nasa kila sekta katika nchi hii. Nimepatwa na wasiwasi sana kwamba katika nchi hii suala la Utawala Bora ni suala ambalo hatutaki kwa njia moja ama nyingine kujua kwamba ndiyo mzimu ambao unalikwamisha Taifa hili kuendelea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitegemea kwamba Wizara ina Mawaziri watatu tusikilize mambo ya Utumishi, tusikilize Mipango, lakini vilevile tuweze kumsikiliza Waziri mhusika anatueleza namna gani Serikali imejipanga katika suala nzima la Utawala Bora. Tulitegemea hapa Waziri atueleze katika suala la Utawala Bora kuhusu viapo ambavyo Waheshimiwa wanaopewa nafasi ya kuongoza nchi hii wanakula na namna gani wanavyovikiuka na ni namna gani baada ya kuvikiuka Serikali inachukua hatua, hili hatukulisikia.

Tulitegemea kwamba tusikie maadili lakini imezungumzwa tu kiujumla jumla, maadili kidogo kidogo tu hatukuweza kumsikia Waziri akitwambia kwa undani suala zima la maadili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mmoja, juzi Serikali ya Uingereza iliunda Tume ya Maadili au kwa kutumia Chombo chake cha Tume ya Maadili kuichunguza *Barclays Bank* ambayo ilifanya makosa ya kimaadili katika utendaji kazi. Hapa *CAG* aliainisha moja ya tatizo tulilonalo katika nchi yetu, watendaji wa Halmashauri kushirikiana na wafanyakazi wa Benki katika kuiba fedha za maendeleo. Tulitegemea tumsikilize Waziri anayeshughulika na Utawala Bora hili analizungumzia namna gani?

Tunajua kwamba hawa watendaji wa Halmashauri, hizi fedha zinapoingia benki wanachelewesha maendeleo makusudi, mikopo ya wanafunzi inapopelekwa wanaichelewesha makusudi. Leo watoto wetu wamageuka kuwa malaya hatari kwa sababu ya kukosa kupata mikopo. Utawala Bora umekaa tu. Jamani nilitegemea sana Mheshimiwa George Mkuchika asimame hapa leo tusikie nini anazungumza, kazungumzia Wizara nyingine, bahati mbaya japokuwa ipo katika mlolongo huo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitegemea Waziri mhusika atueleze namna gani Serikali ipo *transparency*, lakini leo kila kitu kinafungwa fungwa tu. Tulitegemea Waziri wa mambo ya Utawala Bora atueleze *commitment* ya Serikali, hatukuweza kuyapata, tumepata mambo kiujumla jumla tu. Tulitegemea

Waziri atueleze namna gani ya ushirikishwaji wa wananchi kujua mipaka yao, ijlukane hii ni mipaka ya uongozi na hii ni mipaka ya wananchi hayo hatukuyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitokuwa mbaya na naamini sitoeleweka vibaya kama nitasema kwamba suala la Utawala Bora katika nchi hii *is ghost of dead* kabisa kabisa, ni mzimu wa mauti. TunapodharaU suala la utawala bora maana yake ni kwamba tumeua kila kitu ndani ya nchi hii, hatuna ambacho tutaweza kukifanya katika nchi hii kwa kudharau utawala bora. Leo tunasikia nchi imeja migogoro, kuna migogoro ya Walimu, kuna migogoro wa wanafunzi, kuna migogoro ya Madaktari, migogoro ya watu wenye mabasi na SUMATRA, migogoro ya watu wenye mafuta yaani ni migogoro tulitegemea Waziri anayeshughulikia masuala ya Utawala Bora atasimama hapa ili atueleze hali halisi ya nchi hii inavyokwenda, lakini bahati mbaya hayo hatukuweza kuyasikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la TAKUKURU. TAKUKURU tumeona wametengewa fedha, lakini hatukuweza kuambiwa hivi, hii TAKUKURU tangu ianze mafanikio gani wameweza kuyapata. Kwa sababu kilichooneshwa pale ni takwimu tu kwamba wamechunguza kesi fulani, robo yake ndiyo wameweza kuzitekeleza, kwa nini hizi nyingine wameshindwa kuzitekeleza, zina uzito gani, zina ukubwa gani? Leo fedha zinotoroshwa kwenda nje, tunasikia hapa watu wa madini wafanya wanavyopenda, lakini suala la nini kitafanyika, hatua gani itachukuliwa, hatukusikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waziri anayehusika na Mambo ya Utawala Bora, juzi aliongea katika Vyombo vya Habari, nafikiri alijua kwamba leo hatapewa nafasi na Serikali hapa kuweza kuzungumza, akaamua kuongea na Vyombo vya Habari juzi kupitia Gazeti la Mtanzania la tarehe 30 Juni, 2012, alisema kwamba moja kati ya vitu vya kujisifia katika Utawala Bora Tanzania ni Muungano. Mheshimiwa Waziri unaweza kusimama kweli ukajisifia kwamba Muungano ni moja ya mafanikio wakati Muungano wenyewe umejaa migogoro sasa hivi! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi kubwa la hawa ambao mmeungana nao wanasema hawautaki Muungano sasa utawafanya nini? Hebu tuwe wa wazi. Nafikiri Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia haya masuala ya Utawala Bora aje apewe nafasi.

MWENYEKITI: Ongea kupitia kitu.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa na nia ya kutaka kuunga mkono bajeti ya Wizara hii, lakini kwa kweli nataka nichukue nafasi hii kuwashawishi na wenzangu kwamba kuna kila sababu ya kutoiunga mkono bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Nakushukuru. Namwita sasa Mheshimiwa Rosweeter Kasikila na Mheshimiwa Jitu Soni ajiandae na Mheshimiwa Moses Machali ajiandae.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu. Lakini pia nimpongeze Waziri na Timu yake kwa hotuba hii ambayo kwa kweli ina matumaini makubwa kwa wafanyakazi wa Rukwa, lakini kwa Watanzania wote. Kabla sijaendelea naomba kuiunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea kwanza niwakumbushe wananchi wa Rukwa kwamba tarehe 26 Agosti, 2012 kutakuwa na zoezi la kuhesabu watu na makazi. Kwa hiyo, naomba ndugu zangu Wanarukwa wote asibaki hata mmoja bila kuhesabiwa. Kwa sababu tusipohesabiwa wote, basi hata Serikali itakuwa na mkanganyiko wakati wa kutugawia fedha huko Mkoa wa Rukwa ikiwa ni pamoja na madawa. Naomba kila mmoja ajitokeze na tukumbushane kila mmoja ahesabiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naona nitachangia maeneo matatu, kuhusu upungufu mkubwa wa wauguzi na kada nyingine za afya kwa Mkoa wa Rukwa, lakini pia nitachangia juu ya Kurugenzi ya Wauguzi yaani nursing, *directorate* pale Wizara ya Afya, lakini pia nitachangia Wauguzi na changamoto wanazopata kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na upungufu wa Wauguzi Mkoa wa Rukwa, hakuna asiyefahamu kwamba watumishi wengi wanapomaliza vyuo wanapopangiwa Mikoa ya pembezoni na hasa Rukwa

wengi hawaendi na wale wanaokwenda wakifika wakichungulia tu wanarudi. Hali hiyo imepelekekea kuwa na wauguzi wachache sana katika Mkoa wa Rukwa na kwa kuwa na Wauguzi wachache katika Mkoa Rukwa vifo vya akinamama vinavyotokana na uzazi vinakuwa ni vingi sana, lakini pia na vifo vya watoto wachanga.

Kutokana na hali hiyo tumeona kwamba pengine Serikali inaweza isichukue hatua za haraka kwa ku-*alleviate situation* hiyo. Kwa hiyo, tumejiwekea mikakati tukaona tuweze kutafuta namna ya kuzalisha Wauguzi na wafanyakazi wa Idara ya Afya sisi wenyewe kule Mkoa wa Rukwa. Kutokana na hilo tukawa tumefanya juhud, tumbahatisha kuwapata wawekezaji au wafadhili kutoka Italia na wawekezaji hawa mwezi Mei, 2012 walikuwa wamefika, wamekwenda mpaka Sumbawanga wameona *site* ya kujenga hicho chuo na wakawa wamesema kwamba hawatajenga kile chuo ambacho tulikuwa tumewaomba sisi, ni cha hadhi ya chini badala yake watajenga Chuo Kikuu cha Wauguzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwatambua au kwa kupitia Mwenyekiti kuwashukuru hao wawekezaji ambao walikuwa wamekuja Sumbawanga. Daktari Francesco Ricci, Profesa Mario Di Gioacchinono, Profesa Dante Tatone, yeye huyu ni *Administrator*, Profesa Nicola Tinari na Engineer Leo Okoroafor ambaye ni Mnaigeria ambaye alipata *Citizenship* ya Italy. Kwa kweli tunawashukuru kwa sababu wameonesha juhud kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipowapeleka *s/ite* mahali pa kujenga hiki chuo kikuu wakasema kwamba mbona hiki chuo kitakuwa mbali sana na hHspitali ya Mkoa itakuwaje *practice* kwa wanafunzi. Lakini namshukuru Mheshimiwa Stella Manyanya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa akawaambiwa kwamba tuna mpango wa kujenga Hospitali ya Rufaa hapo hapo. Kwa hiyo, wakasema kama wanajenga Chuo Kikuu *wata-take care* na hospitali ya Rufaa kwamba wanakwenda kujenga na ujenzi unaanza mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyasema haya kwa sababu hii ndiyo *PPP*, naomba Serikali iweze kutoa kibali, iweze kuidhinisha mapema sana ujenzi wa Hospitali ya Rufaa kule Rukwa pale Wilaya ya Sumbawanga. Nina imani chuo hiki kitawasaidia sana wananchi wa Rukwa, lakini siyo wa Rukwa tu na nchi nzima ya Tanzania. Kwa sababu walipozungumza wanasema hakitakuwa Chuo Kikuu kitakuwa na hadhi ya Kimataifa. Nina hakika watu wengi watanufaika, lakini wagonjwa ambao wamekuwa wakipelekwa rufaa Mbeya, nao haitakuwa tena safari ndefu ya kwenda kutibiwa Mbeya ni mbali, wataweza kutibiwa pale pale Sumbawanga na hata Mkoa wa Katavi nao unakwenda kunufaika na Hospitali hii ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na baada ya kuiomba Serikali kutuidhinisha au kutupa kibali cha kujenga hiyo Hospitali ya Rufaa, naomba sasa nizungumzie kuhusu Kurugenzi ya Wauguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia hii *Organization Structure* ya *Ministry of Health and Social Welfare*. Ukiangalia *Organisation Structure* hii, it is so unfriendly kwa Wauguzi. Ukisoma hapo juu kuna Waziri, halafu kuna Katibu Mkuu, ambaye chini yake kuna Vitengo mbalimbali vinavyoitika kwa Katibu Mkuu. Baada ya hapo, kuna *Chief Medical Officer*, ambaye chini yake kuna Kurugenzi tano ambazo zote hizi zinakuwa headed na Madaktari, *Doctor of Medicine*. Ukiangalia katika Kurugenzi moja ya *Quality Assurance*, kuna Kitengo cha chini kabisa hapa wameandika *Nursing Services Section*; this is so unfriendly kwa Wauguzi, hawawezi kuwa discarded kwa kiasi hiki. Hakuna anayejua umuhimu wa Wauguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo basi, mimi nasema *structure* kama hii siyo Msahafu wala Biblia, naomba ipitiwe tena ili ifanyiwe marekebisho na marekebisho haya yanapendekezwa na Wauguzi kwamba baada ya Waziri na Katibu Mkuu basi huku kushoto aliko *Chief Medical Officer* na Madaktari wake, kulia aingie *Chief Nursing Officer* na Wauguzi wake. Chini ya *Chief Nursing Officer* kuje *Nursing Quality Assurance Division* ambayo itakuwa na Mkurugenzi. Yupo mtu aliwahi kusema kwamba, Wauguzi hawajasoma; wapo walio na *Ph.D., Masters, Management Skills* na *Administration*. Mwuguzi akishika hii Idara ya Wauguzi kama Mkurugenzi, atawasiliza vizuri sana hawa Wauguzi na shida zao. Baada ya hiyo kuingia na *Nursing Services Curative Section*, *Nursing Services Preventive Section*, *Emergency Preparedness and Response Section*. Hiki kiwe ni kimlolongo ambacho kinaangukia chini ya Kurugenzi

inayoendeshwa na Mwuguzi au inayosimamiwa na Mwuguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wauguzi ni muhimu sana, wapo 30,000 nchi hii na asilimia 60 ya Watumishi wa Afya. Wauguzi ndiyo wanaokaa na mgonjwa saa 24 pale hospitali. Daktari anaweza aka-*prescribe* akaondoka akarudi kuja kumwona mgonjwa baada ya siku nne au tano, lakini Mwuguzi ndiye anayekaa na mgonjwa kwa sasa 24 katika *shift* ya asubuhi, mchana na usiku, Mwuguzi anakuwepo na ndiye anaye-*detect* mabadiliko ya mgonjwa anaendelea vizuri au haendelei vizuri. Mwuguzi anatoa hata dawa ambazo pengine Daktari hakupatikana Mwuguzi anampatia mgonjwa. Nani asiyejua adha wanazopata Wauguzi za mishahara midogo, posho zao, malimbikizo na *promotions* zao? Mwuguzi anaweza akakaa hata miaka 15 hajapata *promotion*. Ukiingia kwenye Vituo vya Afya na Zahanati ndiyo wanao-*prescribe*, hakuna Madaktari kule Wauguzi ndiyo wanafanya kazi. Utakuta pengine hata Zahanati inapoengwa au Kituo cha Afya kinapoengwa, nyumba ya mtumishi anayekuwa *considered* ni Daktari, Mwuguzi anaenda kupanga kijijini na Mwuguzi ndiyo ataitwa hata mara sita au saba kuja kumwona mgonjwa baada ya kazi. Mara nyingine inabidi abebe mtoto mgongoni kwenda kumsaidia mama anayeifungua. Wauguzi wana adha, tunaomba wapewe *directorate* yao, ambako watapeleka haya malalamiko yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwenye Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 44, amezungumzia

kwamba wako mbioni kusikiliza matatizo na malalamiko ya wafanyakazi.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nichukue nafasi hii, kwanza kabisa, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa siku ya leo. Pia naishukuru Serikali kwa kuendelea kubadilisha na kuangalia mifumo mbalimbali ya kuboresha Utumishi wa Umma.

Naomba nisitisize mfumo wa ukandamizi wa kupandisha daraja au vyeo watumishi wa kada mbalimbali, suala ambalo ni muhimu sana kwa Watumishi wote wa Umma. Serikali imeweza kufanya hivyo, yaani *up-grading and re-categorisation* kwa Walimu. Tunawashukuru kwa hilo ambapo limeanza mwaka jana. Tunashukuru kwa upande wa Walimu wamemaliza tatizo, lakini tunaomba sasa iendelee kuangalia Kada zingine zote za Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kutoa mfano; kwa mfano una mtumishi ambaye ana diploma yake labda ni Mhasibu au Afisa Kilimo au Mifugo, yuko katika ngazi fulani, ana uzoefu wa miaka 10 au 15 kule kazini, unakuta labda yupo *TGTS* ngazi E au G au F; lakini anapoenda kuijendeleza kimasomo, anapopata digrii yake akirudi anashuka badala ya kupanda cheo na kuongezewa mshahara, anarudi *TGTS D*, anakuwa sawa na yule mtumishi ambaye anaanza kazi. Mfano, kama mshahara wake ulikuwa Shilingi 800,000 kabla hajaenda kusoma na ana uzoefu wa miaka kumi, unakuta akirudi anaanza na mshahara wa shilingi 400,000 au 450,000. Sasa unakuta mbali na hiyo,

mpaka aje apande tena cheo afikie ile TGTS alipoondoka kwenda kujisomea inachukua miaka kadhaa.

Unakuta muda huo hana kwa sababu tayari alishafanya kazi huko Serikalini kwa miaka 10 au 15 mpaka afikie ngazi ile utakuta mtumishi ameshastaifu, yaani ameshafika muda wa kustaifu. Sasa hiyo inamkatisha tamaa. Wengi wanaenda kujiendeleza lakini hawatoi vile vyeti vyao kwa sababu anajua mshahara utashuka na hatakaa afikie ngazi ile aliyoifika huko mwanzo badala ya kuwa *Senior Officer* anakuwa *Junior Officer*. Pia unakuta yale manufaa ambayo alitakiwa yeye ayapate na Taifa lipate kutokana na kusoma inakuwa haipo.

Huu ni mfumo kandamizi, ambao hauna maslahi na wala haumpi motisha mtumishi kwenda kujiendeleza kimasomo na akirudi katika pensheni yake, yaani mafao yake ya mwisho, kama atakubali kutoa vyeti na aanze daraja la chini, mwisho wakati anastaifu kwenye pensheni yake pia unakuta inamwathiri itakuwa ndogo na ndiyo maana wengi wana vyeti vya digrii au *PhD* lakini wanaendelea kuonesha Vyeti vya *Diploma* tu mradi afikie umri astaifu asipoteze mafao yake mengine. Kwa hiyo, tungeomba Serikali iangalie kama ilivyofanya kwa Walimu iwafanyie watumishi wengine wote ili wakati wanapoenda kusoma wakirudi waweze kupanda daraja na pia mishahara iendelee kupanda badala ya kushuka. Hii itasaidia watumishi wengi baada ya kusoma kutokuhama kutoka katika Utumishi wa Umma kwenda *Private* au kwenda hata nje ya nchi kutafuta

maslahi zaidi wakati wamesomeshwa katika vyuo vyetu kwa kukopa Bodi ya Mikopo au mikopo mbalimbali, labda amesomeshwa na mwajiri wake. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iiangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tunaomba Serikali iangalie kada muhimu ya Utumishi ambayo vibali vingetolewa kwa umuhimu wake. Leo hii fedha zote ambazo zinatolewa na TAMISEMI kwenda kufanya maendeleo katika Wilaya zetu, Wasimamizi Wakuu katika ngazi ya Vijiji ni Watendaji wa Vijiji. Sasa unaweza kuwa na Walimu ukawa na watumishi wengine wote, kama huna Mtendaji wa Kijiji na sehemu nyingi Tanzania tatizo hilo ni kubwa sana hatuna Watendaji wa Vijiji; kwa hiyo, unakuta usimamizi wa fedha na miradi unakuwa haupo. Tungeomba sana Serikali iangalie hasa suala la Watendaji wa Vijiji na Kata ndiyo lipewe umuhimu wa kipekee ili vibali vya kuajiri vitolewe kwa Halmashauri zote ili kada hiyo isiwe na upungufu hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kuchangia ni Sekta ya Maadili ya Utumishi wa Umma. Mimi ninaomba Sekta hii ipewe umuhimu wake, elimu itolewe kwa wananchi zaidi na pia wao wangewezeshwa zaidi ili waweze kufanya kazi yao. Leo hii wapo katika sehemu chache tu ndani ya nchi hii, wangeweza kufanya kazi na wangkuwa na mafungu ya kutosha wangeweza kwenda kufuatilia maadili ya viongozi katika sehemu mbalimbali na tungeweza kugundua mambo mengi. Pia semina mbalimbali zingeendalea kutolewa kwa wananchi, basi sekta hiyo ingeweza kudhibiti mambo mengi ya

ubadhirifu, ambayo leo hii Watanzania wanalamikia ambapo tayari kuna matabaka mawili makubwa ya wale ambao ni matajiri na wale ambao ni wanyonge kabisa. Sekta hii ya Maadili ya Utumishsi wangeweza kusaidia sana katika Sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine muhimu ni pensheni ya wazee. Tunaiomba Serikali iangalie namna ya kuhakikisha kwamba pensheni zao zinalipwa kwa wakati. Hawana nguvu ya kuandamana, hawana nguvu ya kufanya mambo mbalimbali, tunaomba haki zao wapewe. Kwa kuwa tayari wameitumikia Serikali hii kwa muda mrefu hivi unategemea umpe baada ya ye ye kufariki itamsaidia nini! Yeye ameshatumikia apewe haki yake ili na wao waweze kufaidi ajira ambayo waliitumikia kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine muhimu ni suala la *mindset*. Kama nilivyoongea juzi, tunaomba Serikali hasa Sekta hii ya Utumishi wa Umma, ingeendelea kutoa semina mbalimbali ili Watumishi wa Umma wajue suala la *Public Private Partnership (PPP)*. Suala hili halifahamiki sana katika Wizara mbalimbali, lingeweza kufahamika vizuri, naamini kwamba ndani ya mwaka mmoja mtaweza kuona mabadiliko ambayo hayajawahi kutokea ndani ya nchi hii kama *mindset* ya Watumishi wa Umma itabadiika kwa ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la uwajibikaji kazini. Ningombaa kama mlivyofanya kule nyuma wakati mlipoanza marekebisho katika hiyo Wizara, kulikuwa kuna *Customer Charter*, ninaomba iendelee kukumbushwa, Watumishi wengi wamesahau

mambo ya customer charter na huduma kwa mteja na haki za mteja, hiyo mngeweza kukumbushia ili kila mtu ajue haki yake anapofika katika Ofisi za Umma. Mimi naamini kwamba, tunaweza kufanikiwa zaidi na Serikali tayari ina mpango mzuri, naomba tu mwendelee na mpango huo ili Utumishi wa Umma ubadilike na uweze kuleta manufaa na uweze kusaidia wananchi wengi.

Leo hii tabaka la Utumishi wa Umma ni sawa na adui wa wale ambao wanawasimamia iondoke na wawe *friendly*, ijlilikane kwamba watumishi wote ni marafiki wa wananchi ambao wanawahudumia na wao ni watumishi wa wale ambao wako huko bila wao hata huo utumishi usingekuwepo. Kama hiyo ingefanyika, naamini kwamba, nchi hii inaweza kupata mafanikio makubwa sana na tunaomba Wizara hiyo ya Utumishi kama ilivyokuwa huko mwanzo, siku zote inafanya mabadiliko makubwa, lakini pia endeleeni kutoa yale mafanikio yote ambayo mmeyapata kama hii ya *re-categorisation* ya Walimu na *upgrading* hamjaitangaza vizuri, watu wote hawajui, mngeendelea kuboresha ili watu wajue mafanikio ambayo tumepata kwenye Serikali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninawashukuru na pia ningeomba Tume ya Mipango ifike hadi vijijini tupange wote Mipango kwa pamoja.

MWENYEKITI: Kabla sijamwita Mheshimiwa Machali, naomba kusahihisha kidogo, Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya ni kati ya wale ambao hawajachangia hata mara moja. Kwa hiyo, baada ya

Mheshimiwa Machali, nitamwita Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya na Mheshimiwa Jafo atafuatia.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ili nami niweze kuchangia kile ambacho naona kinaweza kulisaidia Taifa letu. Kabla sijaendelea, naomba ninukuu ukurasa wa 55, vifungu au vipengele 64 na 47 kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Anasema kwamba: "Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/13 Serikali inatarajia kutumia shilingi 3,781,100,000,000 kugharimia malipo ya mishahara, upandishwaji wa vyeo na kulipia madai ya malimbikizo na mapunjo ya mishahara kwa Watumishi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Wakala na Taasisi za Serikali."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itusaidie kujua nyongeza ya mshahara kwa Mwaka wa 2012/13 kwa watumishi ni kiasi gani, isiwe tunapewa taarifa ambazo ni za jumla jumla. Pia kama mnashindwa kutueleza kwamba watumishi wanaongezewa mshahara kiasi gani, Walimu ni kiasi gani, Madaktari ni kiasi gani, Mahakimu ni kiasi gani, Wabunge ni kiasi gani, Madiwani ni kiasi gani, tuambieni kila kada inaongezewa kwa asilimia ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia hapa sioni mahali ambapo kuna nyongeza ya mshahara kwa mujibu wa taarifa hii. Kwa sababu taarifa inatueleza bayana, Serikali inatarajia kugharimia kwa kutumia fedha hizo kulipa mishahara, mishahara tunalipwa siku zote, upandishwaji wa vyeo na kulipia madai ya malimbikizo na mapunjo ya

mishahara kwa Watumishi wa Serikali Kuu na Taasisi zingine.

Tutaomba wakati Mheshimiwa Waziri, ana-*wind up* atuambie ameongeza mshahara kiasi gani, maana tumeambiwa kwamba takriban shilingi bilioni 510 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 10.6, hizi zitakwenda kulipa madai. Sasa atuambie ongezeko la mishahara ni kiasi gani, watumishi wanasubiri wanataka kujua; Walimu wanataka kujua, Madaktari na wengine wanataka kujua. Tunaomba atuambie ni kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana ukija pia ukurasa wa 56, kipengele cha 47, pale anasema kwamba: "Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/13, Serikali inategemea kuja kuweka mkazo katika kuandaa mwongozo kwa kutoa motisha kwa watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Aidha, Serikali itafanya utafiti kuhusu mishahara na maslahi ya wafanyakazi baina ya Sekta Binafsi na Serikali kwa lengo la kuoanisha Mishahara ya Watumsihi wa Umma." Mwisho wa kunukuu.

Ninajiuliza katika kipindi cha mwaka 2006 hadi mwaka 2008 na 2009; hivi Mheshimiwa Rais hapa aliunda Tume ya Ntukamazina au Kamati ya Ntukamazina kuweza kupita na kuangalia ni namna gani maslahi ya watumishi yanaweza yakaboreshwa? Leo mnatuambia kwamba, Serikali tutajikita kwenye kufanya utafiti; tafiti hizi mpaka lini kama siyo matumizi mabaya ya fedha? Hizi tafiti kwanza watueleze matokeo ya tafiti ambazo pamoja na kazi zilizofanywa na Tume ya Mheshimiwa Ntukamazina ambaye leo hii

ni Mbunge; zimefanya kazi gani; na zimelisaidia Taifa kwa kiasi gani? Tunazidi kupata hasara na kuzidi kuongeza matumizi ambayo ni *unnecessary*.

Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze sababu za kuweka kapuni, za kuweka kwenye makabati, taarifa ambazo zimetolewa na Kamati ya Ntukamazina; je, zimepuuzwa au hazitakiwi kwa misingi gani? Tunaomba tupate majibu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya umeme naona ni tatizo sijui tutafanyaje. Mambo ya Serikali hayo au mmenizimia mimi peke yangu, lakini nitaona tu.
(Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze kitu kimoja; nilikuwa nimepanga hapa dondo zangu; naomba umeme uwashwe ili niendelee na muda wangu utaulinda. Nitaomba muda wangu uongezwe kwa sababu nimeshindwa kuona dondo ambazo nimeziandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba pia nije kwenye suala la madeni au madai ya watumishi mbalimbali; Walimu, Polisi, Madaktari, Mahakimu na watu wengine kwa ujumla. Ukijaribu kuangalia katika Halmashauri zetu mbalimbali, kumekuwa na ulaghai wa Ofisi za Wakurugenzi kutokuhakiki madai ya baadhi ya watumishi na watumishi kutokulipwa na hasa wahanga wakubwa, naomba nizungumzie Walimu. Maafisa Elimu na Wakurugenzi katika Halmashauri zetu wamekuwa wanakataa kutokuhakiki madai ya watu, wanawaambia kwamba haya siyo madai halali, haya

ni halali halafu na Serikali inakuja kupewa taarifa ambazo ni za uongo. Wakitaka nitibitishe haya nitawaletea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Walimu ambao wanadai fedha za matibabu, wapo Walimu wanadai fedha za masomo, wapo Walimu wanadai fedha za uhamisho na likizo, wako Askari wanadai fedha za likizo na madai mengine hawajalipwa mpaka leo. Vyombo mbalimbali ambavyo ni vya Wafanyakazi kwa mfano, Chama cha Walimu, wamekuwa wanaieleza Serikali mara kwa mara. Mchezo umekuwa ni danadana tutalipa, tutalipa. Mwaka jana mmesema mmelipa na hata mwaka huu. Nasema kwamba, wapo Walimu katika Jimbo la Kasulu Mjini na maeneo mengine na wengine wanatuma *message* hawajalipwa madai yao; Serikali mnachukua hatua gani dhidi ya Ofisi za Wakurugenzi, dhidi ya Ofisi za Maafisa Elimu na dhidi ya Ofisi za *OCDs*; wakati mwingine wamekuwa wanawagandamiza watu hawa ambao ni watumishi wanalitumikia Taifa wakati mwingine kwa uadilifu hawalipwi fedha zao halafu wanaendelea kusumbuka na kunyanyasika huko. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kwa niaba ya Serikali ni kwa nini mnawachezea Watumishi wa Taifa hilli kama vile kichaka cha wendawazimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie pia suala la Serikali ya Jamhuri ya Tanzania na Mikataba ya ulaghai kwa Watanzania kwa sababu kila siku tunaimba suala la Utawala Bora. Hatuwezi kusema kwamba, Tanzania tunapiga hatua kwenye masuala ya Utawala Bora au tuna Utawala Bora wakati bado

tuna Mikataba mibovu ambayo inaendelea kusainiwa mpaka leo hii tunapozungumza. Nenda kwenye Mikataba ya Madini, hakuna Utawala Bora; imegubikwa na usiri na utata ambao umekithiri. Nenda kwenye Mikataba baadhi ya Taasisi ambazo zinatoa huduma ndani ya Taifa letu, kwa mfano Taasisi ya Agha Khan, naomba niitaje nitarudia tena. Tangu tunapata Uhuru, Taasisi ile inasema inatoa huduma kwa watu na inasemekana kwamba taarifa tulizonazo wanapata misamaha ya kodi kwa kiasi kikubwa. Tunapoteza mapato mengi kwa sababu ya Mikataba ambayo imegubikwa na utata. Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU) ni lini mtaingia huko ili mkachunguze Mikataba hiyo na hatimaye Bunge liweze kutaarifiwa na ni hatua gani ambazo zinachukuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unasikia waliokamatwa na rushwa ni wezi wa kuku; hivi hawa makamongo mnaawacha kwa misingi gani? Wanaacha kulipa kodi kwa misingi gani, halafu tunalalamika kwamba Serikali inakusanya mapato kidogo; ndiyo maana mishahara haiwezekani kuongezwa kwa watumishi, ndiyo maana madai mbalimbali ya watumishi hayalipwi na ndiyo maana pesa za likizo hazilipwi. Tunataka tujue ni kwa nini mambo haya yanaendelea kufanyika katika stahili hii? Lini Serikali itabadilika kwa ajili ya maslahi na ustawi wa Watumishi wa Taifa hili?

Ugumu wa maisha ambao unasababisha wakati mwingine ukienda hata kwenye Ofisi kumpata Afisa fulani utakuta matatizo. Wapo wachache ambao kweli wanajitahidi kuwahudumia watu wetu, lakini wengi *the*

system is rotten. Tunaomba tupate ufanuzi ni kwa nini suala la Utawala Bora kwenye takwimu mnatuambia tumezidi kupiga hatua lakini malalamiko ya watu huko nje na huko katika ofisi mbalimbali ni matatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda *CDA* pale wizi mtupu, utakuta kuna kauli ambazo zinatishatisha. Leo tumelalamika tunesema kwamba, tumewapa taarifa hata baadhi ya Mawaziri wetu, kwenye Halmashauri zetu huko wapo watumishi ambao wanaharibu. Kwa mfano, katika Wizara ...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa hii nafasi ili nami niweze kuchangia Hotuba za Bajeti hizi mbili, lakini pia niweze tu kusema kwamba naunga mkono hoja zote zilizotolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, niseme kwamba, nitachangia zaidi katika eneo la Utawala Bora na kwa bahati nzuri kama ulivyotoa ufanuzi asubuhi alisema kwamba sisi hatuulizi maswali tuko upande wa Serikali. Kwa hiyo, leo nitachangia zaidi eneo la Serikali, kwa sababu nina dhamira ya dhati ya kumwunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete katika Hotuba yake aliyoitao jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno nitakayoyazungumza yawezekana wengine hayatawafurahisha, sitapenda yawafurahishe kwa sababu napenda ukweli usikike, Watanzania wasikie na wale wenye kupenda ukweli watafurahi. Mama Teresa alisema: "*Yawezekana usiwe na uwezo wa kumpa mtu kila anachotaka lakini angalau umpe hata furaha.*" Umwoneshe angalau ume-smile ili na yeye iweze kumwongezea maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, mgonjwa anapokuwa Hospitali pale anapoambiwa kwamba hakuna atakayekutibu, anakuwa amenyimwa hata matumaini; ni hali ya kutisha na inakatisha tama. Mimi kama Msomi wa Tanzania nasema; suala hilo linaturudisha nyuma wasomi. Pamoja na kwamba, suala hili lilifikishwa Mahakamani lakini kwa kuwa upande wa pili wamependa kuchangia, siyo vibaya na sisi tukachangia. Kuna suala la mtu kukuomba moyo wako anasema nipe moyo wako usiponipa nitakuua. Kwa hiyo, lugha nyepesi amekuchagulia kifo. Haya ndiyo yanayofanyika kwa wenzetu Madaktari. Nawashukuru sana Madaktari wangu wa Mkoa wa Rukwa, kwa sababu hawajagoma mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kinachohuzunisha na kushangaza, wanaoongoza migomo hii, wanaohitaji migomo hii kwa dhati yote ni wale ambao wako katika Miji Mikubwa, ambao wana fursa ya kwenda kutibu katika hospitali mbalimbali katika hiyo Miji. Kwa mfano, Dar es Salaam wanakwenda Tumaini, wanakwenda Agha Khan, wanakwenda TMJ na kote huko

wanapata hela. Hali kadhalika, wana hospitali zao binafsi na wagonjwa wanaambiwa kwa tatizo hili njoo Muhimbili nitakushughulikia wakati na pesa ameshachukua, lakini haya yote hawayaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa; kwanza, nasema Mwenyezi Mungu ampe afya njema ndugu yetu Dkt. Ulimboka. Nasema kwamba, kutokana na Maandiko, Mungu amemwepusha kuendelea kuongoza mgomo uliokuwa unaondoa uhai wa watu. Mungu amemwepusha kuwa Hitler wa Tanzania. Mungu amemwonea huruma atoke kwenye dhambi hiyo kubwa. Wanaomsaidia kusemasema hapa; tumeshasema mara nyingi, likitokea jambo kabla halijatokea wenzetu wanaanza wanasesmasema siku mbili linatokea. Mimi nilishtuka pia hata Mheshimiwa Martha aliposema siku ile, nikasema nadhani kuna ukweli ndani yake. Kuna ile tabia ya mtu kujipiga kofi shavu la kushoto halafu kujidai kulia mkono wa kulia. CHADEMA mna la kujibu, kwa sababu mnasaidia mgomo huu uendelee. Mnalo la kujibu.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kuhusu Utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(a):
"Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmoja wa Viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na mchangiaji aliyezungumza ...

MWENYEKITI: Samahani, naomba ukae chini. Nimesimama hapa si kukuvunja moyo wala kukatisha maelezo yako. Kwa vile una uhakika wa kile ambacho Mheshimiwa atakuwa amekisema, maana Kanuni hii tukienda ile ya 63 atakuwa amekiuka. Sasa wewe utoe uhakika ambao unaujua kwamba yule anasema sivyo. Ahsante.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilanza kutoa uhakika kwa kusema kwamba, mimi ni Kiongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Mimi ni Mbunge na kwa nafasi yangu ya Ubunge naingia kwenye Vikao vya Chama, lakini ni Mkurugenzi wa Chama wa Habari na Uenezi, Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama na Mjumbe wa Vikao vyote vya Maamuzi vya Chama. Naomba kulihakikishia Bunge lako kwamba, madai yaliyotolewa na mchangiaji kwamba CHADEMA inahusika kwenye migomo inayoendelea siyo ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo kwa kuwa limekwishaingia ndani ya Bunge lako, ili ukweli ujulikane hapa wa chanzo cha hii migomo, tuletewe hapa Bungeni Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, ambayo ilikutana na pande zote; Serikali na Madaktari, itabainika wazi kwamba maelezo tunayopewa humu Bungeni na Serikali ni ya uongo. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge mchangiaji ni Mkuu wa Mkoa, anatoa maelezo ya uongo Bungeni, kuendeleza propaganda za Serikali dhidi ya raia ambao tunawawakilisha, ili ukweli ujulikane taarifa hizi ziletwe hapa Bungeni na Bunge lizijadili.

TAARIFA

MHE. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU:
Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Acha Mheshimiwa Mnyika amalizie.

MHE. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa kwa huyu
aliyekuwa anasema.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika umemaliza?
Mheshimiwa Mwigulu naomba ukae chini.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti,
ninaomba aliyetoa kauli ya kukituhumu Chama cha
CHADEMA athibitishe. Naomba vilevile ili Bunge lako
Tukufu lipewe nafasi kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya
63(2), kuisimamia Serikali kuhusu migomo
inayoendelea, tuletewe Taarifa iliyotumia fedha za
walipa kodi za miezi miwili ikakutana na Madaktari na
Serikali ikaahidi Taarifa hiyo italetwa Bungeni humu na
haijaletwa Bungeni na Serikali inafanya *propaganda*
mtaani kwa kutumia taarifa za upande mmoja.
Tuletewe hapa tuweze kuisimamia Serikali.

TAARIFA

MHE. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU:
Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa aliyetoka kusema. Kwa ajili ya muda, naomba niseme kupitia Kanuni ya 68(8).

MWENYEKITI: Naomba uisome.

MHE. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU:

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema: " *Vilevile Mbunge ye yote anaweza kusimama mahali pake na kusema taarifa na kwa ruhusa ya Spika atatoa taarifa au ufanuzi kwa Mbunge anayesema, ambapo atamtamka Mbunge aliyekuwa anasema aketi kusikiliza taarifa hiyo.*"

Mheshimiwa Eng. Manyanya, alipokuwa anaongelea kuhusu uchochezi ule na kuhusu kuhusika kwa Chama hiki, Kiongozi mmojawapo wa Chama ametokea kukanusha. Mimi siendi mbali, nataka kulithibitishia Bunge na Watanzania jinsi ambavyo hawa wenzetu wameshiriki. Katika taarifa yao ya leo ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kuanzia ukurasa wa 26 pale lakini imetokea ukurasa wa 21, kuhusu migogoro baina ya Serikali na Watumishi wake wameongelea.

MWENYEKITI: Samahani, hebu niongoze; sehemu gani?

MHE. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia ukurasa wa 21, inaongelea migogoro baina ya Serikali na Watumishi wake. Wameelezea migogoro yote ikiwemo na hii ya Madaktari na mwisho pale kwenye ukurasa wa 26 wao

wenyewe kwa kutambua migogoro iliyokuwa inaendelea na njia iliyokuwa inatumika kudai hiyo haki kwamba ilikuwa ni migomo, wao wamesema ukurasa wa 26: "*Rai yetu kwa Watumishi wote wa Umma waendelee kupigania haki zao na sisi tutaendelea kuwaunga mkono.*" Wanaunga mkono mgomo hawa halafu wanasema hawahusiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hili la ndugu yetu Ulimboka, hawa CHADEMA kuna Mbunge wao wa Rombo alipata ajali mbaya karibu na kifo, hawajawahi hata kwenda kumsalimia wala kumpigia simu. Leo hii kwa Ulimboka kwa sababu kuna kazi walimtuma wanallilia kimbelembale. Hivi kweli leo hii amekuwa ndugu yenu kule yule wa Rombo?

WABUNGE FULANI: Boya, boyo!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ina haki ya kujibiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Manyanya, endelea. Nadhani taarifa hizi zimefika kwa wahusika. Sasa naomba tuendelee; Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba kwa wale wenye taarifa basi waniache nimalizie ili waweze kutoa taarifa nyingi zaidi kwa sababu bado naendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kudhihirisha hayo pia katika misemo inayozungumzwa inasema kwamba,

waliokuwa wamemchukua huyo bwana walikuwa sijui na mavazi; lakini ukiangalia mavazi kama ni ya askari yanafanana sana na Magwanda ya CHADEMA. (*Kicheko*)

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, kaa chini. Tafadhalii endelea.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Sikuruhusu.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Kwa hali hiyo basi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Manyanya, kaa chini.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mzungumzaji aliyezungumza na ni Kanuni ya 61(1)(a) inasema kwamba, hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli na hatatumia lugha inayodhalilisha watu wengine. Mzungumzaji aliyezungumza kwanza ametoa taarifa zisizokwu za ukweli kwamba waliomteka nyara Dkt. Ulimboka na kumjeruhi ni watu waliokuwa wamevaa magwanda na kwamba ni watu wanaofanana na CHADEMA na ni udhalilishaji kwa wengine sisi wa CHADEMA.

Niseme kwamba, mzungumzaji anapaswa kufahamu kwamba, kwenye Vyombo vya Habari na Kanuni zetu za Bunge zinasema; Mbunge hatahesabika kuwa anasema jambo la uongo kama atanukuu taarifa za vyombo vya habari.

Kwenye vyombo vya habari, Dkt. Ulimboka bahati nzuri yuko hai, amenukuliwa mwenyewe akisema kwamba, waliomteka nyara ni Askari Polisi na wengine amewataja kwa majina. Sasa kama Askari wa Polisi ni CHADEMA, Mkuu wa Mkoa ambaye ni sehemu ya Serikali, atueleze hapa kwamba Askari wale ni wa CHADEMA? (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mimi nadhani Mheshimiwa Mnyika, ilikuwa kwanza ukarushe Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani hapa ili tuanzie pale, kwa sababu... kaa chini.

Kwa kuwa umeshindwa kujibu hoja ambayo Mheshimiwa Mwigulu alitoa taarifa kutokana ... kaa chini basi, mbona unawashwawashwa! Umeshindwa kuheshimu taarifa ambayo umepewa na Mheshimiwa Mwigulu. Mimi ningependa kuona umahiri wako kama Mkurugenzi wa Habari wa CHADEMA, ukarushe taarifa hii ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani hapa kwanza tuendelee, lakini badala ya kujibu hoja hii umerukia nyingine. Mtayumbisha Kiti, tungeenda taratibu hoja kwa hoja *then* tunakwenda mbele, lakini umeshindwa kujibu hili. Kwa kuwa ulishindwa kujibu hoja hii na kwa kuwa muda hauruhusu, naomba nimwachie Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya aendelee.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nafasi ya kujibu hilo.

MWENYEKITI: Kaa chini. Mheshimiwa Moses Machali, kaa chini. Mheshimiwa Machali, una tatizo moja; kudandia hoja za watu. Usitake umaarufu hapa kaa chini. *Sergeant-At-Arms* mtoe nje Mheshimiwa Moses Machali. Naomba atoke nje ya *gate* arudi kesho asubuhi. (*Makofî*)

(*Hapa Mhe. Moses Machali Alitolewa Ukumbini*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Manyanya, endelea.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa busara zako, lakini niseme tu kwamba ni maana ya rai ya Mheshimiwa Rais; ndiyo maana Mheshimiwa Rais amelihutubia Taifa na akasisitiza kuwa, anataka kuhakikisha kwamba Vyombo vyake vya Ulinzi na Usalama vihakikishe vinafuatilia kwa umakini na kuweza kubaini nani amehusika na vitendo hivyo. Hii yote ni kwa sababu ya kutuondoa sisi kwenye nafasi hii ya kutupiana madongo humu ndani. Kama ni suala la kutupa madongo, kila mtu anao uwezo wa kutupa dongo. Je, tutakuwa tumefikia usuluuhishi; na hapo ndiyo maana nasema mjifunze kwamba hata sisi huku tunayo ya kuwaambieni ninyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kusisitiza kwamba, kila mtu anamtegemea mwenzake, Polisi kama utakumbuka ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda umekwisha, nakushukuru.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu ulichukuliwa.

MWENYEKITI: Naomba uendelee.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakumbuka, najaribu kuangalia yale ambayo yalijitokeza moja kwa moja. Baada ya kutokea lile tatizo tayari Dkt. Mkopi aliomba Vyombo vya Usalama vifanye kazi, kwa maana hiyo tunategemeana. Kuonesha kwamba, mwananchi au huyu ambaye anakuwa ameenda hospitali kakosa matibabu anapata tabu kiasi gani? Madaktari waone jinsi ambavyo walimhudumia mwenzao.

Kwa hali hiyo basi inaonekana kwamba, hata kama wanasema kuna mgomo wenzetu bado wanatoa huduma kwa ndugu zao, lakini wanaokufa ni wale wasio na ndugu. Sasa niungane na alivyosema Mheshimiwa Kasikila, kuna wagonjwa wanaotoka Sumbawanga wanafuata huduma Dar es Salaam, kuna wengine wanafuata huduma Mbeya au KCMC, wanafika pale wanakuta kuna mgomo; na ukiangalia hata katika *distribution* ya watumishi, unakuta kuna baadhi ya maeneo hayana watumishi wenye asilia na huko pengine nao wangepata uchungu wa

kuwasaidia ndugu zao. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba, hizi rasilimali za Taifa, hizi ajira za Taifa, zisambazwe kwa kadiri ya mtazamo wa nchi nzima ili kila mtu anapokuwa kwenye utumishi, aweze kukumbuka umuhimu wa kusaidia ndugu zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naungana na maneno yote aliyoyazungumza Mheshimiwa Rais wetu jana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge, naomba niwakumbushe Kanuni zetu; haya maneno ya sijui nini, hayatusaidii. Naomba tutunze nidhamu, tuongozwe na hizi Kanuni, lakini kwa sababu tunafanya ushabiki Watanzania wanashindwa kutuelewa kama kweli tunastahiki sisi kuwa Wawakilishi wao. Tunazungumza masuala ya msingi hapa, naomba tuzingaite, tunafahamu Kanuni zinazuia kuongea bila ruhusu ya Kiti lakini mmefanya Bunge kama klabu. Bunge siyo klabu ni Chombo cha juu sana, wenyewe mmesema Bunge lina jukumu la kuisimamia Serikali; hivi kweli tunasimamia Serikali?

Mnapofanya hivi, mnazomea, makofi yasiyokuwa na msingi, nadhani tunataka kupoteza heshima yetu. Nawakumbusha kulinda heshima yetu kama Wawakilishi wa Wananchi. Hapa hatujibishani kama tupo sokoni, tunajibishana kwa hoja. Hoja ikitolewa tuijibu kwa ustaarabu. Sasa kama hoja inatolewa hujibu kwa ustaarabu, siyo jambo jema. Naomba tunapoendelea tuendelee kujadili katika hali ya umakini. Tuisaidie Serikali, pale ambapo tunahisi

inahitaji kukumbushwa basi ni wajibu wa Bunge kama Wawakilishi wa Wananchi kufanya hivyo.

Baada ya kusema hayo, kwa vile muda hauruhusu, naomba niwataje watakaonza kuchangia saa tatu baada ya maswali na majibu; Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour na wengine wataendelea. Nawashukuru, jioni njema. Naomba kuahirisha Shughuli za Bunge.

(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 3 Julai, 2012 Saa Tatu Asubuhi)

